SUPA JACKPOT
TZS. 1,058,211,696
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**ALIYESIMAMISHWA** nafasi nyeti CWT arudishwa kazini




UKURASA 13

Jumamosi Desemba 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581162

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mama adaiwa kuwaua wanawe na kujinyonga

## **VICOBA**, mgogoro wa ardhi vyatajwa... *Endelea Uk. 2*




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akizungumza katika mkutano wa viongozi wa Afrika na Marekani, wakati wakijadili masuala ya kilimo, usalama na uzalishaji wa chakula, uliofanyika katika ukumbi wa Convention Centre, Washington DC, Marekani juzi. **PICHA: IKULU.**

## Matatani kwa tuhuma kuchoma nyaraka za ununuzi wenye shaka

UKURASA 2

## Watiwa pingu kumwozesha mwanafunzi usiku mnene

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA SC KAZI NI ILE ILE** UK. 32 **KATUNI** UK. 6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na watumishi wa Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Maurus, Chemchemi mjini Sumbawanga, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Rukwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mama adaiwa kuwaua wanawe na kujinyonga

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

Mkazi wa eneo la Namanditi, Manispaa ya Songea, Amina Maketu (34), anadaiwa kuwaua watoto wake wawili kisha na yeye kujinyonga.

Maketu anadaiwa kuwauwa watoto hao, mmoja kwa kumnyonga na mwingine kwa kumpiga na kitu kizito kichwani na hatimaye kuchukua uamuzi wa kujinyonga kwenye chumba alichokuwa analala.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa Ruvuma, Marko Chilya, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Desemba 15, mwaka huu.

Chilya aliwataja mbali na Maketu, wengine waliofariki dunia ni Jessica Komba na Jennifer Komba mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi minane.

Kamanda Chilya alisema chanzo cha tukio hilo ni ugomvi wa mgogoro wa ardhi kati Maketu na ndugu zake na kwamba kabla hajajinyonga, aliacha ujumbe wa maandishi unaoeleza kuwa amejiua yeye na watoto wake ili asije akawaacha wakipata taabu duniani.

Alisema taarifa za awali pia zinaeleza Maketu alikuwa anakabiliwa na madeni kwenye vikoba, hivyo Polisi inaendelea kufanya upelezi kwa kina ili kubaini ukweli halisi wa chanzo cha tukio hilo. Mwanamke huyo imeelezwa pia alikuwa ametengana na mume wake kwa muda mrefu.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololeti Mgema, akiwa kwenye eneo la tukio, alionyesha kusikitishwa na kitendo hicho ambacho kimesababisha mshtuko mkubwa kwa wakazi wa Songea.

Mgama aliwaomba majirani waone umuhimu wa kutoa ushirikiano na polisi wakati uchunguzi wa vifo hivyo unafanywa ili chanzo cha tukio kifahamike.

Peter Komba mkazi wa Namanditi, ambaye ni mzazi mwenzake na Maketu, akizungumza kwa majonzi, alisema mwanamama huyo alikuwa mke wake lakini walishatengana.

Alisema licha ya kwamba walitengana, alikuwa anafanya naye mawasiliano vizuri na hakuwahi kumwambia kama alikuwa na matatizo yaliyomfanya awaue watoto na yeye kujiua. Alisema jambo hilo limemwumiza sana kwa kuwa alikuwa anawapenda sana watoto wake ambao alipokuwa akikutana nao, walikuwa wanaonyesha nyuso za furaha.

Zainabu Hamisi, mkazi wa Namanditi, alisema walikuwa wakiishi vizuri na Maketu na muda wote alikuwa mcheshi na pia aliishi vizuri na majirani. Pia alisema hivi karibuni kulikuwa na sherehe mtaani ambayo Maketu alikuwa mshereheshaji, hivyo anashindwa kuelewa ni magumu yapi aliyokutana nayo ambayo yalimfanya aamue kuchukua uamuzi mgumu kama huo.

Rashidi Athumani, mkazi wa Namanditi, alisema tukio hilo bado limekuwa na taharuki kwa wakazi wa Namanditi na maeneo mengine ya Songea.

Alisema licha ya muda wote waliokuwa wakiishi naye Namanditi, Maketu alikuwa raia mwema na alikuwa anaongea na watu vizuri jambo ambalo limewashangaza kwa kufanya ukatili huo wa kuua wanawe na yeye kujiua kwa kujinyonga.

Mkazi huyo aliliomba Jeshi la Polisi kupitia dawati la jinsia, kutoa elimu ya jinsia kwa wananchi kwa kila kata ili kuondokana na matatizo wanayoweza kukutana nayo ambayo yanaweza kusababisha kifo kama tukio lililotokea.

# Matatani kwa tuhuma kuchoma nyaraka za ununuzi wenye shaka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amewakabidhi kwa Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mhasibu wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Eric Rutyamirwa, na Mkufunzi wa chuo hicho, Godfrey Msenuka, kwa tuhuma za kuchoma nyaraka za mradi wa ujenzi wa chuo.

Rutyamirwa na Msenuka ambaye alikuwa katibu wa ujenzi, wanadaiwa kuchoma nyaraka hizo, hivyo kupoteza kumbukumbu za ujenzi wa mradi huo ambao ununuzi wa vifaa vya ujenzi unadaiwa kufanywa mara tatu zaidi ya gharama halisi.

Majaliwa aliwakabidhi watendaji kwa TAKUKURU juzi baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo unaojengwa katika kijiji cha Pito, Sumbawanga mkoani Rukwa.

Ujenzi wa mradi huo unaojengwa kwa awamu mbili, unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 7.1 na tayari serikali imeshatoa Sh. bilioni 3.8 kwa ajili ya awamu ya kwanza. Mradi huo ulianza Agosti, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Januari, mwakani.

Waziri Mkuu alisema baada ya kubaini kuwapo kwa matumizi mabaya ya fedha za mradi huo na wizara husika kupanga kwenda kufanya uchunguzi, ofisi ya mhasibu ambayo ilikuwa na nyaraka iliungua.

"Nyaraka ziliungua ndani ya ofisi ya mhasibu huku chanzo cha moto kikiwa bado hakijajulikana lakini mfumo wa umeme haukuwa na hitilafu. Ulikuwa salama hata baada ya tukio la moto kutokea," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Mkuu alihoji kwa nini mhasibu wa chuo alijipa kazi ya kutunza nyaraka za ujenzi kinyume cha taratibu kwa sababu aliyepaswa kuwa na nyaraka hizo ni katibu wa kamati ya ujenzi, hivyo aliagiza wote wachunguzwe.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alitangaza kuivunja kamati ya ujenzi ili kupisha uchunguzi na kuunda kamati mpya ambayo itasimamia ujenzi hadi utakapokamilika.

Katika hatua nyingine, Kipanga alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassam ameridhia kutoa Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kujenga upya vyuo vitano vya ualimu vya Sumbawanga, Morogoro, Tabora, Ngara na Kasulu.

Pia alisema fedha hizo zitatumika katika ukarabati wa vyuo vingine 30 vya ualimu vilivyoko katika maeneo mbalimbali nchini. Serikali ina jumla ya vyuo vya ualimu 35.


**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration**
**Cause No.178 of 2022**
**In the matter of the Estate of the late of the late NORAH IDD KAEGA**
**Of Kizota within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by ANNA KAEGA LUPANGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**
All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16th Day of January, 2023
Dated at Dodoma this 14th day of December, 2022
RESIDENT MAGISTRATE

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 41/2022**
**BENO NYONI ----- MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**RAJESH WILLIAM -------- MJIBU MAOMBI .**
**WITO /KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi anataarifiwa kuwa Muombaji amefungua shauri la mgogoro wa Ardhi dhidi yako .Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 22/12/2022 saa 2:00 asubuhi kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi .

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 22/11/2022.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF MEATU**
**AT MWANHUZI**
**MISC CIVIL NO.3/2022**
**IRENE RAPHAEL LYANGA-APPLICANT**
**VERSUS**
**GODFREY ZEPHANIA-RESPONDENT**
**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Hearing/Mention on the 19 day of January,2023 at 8:00 Am to the forenoon.

**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to really in support your case.

Given under my hand and the seal of the Court this 13 Day of December 2022.
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
MEATU

**BE SERVED UPON**
**GODFREY ZEPHANIA**
**MAKAO VILLAGE**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**VAINESS FESTON MINJA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0679/061 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIMANDOLU SECONDARY SCHOOL mwaka 2017.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MBE/MBE/RB/477204/2022**

## HABARI KITAIFA

# Kigogo aliyesimamishwa CWT arejeshwa kazini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) umemrejesha kwenye nafasi ya urais wa chama hicho, Mwalimu Leah Ulaya baada ya kuridhika na utetezi alioutoa dhidi ya tuhuma zilizokuwa zikimkabili huku akiahidi kuvunja makundi na kutolipa kisasi.

Leah alisimamishwa kipindi cha mwaka mmoja na miezi mitatu kwa tuhuma matumizi mabaya ya madaraka ikiwamo kudaiwa kuidhinisha kumlipa Sh. milioni 300 kiongozi mstaafu wa CWT, Ezekiah Oluoch.

Mkutano huo pia umeazimia kuwafuta uanachama Deus Seif ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa CWT na Mwekahazina wa CWT, Aboubakar Allawi kutokana kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela baada ya kupatikana na hatia ya kutumia madaraka yao vibaya kwa kuchepusha Sh. milioni 13.9 ambazo ni mali ya CWT na hivyo kukosa sifa ya kuwa viongozi na wanachama.

Uamuzi huo wa mkutano mkuu ulifanyika jijini hapa jana chini ya Mwenyekiti, Selemani Ikomba.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Rais Leah alishukuru mkutano mkuu kwa kumpa nafasi ya kusikiliza utetezi wake kwa kuwa tuhuma hizo zilimfanya awe nje ya chama tangu Septemba 16 mwaka 2021.

"Ninawapongeza sana kwa kusimamia chama kuwa imara, tuendelee kumwomba Mungu ili tusiingie kwenye ghadhabu. Mimi ninawahakikishia kuvunja makundi yote yanayoendelea, niwahakikishie kuwa hakuna visasi, niwahakikishie mshikamano wetu utaendelea si kama ilivyokuwa nyuma, bali ni zaidi ya hapo," alisema.

Leah alisema kijiti alichopokea kutoka kwa Gratian Mkoba ataendelea kukifanyia kazi ili chama kiwe imara.

Wakati wa mkutano huo, Oluoch alisema: "Mimi kwa kweli ninapenda kuwaambia mlifanya uamuzi mzuri, huyu mama alituhumiwa kwamba kutokana na uamuzi aliofanya amesababisha chama kupata hasara nikalipwa Sh. milioni 300 wakati sijalipwa hata senti tano."

"Kama kulikuwa na mahali analegalega sasa hatalegalega, hii ni taasisi ambayo inabeba asilimia 60 ya watumishi wa umma, nikuombe kwa sababu umerejeshwa kazini, mimi mkataba wangu tangu uishe Juni 2020 sijalipwa fedha za kurejeshwa nyumbani kwetu Rorya," alisema.

Mkutano huo pia ulimwidhinisha Japhet Maganga kuwa Katibu Mkuu wa CWT kuchukua nafasi ya Seif kutokana na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela.

Maganga alisema: "Niwasihi tu kama walivyosema wazee wetu kina Mkoba, tukipende chama na sio mtu. Niwaahidi nitaendelea kuwa mtumishi wenu, nitumeni na sitakibeba cheo mabegani."

**ASUSIA MKUTANO**

Kabla ya kufikia uamuzi huo, kuliibuka mvutano kati ya Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani na wajumbe na kulazimika kususa kuendesha mkutano huo baada ya kutaka kubadilisha ajenda zilizokuwa zimepangwa hususan kipengele cha kujadili masuala ya viongozi waliosimamishwa.

Mvutano huo uliibuka pale Kaimu Rais huyo alipotaka ajenda hiyo iliyokuwa namba tatu iwe ya saba badala ya kufuata mpangilio wa ajenda uliokuwa umepitishwa na wajumbe.

Hali hiyo ilisababisha Kaimu Rais huyo kuzongwa na baadhi ya wajumbe akiwa kwenye kiti na kulazimika kuahirisha mkutano. Juzi mkutano huo uliahirishwa tena kwa sababu ambazo zilidaiwa zilitokana na ajenda hiyo.

Baada ya kuondoka ukumbini kutokana na shinikizo la wajumbe, walimchagua mwenyekiti wa muda kuendesha mkutano huo ambao ulimpa nafasi kusikiliza utetezi wa Leah na viongozi wengine waliokuwa wamesimamishwa.

# Mwili wa Balozi Mushy kuzikwa Moshi Jumanne

**Na Romana Mallya**

MWILI wa Balozi wa Tanzania nchini Austria, Celestine Mushy, unatarajiwa kuzikwa Jumanne nyumbani kwao, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Balozi Mushy alifariki dunia Jumanne wiki hii katika ajali iliyotokea eneo la Mkata wilayani Handeni mkoani Tanga, baada ya gari alilokuwa akisafiria kugongana na lori la mizigo na kuungua moto akiwa ndani.

Akizungumza na Nipashe jana, mdogo wa marehemu, Ernest Mushy, alisema Balozi Mushy anatarajiwa kuzikwa Jumanne nyumbani kwao, Kibosho, wilayani Moshi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mushy atakumbukwa kwa umahiri wake mkubwa katika masuala ya kidiplomasia.

"Wakati wa uhai wake, Balozi Mushy ameitumikia serikali katika nafasi mbalimbali zikiwamo Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa katika Wizara hii, Kaimu Katibu Binafsi wa Waziri Mkuu katika Serikali ya Awamu ya Nne na Katibu Tawala Msaidizi wa Masuala ya Uchumi, Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara.

Taarifa hiyo ilisema wizara hiyo kwa kushirikiana na familia ya marehemu, inaendelea na mipango ya maandalizi ya mazishi.

# Watiwa pingu kumwozesha mwanafunzi usiku mnene

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kumwozesha mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka 16 (jina linahifadhiwa).

Watu hao, wakazi wa Kijiji cha Shaba, Kata ya Mtimbwilimbwi, Halmashauri ya Nanyamba, wanadaiwa walipanga ndoa hiyo kufungwa usiku ili waoaji na familia ya mwanafunzi wafanikishe mpango huo bila kufahamika, huku ikidaiwa kuwa ilihudhuriwa na watu wachache.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Nicodemus Katembo, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Desemba 12 mwaka huu, kwenye kijiji hicho majira ya saa nne usiku.

Alisema kuwa usiku wa siku hiyo, Radhamani Saidi (38) ambaye ni baba wa mwanafunzi huyo, akishirikiana na mzazi mwenzake, Mwajuma Chilungu (34), mkazi wa Magomeni mkoani Mtwara, walimwozesha mtoto wao ambaye ni mwanafunzi wa sekondari huku wakijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Kamanda Katembo alisema wazazi hao walimwozesha mwanafunzi kwa Hamisi Chiwandi, mkazi wa Charambe mkoani Dar es Salaam na kwamba katika ndoa hiyo, bwana harusi aliwakilishwa na Radhamani Lingwala, mkazi wa Magomeni, Mtwara.

Alisema kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi linawashikilia watu hao watatu ambao ni baba, mama wa mwanafunzi huyo pamoja na mwakilishi wa bwana harusi. Alisema polisi wanaendelea na utaratibu wa kisheria na kwamba watu hao watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya kumwozesha mwanafunzi.

Kamanda Katembo alisema Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu vitendo vya kikatili dhidi ya watoto na kuendelea kukemea ili jamii itambue na kuwathamini watoto na wanawake kwa ujumla.

Baadhi ya ndugu na majirani wa mwanafunzi huyo, waliiambia Nipashe kuwa walishangazwa kuona mwanafunzi huyo akifunga ndoa huku akiwa anasoma na kujiuliza imekuwaje wazazi wake wameridhia ndoa hiyo kufungwa.

Saidi Machapa, babu wa mwanafunzi huyo, alidai kuwa alipoona mchakato wa mjukuu wake kutaka kuolewa, alimwita na kukaa naye na kumuuliza sababu za kutaka kuolewa wakati bado mwanafunzi na akajibiwa kuwa ameshaacha shule ndiyo maana anataka kuolewa na haoni sababu ya kutokuolewa.

Alisema alimsihi mjukuu wake kuachana na mpango huo wa kutaka kuolewa na kuendelea na masomo lakini mwanafunzi huyo alikataa na kumweleza kinagaubaga kwamba hayuko tayari kuendelea na masomo.

Shangazi wa mwanafunzi huyo, Rukia Machapa alisema mwanafunzi huyo alikataa ushauri wa ndugu zake ambao walimshauri kutokukubali kuolewa akiwa bado mwanafunzi na sheria hairuhusu mwanafunzi kuolewa.

"Tulipomshauri alisema hataki shule, anataka kuolewa na kama wazazi wataendelea kumkataza kuolewa, basi atalazimisha kushika ujauzito na mpenzi wake anayetaka kumuoa ili aone kama wazazi wataendelea kumkataza kuolewa na pia atatoroka kwenda Dar es Salaam kwa mpenzi wake," alidai Rukia


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAFUNZO ATAMIZI YA UVUVI**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inakaribisha maombi kutoka kwa vijana wa Kitanzania waliohitimu mafunzo katika fani ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ili waweze kujiunga na mafunzo vitendo (Atamizi). Mafunzo haya yatahusisha ufugaji Majongoo Bahari, samaki kwa njia za Vizimba na Mabwawa. Vilevile, itatolewa elimu ya Ujasiliamali.

1. Sifa za Mwombaji
   i. Mwombaji awe kijana wa kitanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18). Wanawake na Watu Wenye Ulamavu wanapewa kipaumbele.
   ii. Awe amehitimu mafunzo ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada katika fani za Uvuvi, Ukuzaji Viumbe Maji na fani nyingine zinazohusiana na hizo.
   iii. Awe tayari kupata mafunzo katika mkoa atakaopangiwa ambayo ni Kagera, Geita, Mwanza, Simiyu, Mara, Pwani, Dar es salaam na Mtwara.

**2. Muda wa Mafunzo:-**

Mafunzo hayo yatatolewa bure kwa muda wa miezi mitatu (3). Wanufaika wa mafunzo watajitegemea kwa chakula na malazi. Aidha, Serikali itatoa kiasi cha shilingi 150,000/= kwa kila mnufaika kwa mwezi.

**3. Jinsi ya kutuma Maombi**
   i. Maombi yaambatanishwe na nakala ya vyeti pamoja na wasifu (CV).
   ii. Barua inayoeleza nia ya kujifunza (motivation letter) na uzoefu ulionao katika uvuvi na ufugaji wa samaki.
   iii. Maombi yote yatumwe kwa Katibu Mkuu, Sekta ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, S.L.P 2847, Mji wa Serikali, Mtumba, Mtaa wa Ulinzi, 40487-Dodoma kupitia barua pepe ps@uvuvi.go.tz
   iv. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 30 Disemba, 2022 na mafunzo yanatarajiwa kuanza Mwezi Januari na kukamilika mwezi April, 2023.
   v. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Anthony Dadu, Mkurugenzi Msaidizi, Huduma za Ugani-Uvuvi. **Simu 0652502711, 0627863785, E mail:- anthony.dadu@uvuvi.go.tz**

**Imetolewa na :**
**KATIBU MKUU - UVUVI**

217198301

# Kamishna aonya vitisho kwa wanafunzi

**Na Mary Geofrey**

KAMISHNA wa Elimu nchini, Dk. Lyabwene Mtahabwa amewataka walimu kuacha tabia ya kutumia vitisho wakati wa kufundisha wanafunzi kwa kuwa vinaathiri mwenendo wa kujifunza wa mwanafunzi.

Alitaja vitisho hivyo ni pamoja na baadhi ya walimu kutumia kauli za kuwakatisha tamaa wanafunzi au kuwahukumu na kuwachapa pale wanapokosea.

Dk. Mtahabwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari, akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Francis Michael kwenye kikao cha wadau wa Mradi wa Kuboresha Walimu Tanzania uliofadhiliwa na Serikali ya Canada.

Aliwataka walimu kutumia busara, hekima na upendo kuwaelimisha na kuwaonya watoto hao kwa sababu ni njia zinazoonyesha kusaidia wanafunzi wengi kubadili tabia kuliko kutumia adhabu na vitisho.

"Mwalimu aliyejawa na upendo anaweza kufanya wanafunzi wote kuwa na matokeo bora ya masomo.

"Kitendo cha kutumia viboko wakati wote siyo mtazamo sahihi. Wanafunzi hawalingani uwezo na hivyo wanatakiwa kufundishwa kwa upendo.

"Vitisho vinaua elimu kwa wanafunzi wa Tanzania, mradi huu umelenga kubadili walimu kuwa na mtazamo wa kuwajenga wanafunzi zaidi," alisisitiza.

Mratibu wa Mradi huo wa kuendeleza elimu ya walimu, Cosmas Mahenge alisema una thamani ya dola za milioni 53.

Alisema mradi umejikita kuimarisha elimu kwa walimu nchini wa ngazi ya astashahada na stashahada, kutoa mafunzo zaidi ya mara moja kwa wakufunzi 1,300 yakiwamo ya TEHAMA, usawa wa kijinsia, mafunzo ya kufundishia na utaalamu wa ualimu.

Alisema kupitia mradi huo, wametoa vifaa vya TEHAMA kwenye vyuo, uunganishaji wa vyuo 35 kwenye Mkongo wa Taifa wa TEHAMA na ujenzi na ukarabati wa vyuo.

Alisema ukarabati umefanyika kwa vyuo saba na kujenga maktaba kubwa za kisasa, maabara za TEHAMA na sayansi.

Mwenyekiti wa Wakuu wa Vyuo vya Ualimu nchini, Augustine Sahili alisema walimu wamepata mafunzo yanayowapa mwongozo wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi nchini.



WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akizungumza na waandishi wa habari na sehemu ya menejimenti ya ofisi hiyo wakati akitoa taarifa ya uzingatiaji na utekelezaji wa kanuni na mwongozo wa biashara ya kaboni jana, jijini Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Makalla amaliza mgogoro wa barabara Kigamboni

**Na Faustine Feliciane**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amemaliza mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi Kimbiji, Manispaa ya Kigamboni, kwa kuagiza barabara ifunguliwe baada ya mwekezaji, kampuni ya ASM, kujenga ukuta na kuifunga.

Makalla jana alifanya ziara ya pili kwenye eneo hilo la mgogoro na kufanya kikao cha pamoja kati ya wawekezaji wa maeneo hayo, wananchi, viongozi na wataalam wa ardhi kutoka Manispaa ya Kigamboni na wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Alisema wameamua mwekezaji ASM alipwe fidia na ukuta huo ubomolewe ili barabara hiyo ya asili iendelee kutumika kama ilivyokuwa awali.

"Baada ya kupitia vielelezo vya ramani ya mipango miji toleo la mwaka 2021, tumeona hakuna uhalisia wa kuanzisha barabara mpya. Tumeona barabara hii ya zamani inafaa. Sasa nimeagiza leo (jana) hii huyu mwekezaji aandikiwe barua na imfikie leo hii kumwarifu juu ya uamuzi huu," alisema.

Makalla pia alisema kwa kuwa tathimini ya awali ya kumlipa fidia mwekezaji huyo ilishafanyika, mchakato huo uendelee na ASM alipwe fidia ili barabara hiyo ianze kutumika.

"Gharama ya kuanzisha barabara mpya ambayo tumeonyeshwa hapa ni kubwa zaidi kuliko kumlipa fidia huyu mwekezaji. Sasa maamuzi ya kikao tulichofanya ni hayo, utekelezaji wa kulipa fidia uanze mara moja, tumefanya hivi kwa manufaa mapana ya nchi" alisema.

Mgogoro huo wa ardhi umedumu kwa takriban miaka saba kutokana na ASM (T) Ltd, inayomiliki viwanja pacha vinavyotazamana katika kijiji cha Mikenge kata ya Kimbiji, kuziba barabara inayoelekea kwenye ufukwe wa bahari na kwa wawekezaji wengine.

Wananchi na wawekezaji wengine ambao walikosa barabara ya kupita walilalamika kwa Manispaa ya Kigamboni na kuomba barabara hiyo ifunguliwe.

Hata hivyo uongozi wa Manispaa ya Kigamboni kwa kushirikiana na ASM, walianzisha barabara nyingine iliyopita kando ya mto unaomwaga maji baharini kitendo ambacho wananchi hao walikipinga.

Akizungumza baada ya uamuzi huo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mikenge, Lameck Mayala, alisema uamuzi huo ni wa busara na waliusubiri kwa muda mrefu.

"Kiukweli tunaishukuru sana serikali kupitia kwa mkuu wetu wa mkoa kwa maamuzi haya. Hii barabara ilikuwapo kwa miaka mingi sana. Ni barabara ambayo inawawezesha wananchi kufika baharini ambako wanafanya shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato.

Lakini pia wako wawekezaji ambao walitoa ajira kwa vijana wetu kwenye hoteli zao walishindwa kufika kwenye maeneo yao, tunashukuru kwa maamuzi haya ya serikali," alisema Mayala.

Mmoja wa wawekezaji anayemiliki hoteli maeneo hayo, ambaye biashara yake iliathirika kutokana na kufungwa barabara hiyo, Vidate Msoka, alisema maamuzi hayo yatawafanya kuendelea na biashara zao na kuchangia pato la taifa kwa kulipa kodi.

"Biashara zetu zilisimama kwa muda, hatukuwa tunapata wateja kwa sababu ya kukosekana barabara ya kutufikisha hotelini, maamuzi haya yametupa faraja kubwa, tunashukuru," alisema msoka.

Katika kikao cha jana kilichokuwa chini ya Makalla, mwekezaji ASM hakuhudhuria licha ya kupewa taarifa na badala yake alitumia mwakilishi.

## Walaani wenzao kutandikwa viboko

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi, umelaani kitendo cha mtu aliyetambulika kwa jina la Macho Salehe wa kata ya Kasisi, Urambo mkoani Tabora, kuwachapa viboko wanawake wakongwe kwa madai ya kujihusisha na ushirikina.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na mtandao huo, mwanamke mmoja ametoa taarifa kuwa yeye, pamoja na wanawake wengine watatu na binti zao wawili, mmoja akiwa mjamzito, wamechapwa viboko wakiwa wamemwagiwa maji na kupunguzwa nguo mwilini.

Taarifa hiyo ilisema kitendo hicho kimefanywa na Diwani wa Kasisi, kwa madai kuwa wanawake hao ni wachawi na washirikina ambao wamekuwa wakichukua vyakula vya watu kimiujiza wakati wa usiku.

"Wanawake hao walipatwa na kadhia hiyo wakiwa katika shughuli zao za kujipatia kipato na kutokana na tukio hilo walipoteza mazao na vitu mbalimbali. Tukio hilo pia liliwasababishia maumivu makali ya mwili na viungo, limewadhalilisha wao binafsi, familia zao na jamii nzima.

"Mpaka taarifa hizi zinatufikia, tayari familia za wanawake hao zilikuwa zimelazimika kuhama makazi na kwenda kuishi maeneo mengine kwa kuogopa vipigo zaidi, kubomolewa nyumba zao na vitisho dhidi ya maisha yao ambavyo walivipata kutoka kwa diwani huyo," ilisema taarifa hiyo.

"Mtandao unajiuliza, Je usalama wa hawa watu uko wapi? Mali zao walizoacha ziko salama? Huko waliko wamepewa ulinzi? Vitendo hivi vya kikatili ni mwendelezo wa ukiukwaji wa haki za binadamu huku wanawake wakiwa ndio wahanga (waathirika) wakubwa wa matukio hayo hapa nchini. Havipaswi kufumbiwa macho, havivumiliki na havikubaliki na tunavilaani kwa nguvu zote," ilisisitiza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema: Hivi karibuni katika kipindi cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, tulishuhudia binti mmoja aliyejulikana kama Florencia Mjenda ambaye alieleza kupitia vyombo vya habari kuhusu tukio la kupigwa na Mkuu wa Wilaya ya Songwe hadharani kwa madai ya kukalia jukwaa kimakosa.

"Vitendo hivi vinaonekana kushika hatamu na vikikaliwa kimya vitaendelea kushamiri na kuota mizizi. Ni jambo la kutafakarisha sana ikiwa viongozi ambao wamepewa dhamana na serikali na wananchi kuwaongoza kwa kufuata sheria na miongozo wao ndiyo wanakuwa wa kwanza kuvunja sheria."

Taarifa hiyo ilisisitiza kuwa ukatili wa kijinsia haukubaliki wakati wowote na mtu yeyote awe kiongozi au raia wa kawaida na kwamba uthubutu wa kuendelea kufanya vitendo hivyo hususan katika kipindi hiki cha kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, vinakasirisha na kukera na vinaonyesha upungufu wa maadili na uvunjwaji wa sheria.

Pia ilisema vitendo hivyo vinafifisha jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wa masuala ya haki za wanawake na binadamu kwa ujumla.

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA
## MATUMIZI YA NAMBA YA UTAMBULISHO (TIN) SAHIHI KWA WAAJIRIWA NA AINA YA AJIRA

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inapenda kuwakumbusha waajiri wote kuhusu uzingatiaji wa matumizi ya TIN sahihi kwa waajiriwa wote katika uwasilishaji wa ritani za Pay as You Earn (PAYE). Mamlaka imefanya maboresho katika mfumo wa uwasilishaji ritani ambapo kushindwa kutumia TIN sahihi kutakwamisha uwasilishaji wa ritani sahihi kwa waajiri katika mfumo huo na hivyo kupelekea usumbufu usio wa lazima ikiwemo riba na adhabu.

Ikumbukwe kuwa, Mamlaka imekuwa ikuwakumbusha waajiri wote kuhakikisha kuwa waajiriwa wao wana TIN na zinatumika kikamilifu sawa na matakwa ya **kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438.** Pamoja na ukweli kwamba waajiri wengi wameonesha mwitikio chanya bado kuna baadhi ya waajiri ambao wameshindwa kusimamia matakwa hayo ya kisheria kwa kuendelea kuwasilisha ritani za PAYE bila kutumia TIN sahihi za waajiriwa au kutumia **TIN 999 999 999**.

Kufuatia hilo, Mamlaka inapenda kuwakumbusha waajiri na waajiriwa wote kuhakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kisheria la kuhakikisha matumizi sahihi ya TIN katika uwasilishaji wa ritani ya **PAYE** kuanzia mwezi **Disemba, 2022**. Mfumo wa uwasilishaji ulioboreshwa ***(Upgraded e-filing)*** utashindwa kupokea majina ya waajiriwa wasio na TIN sahihi na hivyo kuathiri usahihi wa ritani husika. Sambamba na matumizi ya TIN sahihi, waajiriwa wanakumbushwa kuhakikisha wanaweka rekodi sahihi za ajira za waajiriwa wao kati ya ***ajira ya msingi (Primary Employment) au ajira ya ziada (Secondary Employment).***

Ikumbukwe kuwa TIN hutolewa bure na upatikanaji wake ni rahisi ambapo kwa waajiriwa wenye namba za usajili inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wanaweza kuomba TIN kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa **Online TIN Registration** kupitia tovuti ya TRA (www.tra.go.tz). Waajiriwa wasio na namba ya NIDA wanakumbushwa kutembelea Ofisi za TRA ili kupatiwa TIN.
Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

| | |
|---|---|
| **Tovuti** | : **www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | : **0800 750 075 au 0800 780 078** |
| **WhatsApp** | : **0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | : **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

17195002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga SC fanyeni kweli usajili dirisha dogo

**DIRISHA** dogo la usajili limefunguliwa, hii ni nafasi adhimu kwa Simba na Yanga ambazo zitaiwakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa, kuimarisha vikosi vyao.

Simba inaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya mabingwa Afrika, wakati Yanga ikiwakilisha kwenye Kombe la Shirikisho la Afrika ambayo yote huandaliwa na kusimamiwa na CAF.

Kwenye michuano hiyo, Simba na Yanga zote wapinzani wao wameshawajua baada ya wiki iliyopita CAF kuweka hadharani makundi katika mashindano hayo makubwa zaidi kwa kazi ya Klabu barani Afrika.

Timu ambazo zimepangwa kwenye makundi yao ni zile ambazo uwekezaji wao kwenye vikosi ni mkubwa na hata wachezaji wao ni wale wenye majina makubwa na vipaji vya uhakika.

Kwa upande wa Simba imepangwa kundi C pamoja na Raja Casablanca ya Morocco, Horoya ya Guinea na Vipers ya Uganda.

Huku kwa wao Yanga wamepangwa Kundi D pamoja na Monastir ya Tunisia, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Real Bamako ya Mali.

Ikumbukwe Yanga ilifuzu hatua hiyo baada ya kuitoa Club Africain ya Tunisia kwa kuichapa 1-0 pale Tunis kufuatia suluhu jijini Dar es Salaam.

Monastir ni vigogo wengine wa Tunisia ambao ndio ambao walitwatoa waliokuwa mabingwa watetezi wa michuano hiyo.

Simba na Yanga, zinapaswa kufanya kweli katika usajili huu ili kuimarisha vikosi vyao na viweze kuleta ushindani mkubwa kwenye michuano hiyo, hasa baada ya kuwajua wapinzani wao.

Desemba 15 dirisha dogo la usajili lilifunguliwa ambalo linatarajiwa kufungwa Januari 16, 2023 ni wastani wa mwezi mmoja ambao pasina shaka unatosha kwa timu hizo kufanyia marekebisho vikosi vyao. Ni suala la uongozi na klabu zao kukaa na kuangalia ni wachezaji wapi watafaa kuwasajili kwenye timu zao.

Msemaji wa Klabu ya Simba, Ahmedi Ali alisema kufunguliwa kwa dirisha la usajili kutafanya timu yao ipate nafasi ya kusajili wachezaji wengine watakaoongeza nguvu kwenye kikosi chao.

"Ni kweli dirisha la usajili limefunguliwa na tayari kocha Juma Mgunda, ameshapeleka mapendekezo ya wachezaji anaowataka ili kukiimarisha kikosi," alisema.

Aliongeza: "Zipo tetesi nyingi zinasemwa mara Manzoki, Mudathiri, Saido Ntibanzonkiza lakini niseme kwamba bodi ya timu pamoja na uongozi wake wao ndio wanajua mchezaji gani anayetakiwa."

Pia msemaji wa Yanga, Ali Kamwe alibainisha kuwa dirisha hili hawatofanya mzaha kwenye usajili.

"Dirisha hili linatupa nafasi ya kuongeza wachezaji wengine wapya, naamini kocha ana maono na atafanya uamuzi mzuri katika kupata wachezaji wa kuongeza nguvu ili kufika hatua ya mbali kwenye mashindano," alisema.


"Ndani ya muda huu wa usajili ambao ni wastani wa mwezi mmoja tutakuwa tayari tumefanikisha usajili na niwahakikishie mashabiki kwamba uongozi upo makini na unafanyia kazi mawazo ya wananchi."

Pamoja na tambo kutoka kwa wasemaji wa klabu hizo, lakini ukweli ni kwamba, wanapaswa kuzingatia na kuangalia kwa makini aina ya wachezaji ambao wanahitajika kwenye vikosi vyao.

Huu ni wakati mzuri zaidi wa kurebisha makosa kwenye vikosi vyao ambayo waliyaona kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ambao sasa umeingia kwenye ungwe ya pili.

Hivyo, Nipashe inawataka viongozi wa Simba na Yanga kutumia vizuri zaidi kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili kwa ajili ya kuimairsha vikosi vyao ili waweze kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Klabu, wachezaji TFF kuweni makini dirisha dogo la usajili

**INAWEZEKANA** kuwa dirisha hili dogo la usajili likawa na pilikapilika nyingi za usajili kuliko mengine yote yaliyowahi kupita huko nyuma.

Nasema hivyo kwa sababu inaonekana klabu nyingi za Ligi Kuu zina uhitaji kubwa wa wachezaji tofauti na madirisha mengine madogo ya usajili yaliyowahi kupita.

Kila ukimsikia kocha wa timu analalamika udhaifu kwenye baadhi ya maeneo ya kikosi chake. Ni klabu moja tu ambayo nimemsikia kocha wake akisema kuwa hahitaji kufanya usajili kwa sababu ana kikosi kipana. Huyo ni Kocha Mkuu wa Azam, Kalimangonga Ongala.

Lakini klabu zote zilizobaki zimeonekana kuwa na mapungufu na zikilalamika kuwa ikifika kipindi cha usajili wa dirisha dogo ni lazima waongeze nguvu kwenye vikosi vyao.

Kuanzia Simba, Yanga, Ihefu hadi Dodoma Jiji, nina maana timu 15 zilizobaki zinaonekana kuwa na uhitaji wa kuongeza nguvu vikosi vyao.

Na kilio nilichokisikia zaidi ni cha ushambuliaji. Hili limeonekana kuwa tatizo sugu kwa timu nyingi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mfano Simba ambayo ndiyo inayoongoza kuwa na safu kali ya ushambuliaji, ikifunga mabao 31, lakini bado inalia na nafasi hiyo ikitaka kusajili straika asilia, mmoja au wawili.

Yanga ambayo nayo ina straika wake hatari kabisa nchini, Fiston Mayele inaonekana nayo itasaka mshambuliaji kwa sababu haina mbadala wake kama akiumia au kupatwa na tatizo lolote litakalomuweka nje.

Hizo zingine ndiyo usiseme kabisa. Timu nyingi zina washambuliaji, lakini hazina wafungaji kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Ihefu, Juma Mwambusi, akiongeza kuwa watu wa aina hiyo adimu sana.

Mwinyi Zahera naye akasema kuwa anahitaji straika mwenye uwezo wa kufunga mabao manane hadi 10 kwa msimu na si mradi straika tu.

Hii inaonyesha kuwa dirisha hili dogo linaweza kuwa na vita kali kama lilivyo dirisha kubwa. Kunyang'anyana wachezaji na michezo mingine isiyo ya manufaa kwenye mchezo wa soka inaweza kufanyika kwa sababu inaonekana kuwa dirisha hi dogo na mahitaji ni makubwa.

Ndiyo maana Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kupitia Afisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo akatoa rai kwa klabu na wachezaji jinsi ya kulitumia dirisha hilo, pamoja na kutoa onyo.

"Dirisha la Usajili, Ligi ya Wanawake, Championship, Ligi Daraja la Kwanza, linachukua mwezi mmoja hadi Januari 15, timu zinafanya usajili, pamoja na uhamisho, yeyote anayeona kuna maboresho au kuimarisha kikosi chake, basi ni wakati wake huu.

Dirisha dogo ni wakati wa kuongeza nguvu au kuimarisha kikosi, siyo wa kusajili kikosi kizima, tumeshatoa semina ni jinsi gani usajili huu unatakiwa kufanyika mwanzoni mwa msimu mameneja waliitwa, naamini kwa kipindi hiki chote hakutakuwa na changamoto yoyote katika eneo hilo la kusajili," akasema Afisa Habari na Mawasiliano huyo na kuongeza.

"Tunatoa nafasi kwa klabu yoyote ikipata changamoto wakati wa kusajili au kuhamisha mchezaji, basi wawasiliane na TFF ili kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa kabla ya dirisha kufungwa. Dirisha ni mwezi mmoja, klabu zitumie muda vizuri, waache ule mtindo wao wa kusubiri hadi siku za mwisho ndiyo wanaanza kuhangaika kufanya usajili, muda unaruhusu na zile klabu ambazo zitasajili wachezaji ambao bado wana mikataba na wachezaji watakaosaini mara mbili, bahati nzuri kanuni zipo wazi na zitahusika kuwahukumu," alisema.

Natarajia klabu zitasajili wachezaji ambao wanawahitaji, lakini pia kwa kufuata taratibu ili kuepuka mambo ya kusajili wachezaji ambao wana mikataba na klabu zingine kama ilivyojitokea kwenye dirisha kubwa pale Singida Big Stars ilipomsajili kipa Metacha Mnata akiwa na mkataba na Polisi Tanzania na Prisons ikamsajili kipa Musa Mbisa aliyekuwa bado ana mkataba na Coastal Union.

Kilichotokea ni kwamba wachezaji hao waliruhusiwa kuchezea klabu zao mpya, lakini zikifungiwa kusajili dirisha hili dogo, ingawa tayari adhabu hizo zimeondolewa kwa kupewa adhabu zingine mbadala.

Wachezaji wao wanatakiwa kuwa makini, wasiingize klabu mkenge. Kama wana mikataba na klabu zao, waseme ili zile zinazowataka zifuate utaratibu na si kusema uongo.

Kwa upande wa TFF na Kamati yake ya Sheria na Hadhi za wachezaji inatakiwa itende haki kwa pande zote na si kuzionea klabu ndogo. Mchezaji wa klabu ndogo anaweza kuchukuliwa na klabu kubwa bila utaratibu lakini ukakuta iliyochukuliwa haitendewi haki kwa sababu ya maslahi wa klabu kubwa, huu ni uonevu.

Kama klabu zitatuliza kichwa na kuwa makini kwa kila kitu, nadhani linaweza kupita salama bila malalamiko yoyote na tunaombea iwe hivyo.

# Chataanda ataka wanawake kumuezi Bibi Titi Mohamed kwa kufanya kazi

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, amesema njia mojawapo ya kumuenzi mwasisi wa umoja huo, Bibi Titi Mohamed, ni wanawake kutosubiri kuwezeshwa bali wajiamini katika majukumu yao.

Amesema wanawake wakiondokana na mawazo ya kusubiri kuwezeshwa, wakijiamini na kuonyesha uwezo walionao, ni rahisi kufika mbali hata pasipokuwa na msukumo wowote mkubwa kutoka nje.

Chatanda alisema hayo juzi kwenye kongamano la kumuenzi Bibi Titi, Ikwiriri, Rufiji mkoani Pwani huku akisema baadhi ya wanawake wamefanikiwa kwa kuthubutu kuonyesha jitihada katika nyanja mbalimbali.

"Iko mifano mingi ya wanawake waliothubutu hata kwenye siasa. Hapa kipekee ni lazima tumrejee Rais wa kwanza mwanamke wa Tanzania tangu tupate Uhuru mwaka 1961, Dk. Samia Suluhu Hassan," alisema Chatanda.

Alisema Rais Samia ndiye wanaweza kumwita Bibi Titi wa leo kwa kuwa katika uongozi wake wa takribani miaka miwili, ameleta mageuzi ya kusimulia historia kwa historia katika kuongoza nchi.

"Serikali yake imejenga miundombinu ya huduma za afya, elimu ikiwamo chuo cha ufundi na shule ya wasichana ya mkoa wa Pwani iliyopewa jina la Bibi Titi Mohamed. Mambo yote hayo na mengine yanaonyesha kweli Rais Dk. Samia ni Bibi Titi wa sasa anaeyaishi maono ya waasisi na kuwa jasiri katika kuongoza nchi.

"UWT tunadhani ni wakati mwafaka sasa kwa wanawake kuacha kusubiri kuwezeshwa. Tujiamini na tujitume na kuonyesha uwezo tulio nao. Ni rahisi kufika mbali hata pasipokuwa na msukumo wowote kutoka nje," alisema.

Pia alisema kuwapo UWT na harakati za kupigania usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake tangu enzi za Bibi Titi, kumewezesha harakati nyingi za kupigania na kutetea haki za wanawake na wasichana.

Chatanda alisema harakati zimeongezeka na kufanya mamilioni ya wanawake na wasichana hadi kufikia sasa wanatambua haki zao vizuri na kuzitetea, na kwamba aasa jambo la mwanamke ni jambo la mwanamke mwingine.

"Lakini pia tunapopaza sauti kama taifa au kwa ngazi ya kimataifa kuhusu usawa wa kijinsia, wanawake hatupaswi kubweteka tukisubiri huruma ya mipango na mikakati kutoka serikalini au kwa wadau wa maendeleo," alisema.

Alisema kama ambavyo Bibi Titi alipigania usawa katika kujenga uzalendo Tanganyika mwaka 1955 hadi 1965, ndivyo nyakati hizi za awamu ya sita wanaona Rais Samia alivyotanguliza ajenda ya usawa ndani ya CCM.

"Juhudi hizi za kuwainua wanawake zinajidhihisha pale ambapo Wanawake wabunge wameongezeka hadi kufikia asilimia 37 mwaka 2022 kutoka asilimia 21.5 ya mwaka 2005, Wanawake wakuu wa mikoa wameongezeka kutoka asilimia 10 mwaka 2005 hadi asilimia 23 mwaka 2022," alisema.

Alisema katika kuleta usawa wa kijisia wanawake wakuu wa wilaya wameongezeka kutoka asilimia 19 hadi 25 mwaka 2022 na wanawake mawaziri wamefikia tisa katika kutoka wanne.

"Wito wangu kwa wanawake wote nchini, tufuate nyayo za mashujaa wetu Bibi Titi Mohamed na Dk. Samia kwani sisi wanawake ndio tumebeba hatima ya kizazi chetu katika kila sekta kwa kuzingatia tunaongoza kwa wingi zaidi ya asilimia 51 ya Watanzania wote kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya mwaka 2022," alisema.



Mwenyekiti wa Taifa Jukwaa la Wadau wa Matumizi ya Maji Mtambuka, Mhandisi Mbogo Futakamba, akifungua mkutano wa kwanza wa kikosi kazi cha maji, uliofanyika jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Anayedaiwa kujihusisha na ugaidi awekwa chini ya uangalizi polisi

**Na Grace Gurisha**

KIJANA David Mwelase, anayedaiwa kujihusisha na mambo ya ugaidi, amewekwa chini ya uangalizi wa polisi kwa kipindi cha miaka mitano, ikiwamo kuripoti kwenye ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Kanda ya Dar es Salaam.

Imedaiwa kuwa pamoja na uchunguzi kumbaini, polisi walishindwa kukusanya ushahidi wa kutosha kumfungulia mashtaka ndiyo maana Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda ya Dar es Salaam (ZCO) ikaamua kupeleka maombi maalum mahakamani.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, baada ya ofisi ya ZCO kuwasilisha maombi na kijana huyo kuwa chini ya uangalizi.

Akisoma maombi hayo yaliyoambatana na kiapo cha ZCO, Rogasian Wenga, Wakili wa Serikali, Yusuph Aboud aliomba Mwelase awekwe chini ya ulinzi kwa kipindi cha miaka mitano.

Pia ZCO aliiomba mahakama itoe amri ya kutotenda kosa lolote la jinai hasa linalohusiana na vitendo vya ugaidi pamoja na amri nyingine mahakama itakayoona inafaa.

Wakili Aboud aliendelea kusoma kiapo hicho kuwa Novemba 10, 2022 alipokea taarifa za kiintelejensia zinazohusu Mwelase kujihusisha na vitendo vya ugaidi.

Ilidaiwa kuwa baada ya kupokea taarifa hizo, alifungua jalada la kesi na kuanza uchunguzi ambao alibaini kuwa anajihusisha na vitendo vya ugaidi kwa kushirikiana na raia wa Msumbiji aliyemtaja kwa jina la Obety Batista. "Pamoja na uchunguzi kumbaini Mwelase anahisiwa kujihusisha na vitendo vya kigaidi polisi walishindwa kukusanya ushahidi wa kutosha kumfungulia mashitaka ndiyo maana wakaamua kuwasilisha maombi hayo mahakamani.

"Mwelase alikuwa makini na mwenye kuchukua tahadhari hivyo kuwafanya washindwe kupata ushahidi na waliamua kuwasilisha maombi haya kwa kuwa jambo hili ni zito na lenye kugusa usalama wa maisha ya watu, amani na utulivu wa nchi," alidai Aboud.

Baada ya Aboud kumaliza kusoma kiapo hicho, Hakimu Mrio alikubaliana na maombi hayo na kutoa masharti ya dhamana kwa Mwelase, ambapo alitakiwa kuwa na

wadhamini wawili wenye vitambulisho watakaosaini bondi ya Sh milioni tano kila mmoja.

Pia Hakimu Mrio alimtaka Mwelase kuzingatia na kuwa tayari kubadilika kwa sababu suala la msingi ni kubadilika na kuwa mtu mwema, hivyo akishindwa kufanya hivyo atawapa shida wadhamini wako.

Baada ya Hakimu Mrio kusema hayo, Mwelase aliahidi mbele ya mahakama kubadilika na kuwa mtu mwema. Alitimiza masharti hayo na kuachiwa huru.

# Mhagama aonya taasisi kukaidi kufanya mabaraza wafanyakazi

**Na James Mwanamyoto,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amezionya taasisi za umma zinazokaidi kufanya vikao vya mabaraza ya wafanyakazi.

Amesema vikao hivyo ni takwa la kisheria, hivyo kila taasisi ihakikishe inafanya vikao hivyo ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi.

Mhagama alitoa onyo hilo jana wakati akifungua Kikao cha Pili cha Baraza la Sita la Wafanyakazi la Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kilichofanyika mjini hapa.

Alisema ni lazima taasisi zote zihakikishe zinatekeleza takwa hilo la kisheria kwa kufanya mabaraza ya wafanyakazi ili kujadili changamoto zinazokwamisha utendaji kazi wa taasisi pamoja na kuweka mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma.

Vikao vya mabaraza ya wafanyakazi, alisema vikifanywa kwa wakati, vinaondoa uwezekano wa kufanyika kwa vikao vya watumishi visivyo rasmi, ambavyo mara nyingi vinatengeneza makundi na kuibomoa taasisi kwa kuwa havina tija katika kufikia malengo ya taasisi.

"Kwa ujumla, vikao vya mabaraza ya wafanyakazi vina tija kwenye ustawi wa nchi kwani vinawezesha kuongeza ari na morali ya utendaji kazi pamoja na kujenga uhusiano na ushirikiano mzuri wa kiutendaji baina ya menejienti na watumishi," alisisitiza.

Waziri alisisitiza kuwa ushirikishwaji wa wafanyakazi katika mabaraza ni lazima kwa kuwa sheria zinaeleza wazi umuhimu wa mabaraza hayo ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Alisema taasisi zote za umma zinapaswa kufanya vikao vya mabaraza ya wafanyakazi kwa wakati.

Alisema serikali inatarajia kuwa baada ya kikao hicho, kupitia maazimio watakayokuwa wamejiwekea kila mtumishi kwa nafasi yake atakuwa kwenye nafasi nzuri ya kutekeleza majukumu yake kikamilifu ili kufikia malengo ya taasisi.

Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi hiyo, Dk. Albina Chuwa, alisema kikao hicho kina mchango mkubwa katika kufikia malengo ya taasisi ya kutoa takwimu sahihi za kupanga mipango ya maendeleo katika taifa.

Dk. Chuwa alitaja baadhi ya mafanikio ambayo taasisi yake imeyapata ndani ya miezi sita katika kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 kuwa ni pamoja na kupata takwimu sahihi za mfumuko wa bei, pato la taifa la kila mwezi na kutoa takwimu za idadi ya watalii walioongezeka kupitia filamu ya The Royal Tour ambayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameitumia kutangaza vivutio vya utalii nchini.

# NMB yakabidhi vifaa vya kuboresha sekta ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekabidhi vifaa vya kusaidia maendeleo ya elimu wilayani Kibaha vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 37 kama sehemu ya kuchangia ustawi wa huduma za kijamii nchini.

Kiasi hicho ni sehemu ya asilimia moja ya faida baada ya kodi ambayo benki hiyo hutenga kila mwaka kusaidia kutatua kero zinazoikabili jamii na kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo.

Akizungumza kabla ya makabidhiano hayo jana, Meneja wa Tawi la NMB Kibaha, Festo Isango aliyemwakilisha Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam inayojumuisha pia Mkoa wa Pwani, alisema bajeti ya mwaka huu ya benki hiyo ya uwajibikaji kwa jamii ni zaidi ya Sh. bilioni mbili.

"Kwa miaka kadhaa sasa, NMB imekuwa ikisaidia miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi kwa kujikita zaidi kwenye miradi ya elimu (madawati na vifaa vya kuezeka), afya (vitanda, magodoro yake na vifaa vingine vya kusaidia matibabu) na kusaidia wakati wa majanga yanayoipata nchi yetu. "Na kwa miaka saba mfululizo tumekuwa tukitenga asilimia moja ya faida yetu kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii inayotuzunguka," Isango alisema.

Hafla ya kukabidhi vifaa hivyo kwa ajili ya shule nne za sekondari na mbili za msingi ilifanyika kwenye Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri aliyeipongeza benki hiyo kwa ushiriki wake wa dhati katika maendeleo taifa.

Kiongozi huyo alisema kuwa mbali na kuipa fedha wilaya hiyo, NMB pia mshirika mkubwa wa maendeleo ya jamii na kiuchumi wilayani mwake kupitia uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi na taasisi mbalimbali.

"Tunaipongeza NMB na viongozi wake kwa kuchangia juhudi za serikali kuboresha huduma za jamii na maisha ya watanzania kwa ujumla," Mkuu Wilaya huyo alisifu.

Kwa mujibu wa Isango, kiwango cha uwekezaji cha NMB kwenye miradi ya maendeleo ni kikubwa na kinaifanya benki hiyo kuwa kinara wa ustawi wa jamii miongoni mwa taasisi za fedha nchini.

"Vifaa hivi tunavyokabidhi leo (jana) ni moja ya ushiriki wetu kwenye maendeleo ya jamii na sisi kama benki inayoongoza Tanzania, tunao wajibu wa kuhakikisha jamii inayotuzunguka inafaidika kutokana na faida tunayoipata," kiongozi huyo alifafanua.

Pia alibainisha kuwa NMB imekuwa inashiriki kwa karibu kwenye masuala muhimu ya maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kama ambavyo imekuwa inafanya sehemu nyingine nchini.

Shule zilizopata msaada wa benki hiyo jana ni Shule za Msingi Sofu na Mwanabwito. Za Sekondari ni Mwanalugali, Pangani, Kibaha Girls na Mbawa Miswe.

Usaidizi zilizoupata ni wa samani za ofisi za walimu, meza na viti vya wanafunzi, vitanda, makabati na mabati.

"Pamoja na makubwa yanayofanywa na serikali, sisi kama wadau tunao wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za maendeleo kwa kusaidia jamii zetu kwani jamii hizi ndio zimeifanya Benki ya NMB kuwa hapa ilipo na kubwa kuliko benki yoyote nchini," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, Sara Msafiri, akiangalia viti 50 na meza vilivyotolewa katika hafla ya makabidhiano ya misaada mbalimbali kutoka NMB kwa shule sita vyenye thamani ya Sh. milioni 37 kwa Shule ya Sekondari Pangani wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa kwa shule za sekondari na msingi za wilayani Kibaha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni za bima India zatua nchini

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa kampuni mbili kubwa za bima India wako nchini kwa lengo la kutafuta fursa za uwekezaji zinazoweza kuifanya sekta hiyo kuwa ya ushindani zaidi.

Kumar Ramasubramanian, Mwenyekiti wa Shirika la Bima ya Maisha (LIC) na Devesh Srivastava, Mwenyekiti wa General Insurance Corporation (GIC) kutoka India, juzi walifanya mazungumzo na wadau wa sekta hiyo jijini Dar es Salaam kupitia mkutano ulioandaliwa na Ubalozi wa India nchini.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Mkurugenzi wa Usimamizi wa Soko la Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Abubakar Mgata alisema wanashirikiana na India kwa kuwa imepiga kubwa kwenye masuala ya bima.

"LIC na GIC ni kampuni za bima mtawanyo na kwenye utaratibu wa bima kuna kampuni ya kawaida, inaandikisha na bima mtawanyo, unachukua ada halafu ikitokea janga inalipwa kwa pamoja," alisema.

Mgata alitumia fursa hiyo kuzikaribisha kampuni hizo na nyingine kuja kuwekeza Tanzania kwa kuwa kwa sasa tasnia ya bima inakua na kuna ongezeko la ada mwaka hadi mwaka ambapo kwa mwaka jana waliandikisha karibu trilioni moja.

"Wachangamkie hizi bima watanzania wanazihitaji, mfano sekta ya kilimo, bima za mifugo huko hatujagusa kabisa, ni maeneo mapya tunawakaribisha kuwekeza," alisema.

Kiongozi huyo alisema huu ni mwisho wa mwaka na kampuni hizo zimekutana kujadiliana namna ya kufanya biashara kwa mwaka ujao wa 2023.

"Hii sehemu nzuri ya kubadilishana mawazo na kutengeneza biashara kutokana na uhusiano wetu, TIRA kazi yetu ni kuweka mazingira mazuri, kampuni kama hii anapofika kwetu inaona mamlaka tupo.

"Kama mlivyosikia GIC anafikiria kuweka ofisi Tanzania ambapo hapo tutakuza ajira na kuvutia uwekezaji," alisema.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan alisema mkutano huo ni fursa kwa wadau wa bima kutoka Tanzania kubadilishana uzoefu na kampuni hizo kongwe kutoka India.

Alisema lengo lake ni kubadilishana uzoefu katika sekta ya bima kwa kuwa kumekuwa na ushirikiano mkubwa kati ya nchi hizo mbili katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Balozi huyo alisema fursa hiyo ni muhimu kwa kampuni za Tanzania ili kutumia uzoefu wa LIC na GIC ambao haujafikiwa hasa katika bima ya maisha.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa LIC, Ramasubramanian alisema pamoja na mambo mengine, wapo Tanzania kutafuta fursa zinazohusiana na bima ili washirikiane na kampuni za wazawa kuwekeza kwenye eneo hilo.

Alisema lengo la LIC ni kusaidia kampuni za ndani kuongeza huduma hasa bima ya maisha kama ilivyo nchini India ambako huduma hiyo ni kubwa.

Alisema wanahitaji kuona bima inavyotumika kwenye maeneo mengine ya maendeleo kama vile sekta ya kilimo kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mwenyekiti wa GIC, Srivastava alisema mpango wa muda mrefu wa kampuni yao ni kuona namna watanzania wanafurahia huduma za bima kwa kufungua tawi lao nchini.

# Ataka mpango kazi kuzuia uharibifu vyanzo vya maji

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga ameagiza kila kikundi kazi cha utunzaji wa rasilimali za maji, kiandae mpango kazi wa utekelezaji kila mwaka wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali hiyo ili kukabiliana na uharibifu na mabadiliko ya tabianchi.

Jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Taifa Jukwaa la Wadau wa Rasilimali za Maji kutoka sekta mtambuka, Mbogo Futakamba, alitoa agizo hilo kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Sanga, wakati akifungua mkutano wa kwanza wa vikundi kazi vitatu vitakavyoshirikiana na jukwaa la utekelezaji wa majukumu ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Futakamba alisema lengo la kuunda jukwaa hilo ni kukutanisha wadau wa rasilimali za maji kujadili na kubadilishana uzoefu na ujuzi ili kuboresha utendaji kazi na kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za maji kwa maendeleo ya kizazi cha sasa na baadaye. "Jukwaa hili lina wadau zaidi ya 100 wanaotoka katika taasisi takriban 90 nchini na hata nje ya nchi, ambao ni wawakilishi kutoka sekta za serikali, sekta binafsi, mashirika ya umma, vyuo vya elimu, wadau wa maendeleo na taasisi zisizo za kiserikali.

"Nitumie fursa hii kuwapongeza wadau wote kwa mafanikio ambayo tayari mmeshayapata tangu kuanzishwa kwa jukwaa hili mwaka 2017.

"Niwashukuru pia wadau ambao wamekuwa wakishiri kila mwaka bila kukosa, michango yenu imesaidia sana kuimarisha utekelezaji wa jukwaa na mafanikio hayo yaliyopatikana," alisema Futakamba. Alisema Tanzania inategemea upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu unaotokana na nguvu ya maji.

"Kwa mfano, gharama za uzalishaji umeme wa nguvu za maji ni Sh. 13 kwa uniti, umeme wa gesi asilia Sh. 129 hadi 153 na kwa mafuta ya dizeli Sh. 546 hadi 675.

"Kwa kutambua hilo, serikali inatekeleza miradi mikubwa ikiwamo ujenzi wa Bwawa la Nyerere kwa ajili ya kuzalisha umeme wa maji kiasi cha megawati 2,115 ambapo mradi huu ukikamilika zaidi ya asilimia 70 ya umeme wote nchini utakuwa ni wa maji," alisema.

Aliongeza: "Sote tunatambua umuhimu wa maji kwa binadamu, wanyama, mimea na viumbe hai vyote kwa ujumla. Vilevile, ustawi wa jamii, maendeleo ya viwanda, uzalishaji wa nishati ya umeme, kilimo na mifugo hutegemea kuwapo maji ya kutosha. Ndio maana tunasema maji ni uhai na maji ni uchumi.

"Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2026; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2025); na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (2015-2030 nusu ya Malengo 17) vyote vinategemea uhakika wa maji kwa kuwa maji ni kiungo muhimu kwa sekta zote za kijamii, kiuchumi na mazingira," alisema.

# Fedha ujenzi madarasa kaa la moto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ONGEZEKO la fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa, Sh. milioni 226 zilizoingizwa nje ya bajeti katika Halmashauri ya Arusha, sasa limekuwa 'kaa la moto' kwa watendaji wa halmashauri hiyo.

Kutokana na ongezeko hilo, jana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alitoa siku saba za kuchunguzwa matumizi hayo na ripoti yake kuwasilishwa wizarani.

Kairuki aliagiza uchunguzi huo kufanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkaguzi wa Ndani na Mhandisi wa Halmashauri ya Arusha, wakati alipokwenda kukagua vyumba vya madarasa vya Shule ya Sekondari ya Kiutu.

Akiwa katika ukaguzi huo, waziri alibaini ongezeko la fedha hizo ambazo ni tofauti na mwongozo wa TAMISEMI wa matumizi yasiyozidi Sh. milioni 600.

"TAKUKURU, Mkaguzi wa Ndani (Winani Marwa) na Mhandisi wa Wilaya (Nuru Mkwazu), nileteeni ripoti ya uchunguzi ndani ya siku saba kuanzia leo (jana) ili nijue ongezeko hilo limetokana na nini kama ni gharama za ujenzi au laa!

"Lakini pia, kamati ya ujenzi kagueni hatua kwa hatua mradi wa ujenzi wa ghorofa wa shule hii ili kubaini kasoro zilizopo na kuzirekebisha, badala ya kusubiri viongozi wafike na kuzibaini," alisema.

"Na wewe mhandisi kuwa makini sana. Hapa nataka kujua kwa nini fedha hizi zimeongezeka badala ya Sh. milioni 600 kama mwongozo unavyosema. Mambo ya ajabu kabisa haya, matokeo yake fedha imezidi na kufikia Sh. milioni 826 hii imetokana na nini ili nijifunze kwa wengine nitakapoenda.

"Nataka kujifunza zaidi hili ongezeko la shilingi milioni 226 kama ni sahihi au la, kagua kwenye mbao, mchanga na vitu vingine na hii itanisaidia huko mbele ya safari."alisema

Baada ya Waziri Kairuki kuhoji, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha iliyoko Wilaya ya Arumeru, Suleiman Msumi, alisema ongezeko la fedha hizo, limetokana na matatizo mbalimbali.

"Kwa kuwa mradi bado haujamalizika, pia kama Halmashauri tutalazimika kuchukua shilingi milioni 130 ya Kituo Cha Afya cha Mateves ili kukamilisha shule hii,"alisema Msumi



Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Mirerani, Menard Msengi (kushoto), akiwasilikiza wadau wa madini ya tanzanite wa wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Mawakili wawatembelea watoto yatima, wagonjwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAWAKILI 50, ambao ni wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Kanda ya Arusha, wametembelea watoto yatima, wagonjwa na kupanda miti kando ya Mto Ngarenaro ili kuchagiza kampeni ya utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji.

Mwenyekiti wa Mawakili Kanda ya Arusha, George Njooka, alisema jana kuwa wameamua kutoa msaada huo kwa kuwa wanatambua kuwa wanajukumu la kuchangia shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kusaidia wagonjwa na yatima.

Aidha, Njooka, alisema kuwa wamepanda miti katika chanzo cha Mto Ngarenaro zaidi ya miti 100, kutembelea na kutoa zawadi kwa wagonjwa wasio na uwezo Hospitali ya Rufani ya Mount Meru, kutembelea yatima na kuwapatia mahitaji.

"Tumeona sisi ni mawakili tunapaswa kuahiriki shughuli za jamii kama moja ya kurudisha shukrani zetu kwa kutuamini kuwahudumia katikaukuwapa elimu na kuwasimamia kesi zao mbalimbali," alisema

Nembris Baltazari, Mkazi wa Arusha, alisema amefurahi kupata msaada wa kisheria hususani katika eneo la ardhi kwa kuwa awali alikuwa na uelewa mdogo ila TLS wamemfungua akili.

Baltazari aliwaomba mawakili hao kwenda maeneo ya vijijini ambapo watu wengi wanaonewa na hawajuwi haki zao.

Shughuli hiyo ilitanguliwa na utoaji wa msaada wa kisheria katika viwanja wa Kanisa la Mtakatifu James la Angalikana, Dayosisi ya Mount Kilimanjaro.

Katika kazi hiyo, zaidi wa watu 500 walihudumiwa kwa kupatiwa elimu na msaada wa kisheria, wakiongozwa na Wakili Baraka Sulus, ambaye ni Mwenyekiti wa Msaada wa Kisheria Mkoa wa Arusha.

# Madaktari bingwa waweka kambi uchunguzi maradhi yasiyoambukiza

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JOPO la madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Apollo, New Delhi nchini India, kwa kushirikiana na Hospitali ya Misheni ya St. Joseph ya Jijini Arusha, limeanza kambi maalum ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali yasioambukiza, yakiwamo saratani na figo.

Kambi hiyo imepanga kutoa matibabu kwa wakazi wa mkoa wa Arusha na nje ya mkoa huo ili kuwasaidia wananchi kuondokana na gharama za kufuata matibabu mbali.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Silvia Mamkwe, ni vizuri wananchi wakatumia fursa hizo za kuonana na madaktari bingwa wanaofika nchini katika hospitali mbalimbali ili kuokoa gharama za kuwafuata kwenye nchi zao.

"Lengo la serikali kuruhusu ujio wa madaktari hawa kwenye hospitali za serikali na binafsi ili kuokoa gharama kwa wananchi na serikali za kufuata matibabu mbali," alisema.

Alisema ni muhimu kwa kila mwananchi kufanya uchunguzi wa miili yao kwani kwa sasa magonjwa yasiyoambukiza yanashika kasi na kusumbua watu wengi.

"Kama hapa Arusha tuna asilimia 30 ya magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanasumbua watu mbalimbali na haya kwa asilimia kubwa husabishwa na mfumo wa maisha bwete tunayoishi wengi,"alisema


Pia alipongeza serikali kuboresha miundombinu ya afya na kusomesha madaktari mbalimbali na kusaidia Tanzania kuwa na wataalamu wa kutibu magonjwa yaliyokuwa yakiwapeleka watu nje ya nchi kwa ufanisi mkubwa.

Akizungumzia zaidi kambi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya St.Joseph, Dk.Thobias Mkina, alisema wanafunga mkono jitihada za serikali za uboreshaji huduma za afya kwa kuingia makubaliano na hospitali ya Apollo ili kuwasaidia wananchi wenye uhitaji wa kuonana nao.

"Naamini wanapofika nchini tunasaidia wananchi kuokoa gharama ambazo wanachangishana kwa ndugu ili kuweza kusafiri au serikali kusafirisha watu nje ya nchi na utaratibu huu utakuwa endelevu wa kuwaleta nchini kutoa huduma za matibabu kila baada ya miezi mitatu,"alisema.

Miongoni mwa madaktari bingwa waliokuja katika kambi hiyo ya siku mbili kutoka Hospitali ya Apollo ni Dk. Vijaya Rajakumari, ambaye ni bingwa wa upasuaji na upandikizaji figo. Mwingine ni Dk. Raguaya Mir, ambaye ni bingwa wa saratani ya matiti, damu, koo, kizazi na upasuaji.

Pia magonjwa mengine wanayopima na kutibu ni pamoja na tezi dume, utumbo, ngozi, ini na kiboko cha mkojo.





# DED maofisa watano wasimamishwa madai ya matumizi mabaya ya fedha

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe, mkoani Tanga, Nicodemus Bei na maofisa wake wengine watano, wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi kutokana na tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Bei na wenzake, walisimamishwa kazi jana na Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, ambaye aliamuru kuwekwa chini ya uangalizi wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna msaidizi mwandamizi (SACP) Henry Mwaibambe.

Mgumba alifikia uamuzi huo, baada ya kukagua na kubaini miradi mitano ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Magunga, zahanati tatu za Mgombezi, Old Korogwe na Kilole, Soko la Kilole na shule moja ya sekondari haijamalizika.


"RAS (Katibu Tawala wa Mkoa), chukueni hawa wote wanaohusika katika suala hili. Ukianza na DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri), Ofisa Manunuzi, Mhandisi wa Ujenzi, Ofisa Elimu Sekondari na huyu Ofisa Ardhi. Nendeni nao mkafanye uchunguzi pamoja na wote mnaohusika kila mmoja afanye yake.

"Halafu RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) na ninyi mchunguze jinai kwa hawa watu na wakati huo huo wasimame kazini ili wapishe uchunguzi mpaka tutakapojirdhisha kama hawana hatia, basi watarudi katika nafasi zao kuendelea na majukumu yao." alisema Mgumba.

Akiwa katika ukaguzi wa miradi hiyo, Mgumba, alisema amechukizwa na kitendo cha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe, kushindwa kusimamia miradi na kukamilika kwa wakati, huku baadhi yake ikitekelezwa kinyume na muongozo wa serikali.

"Sijaridhishwa kabisa na maendeleo haya ya ujenzi wa miradi ya maendeleo. Kati ya miradi niliyotembelea ni mradi mmoja tu wa soko, ndiyo uko vizuri. Hii haikubaliki na kila ninapokuja kutembelea miradi DED hayupo anaumwa, mara amefiwa na kila aina ya sababu anayo," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Aidha, Mgumba alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha mazao yote yanayovunwa shambani yanashushwa katika soko hilo ili kuvutia wafanyabiashara wengi kulitumia.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akisalimiana na baadhi ya wazee wanaolelewa katika makazi ya wazee yaliyoko Njoro mkoani Kilimanjaro, alipotembelea makazi hayo juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Serikali yaweka sharti uuzaji tangawizi

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI imeweka sharti la lazima kwa wakulima wa tangawizi wanaofanya shughuli za uzalishaji katika safu za milima ya Upare, wilayani Same mkoani Kilimanjaro, kuuza mazao yao kwa Kampuni ya Mamba Miamba Ginger Growers Ltd.

Licha ya kuwekwa kigezo hicho, pia imeagiza mwekezaji aliyeingia ubia wa uendeshaji wa kiwanda cha kusindika na kuchakata tangawizi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kupandisha bei ya zao hilo kwa kilogramu moja ili kuwatia moyo wakulima.

Amri ya kutouza zao hilo nje ya soko lililopendekezwa, ilitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, wakati alipokwenda kushuhudia ukarabati wa kiwanda kipya cha kisasa cha kuchakata tangawizi.

"Mimi nimekuja hapa kumwakilisha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alipaswa kuja kuzindua shughuli hii muhimu ambayo inalenga kukuza kipato cha mkulima wa tangawizi. Ni wajibu wa kila mkulima kuhakikisha analeta tangawizi hapa," alisema.

Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa ubia kati ya PSSSF na Ushirika wa Wakulima wa Tangawizi wa Mamba Miamba Ginger Growers Limited. PSSSF inamiliki asilimia 67 ya hisa na wanaushirika wanamiliki asilimia 33.

"Hatutapenda kuona wakulima wanasumbuka na bei, wala malighafi zinapelekwa nje ya nchi, kinyume na taratibu kanuni na sheria tulizojiwekea. Ni lazima mkumbuke uwekezaji huu utatuongezea ajira, kwa vijana wetu na kukuza uchumi wa taifa letu." Alisema.

Kabla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema uwekezaji uliofanywa na mfuko huo, umefanyika kwa kufuata miongozo ya Benki Kuu pamoja na Sera ya Uwekezaji ya Mfuko.

"Lengo kuu likiwa ni kuwa na uendelevu wa kifedha ili kulinda thamani ya fedha za wanachama na lengo lingine ni kupata faida ya uwekezaji ili kukuza hazina na kuongeza uwezo wa kulipa mafao pale yanapohitajika na pia kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi," alisema.

Kashimba, alisema kiwanda hicho kilichojengwa mwaka 2012, kina uwezo wa kusindika tangawizi tani 9.8 kwa siku, jambo ambalo halikuwezekana awali, kwa kuwa kiwanda kilikuwa kikizalisha chini ya tani moja kwa siku.

# DC aagiza mabanda umiza yote kufungiwa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Juma Irando, ameagiza Jeshi la Polisi kuvifunga 'vibanda umiza' vyote vinavyotuhumiwa kuonyesha picha za utupu za video, kwa kuwa kinachofanywa hivi sasa huko mitaani ni kinyume cha maadili ya Mtanzania.

Irando ameeleza kuwa hafurahishi na mabanda hayo kukiuka maadili kwa sababu waathirika wakubwa ni watoto, hasa katika masuala ya ukatili wa kingono.

Alitoa agizo hilo jana, alipokuwa akizungumza na wajumbe wa kamati ya afya ya msingi ya wilaya hiyo.

"Kwanza OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) nataka uchunguzi ufanyike haraka ili kubaini vibanda hivyo na kuvifungia kwa sababu sisi serikali tunapaswa kuhakikisha ulinzi na usalama wa mtoto una kuwepo kwa muda wote.

"Piteni chunguzeni na kufuatilia na kuona nini hasa kinafanyika huko na vile ambavyo tunaona vinakwenda kinyume na maadili yetu tuvifungie. Kwanza siku hizi kila mtu ana televisheni yake nyumbani, teknolojia imebadilika siku hizi, hebu tuone kama vinatusaidia, kama havitusaidii tuvifungie.

"Tunaweza kubadilika kutoka kwenye mambo ya vibanda umiza na watu wawe na televisheni zao nyumbani ili ulinzi wa watoto uwepo na si kuwapeleka kwenye mabanda haya na huko wanaonyeshwa picha za ngono," alisema.

Kutokana na kuporomoka kwa maadili, mkuu huyo wa wilaya, aliwasihi wazazi na walezi, kuacha tabia ya kuwa wakarimu kwa kupokea wageni na kuwalaza chumba kimoja na watoto, kwa vile baadhi ya wageni huwageuka watoto na kuwafanyia ukatili wa kingono na kuwatishia wasitoe taarifa kwa mtu yoyote.

Juni, 2019, serikali ilipeleka Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (Sura ya 230) na kutungwa upya ili kuhakikisha kwamba kumbi na vibanda vinavyotumika kuonyesha video, vinapaswa kurasimishwa chini ya kifungu cha 10 cha sheria hiyo.



## Jafo ataka utekelezaji biashara hewa ya ukaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeiagiza idara ya mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, kituo cha ufuatiliaji wa Kaboni na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kanda zote kushirikiana na wizara za kisekta kusimamia utekelezaji wa kanuni na mwongozo wa usimamizi wa biashara za hewa ukaa (kaboni).

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, aliagiza jana jijini hapa, alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu uzingatiaji wa kanuni na mwongozo wa biashara ya kaboni.

Pia Jafo alizielekeza sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wadau wa maendeleo kusimaia kwa ufanisi utekelezaji wa kanuni hizo na mwongozo ili kuleta tija kwa taifa.

Alisema biashara ya kaboni ni moja ya nyenzo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi duniani.

"Biashara hii hufanyika miongoni mwa nchi wanachama wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi, itifaki ya Kyoto na makubalianao ya Paris. Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa mikataba hii.

"Pamoja na sera na mikakati iliyopo na kwa kuzingatia umuhimu wa biashara hii, serikali imeandaa kanuni na mwongozo wa taifa wa usimamizi wa biashara ya kaboni nchini," alisema Jafo.

Aidha, alisema malengo makuu ya kanuni na mwongozo huo ni kuweka utaratibu na masharti ambayo wadau na wajasiriamali wa biashara ya Kaboni watapaswa kuzingatia wakati wa utekelezaji wa miradi mipya na miradi inayoendelea katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

"Kanuni na mwongozo vinalenga pia kuweka mazingira rafiki ya usimamizi wa mazingira na biashara nchini kanuni na mwongozo tayari zimekwishasainiwa na kutangazwa katika gazeti la serikali Na 636 na 637 la Oktoba 28, 2002 hivyo kuwa tayari kwa matumizi," alisema.

Kadhalika alisema kanuni na mwongozo wa usimamizi wa biashara ya Kaboni zimejikita katika kuimarisha mchango wa nchi katika jitihada za kupunguza uzalishaji wa gesijoto hivyo kupunguza athari za mazingira.

"Aidha kanuni hizo zinalenga kuhakikisha kuwa jamii, wadau mbalimbali wanahusika na biashara hiyo ikiwa pamoja na serikali kunufaika kikamilifu kutokana na faida zilizopo katika biashara ya kaboni nchini," alisisitiza Jafo.

Alitoa rai kwa wawekezaji, wananchi na watu wote wanaohusika na utekelezaji wa miradi hiyo, waanze mara moja kuhuisha miradi yao na kujisajili upya kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Kituo cha Ufuatiliaji wa Kaboni kilichoko Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro.

# Mkenda aapa kusimamia maadili walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameapa kusimamia maadili ya walimu huku akisema serikali itachukua hatua kali dhidi ya mwalimu atakayejihusisha na wizi wa mitihani na uhusiano wa kimapenzi na mwanafunzi.

Aidha, amesema viongozi wa dini watumike mara kwa mara kwenye shule ili kuongea na wanafunzi ili kuwaambia madhara ya kujiingiza kwenye mambo yasiyofaa ikiwamo ngono na dawa za kulevya.

Akifungua juzi jijini hapa mkutano wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA), Prof. Mkenda alisema suala la malezi kwa wanafunzi kwa sasa ni muhimu kushinda wakati mwingine wawe macho na wanaofanya matendo yasiyofaa.

"Suala la malezi kwenye shuleni lizingatie mwongozo wa malezi, unasihi na ulinzi, kuna wanafunzi wapo bweni hata wanaokaa nyumbani wazazi wanaenda kazini watoto wanakuja shule, saa nyingi watoto wanakuwa na walimu, tunaomba mpitie mwongozo kama kuna maeneo tuimarishe.

"Akitokea mwalimu mmoja anafukuzia binti zetu, watu wanaanza kuona walimu wote ni wabaya, akifahamika tu achukuliwe hatua haraka kwanza kabisa afukuzwe kazi, kuangalia jinai na kumshtaki hii ni kazi ya walimu wakuu," alisema.

Alipiga marukufu katika shule za bweni wanafunzi wawili kulala kitanda kimoja.

"Kama vitanda havitoshi mabweni hayatoshi tumwambie Mkurugenzi na mimi nitafuatilia, kama kuna Mkurugenzi atatumia fedha maeneo mengine na kuacha watoto wa wazazi wenzake kitanda kimoja watoto wawili, huyo Mkurugenzi hafai kuwa ofisi," alisema.

Kuhusu suala la vyoo, alisema kuna shule aliwahi kwenda alimwambia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoas na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), shule hiyo itafungwa kwa hali iliyopo.

"Mwalimu ukiona mazingira ambayo hayasaidii malezi na maadili ya watoto usiogope semeni, sema hii shule nitafunga kwa hali ilivyo nahitaji vitanda," alisema.

Kuhusu mitihani, Prof.Mkenda alisema kuna baadhi ya walimu wanachezea mitihani na tatizo hilo linatokea shuleni.

"Mwalimu hawezi kufungua mtihani mwenyewe wanaohusika ni wengi, kufungua mtihani ili kusaidia shule kufanya vizuri, mnakumbuka yule mtoto aliyebadilishiwa namba, yaani mwalimu unafundisha mtoto uongo na unatarajia awe kiongozi mwaminifu," alisema.

Alisema hali hiyo inahatarisha elimu inayotolewa kuwa na kada zisizo na ujuzi husika na kuwataka wakuu wa shule kudhibiti hilo.

"Unafundisha mtoto kuhusu rushwa mapema sana kwa kuwaibia mtihani lakini mnawanyima fursa watoto ambao wametumia akili zao, walimu wengi wanatuambia kuhusu hili, na kila atayefanya udanganyifu kwenye mtihani tutamkamata tumefungua macho yetu kweli," alisema.

Alitaka Baraza la Mitihani nchini (NECTA) kusimamia suala hilo na kwamba kwa anayetaka kuliingilia hakupenyeji na atakayejaribu atakamatwa na kufungwa.

Awali, Mwenyekiti wa TAHOSSA, Frank Mahenge, aliomba ujenzi wa vyumba vya madarasa uende sambamba na ujenzi wa nyumba za walimu




Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu ,Dk John Jingu akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha Makatibu wakuu cha mafunzo ya usawa wa kijinsia yaliyofanyika jijini Dodoma jana kwa kuandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia ,Wanawake na Makundi Maalumu.**PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Jamii yahimizwa kupaza sauti vitendo vya ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dk. John Jingu, ameitaka jamii, wadau na kila mmoja kwa nafasi yake kupaza sauti dhidi ya vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikiendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Dk. Jingu ameyasema hayo Jijini Dodoma kwa niaba ya Katibu Mkuu Kiongozi wakati akifungua kikao cha makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu kuhusu mafunzo ya Usawa wa Kijinsia na Tathimini ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Alisema licha ya mafanikio yaliyopo kutokana na juhudi zinazofanywa kukabiliana na vitendo hivyo, bado ukatili umeendelea, hivyo kuna haja ya kuwa na afua mbalimbali za kuwatetea manusura wa vitendo hivyo.

"MTAKUWWA lengo lake ni kutokomeza ukatili wa aina zote unaofanywa katika jamii sasa. Ukatili bado upo, hivyo tumekubaliana kila mmoja wetu awe kinara wa mabadiliko chanya kuhakikisha tunakuwa na malezi bora na afua za kuyalinda makundi yote," alisema.

Pia alitoa wito wito kila kundi kwa nafasi yake, wizara za kisekta, taasisi za serikali, mashirika ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali, viongozi wa dini, wazee wa kimila na vyombo vya habari kuongeza juhudi za kuimarisha usawa wa jinsia na kutokomeza ukatili .

"Nitoe rai tuendelee kushirikiana ili kutokomeza vitendo vya ukatili katika jamii na kufikia malengo na mikakati tuliyojiwekea. Nishukuru wadau wote kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali na kuhakikisha makundi yote yanalindwa dhidi ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Dk. Jingu alibainisha kuwa miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na kuwepo kwa Mpango maalumu wa malezi ya vijana balehe ili waweze kukua katika maadili, kujitambua na kufahamu nafasi yao kwa jamii.

Pia alisema uzingatiaji wa bajeti kwa mtazamo wa kijinsia katika sera, mipango na bajeti za wizara na sekta utasaidia kuleta maendeleo endelevu katika nyanja zote za kijamii.

"Uandaaji wa bajeti na mipango kwa mtizamo wa kijinsia una manufaa makubwa sana katika jamii yetu kama kushughulikia upungufu wa kijinsia hususan ule unaotokana na uwapo wa mahitaji tofauti baina ya wanawake na wanaume katika jamii au sehemu zetu za kazi," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, aliwataka maofisa maendeleo kupitia ngazi za vijiji, kata hadi wilaya kutimiza wajibu wao kuhakikisha maendeleo yanapatikana, wananchi wanakuza uchumi wao na kushiriki katika maendeleo kwa kulipa kodi.

"Kupitia mafunzo haya tumeongea mambo mengi yakiwamo mpango wa kitaifa wa malezi kwa makundi ya vijana balehe ambao una malengo mengi kama kuzuia Ukimwi, mimba za utotoni, ajira na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kumwandaa mtoto kuwa kiongozi bora kuanzia ndani ya familia," alisema.





# Waziri ataja faida UN kufungua ofisi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma amesema serikali imefurahishwa na uamuzi wa Umoja wa Mataifa kufungua ofisi za Shirika la Mpango wa Chakula (WFP) Zanzibar, ikiamini hatua hiyo itasaidia kufuatilia kwa karibu matukio na mwenendo wa majukumu yake.

Aliyasema hayo jana visiwani hupa wakati wa hafla ya kufungua ofisi ya WFP Zanzibar na kukabidhi ndege mbili zisizokuwa na rubani kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali.

Alisema serikali imejipanga kutekeleza malengo endelevu ya dunia ambayo yanakwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya 2050 ambayo imejikita katika kuona ustawi bora wa wananchi na ukuaji wa uchumi.

Waziri huyo alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuongeza kasi ya uzalishaji wa chakula kupitia mpango wa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ambao tayari mashamba ya mpunga yenye ukubwa wa ekari 4,570 yamejengwa miundombinu yake ya usambazaji maji shambani.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumejipanga kuona Zanzibar inajitosheleza kwa chakula, tumejikita kwenye kilimo cha umwagiliaji ili wakulima wazalishe chakula kingi," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa WFP nchini, Sarah Gibson alisema wamejipanga kusaidia mbinu mpya za kuongeza uzalishaji wa chakula kwa wakulima na kupambana na majanga ambayo yamekuwa yakisababisha maafa makubwa kwa wananchi.

Alisema wanaunga mkono vipaumbele vya Serikali ya Zanzibar ambavyo vyote vimejikita katika kuwainua wananchi kiuchumi na maendeleo kwa kupata huduma muhimu za kijamii.

Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Zlatan Milistic alisema wataendelea kuisaidia Zanzibar kuyafikia malengo endelevu ya dunia ikiwamo kujitosheleza kwa chakula na kuondokana na tatizo la lishe duni kwa watoto pamoja na kujikinga na majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mipango ya uhakika wa kupata chakula na kuimarisha lishe pamoja na kuwajengea uwezo wakulima kwenye kilimo cha umwagiliaji, ni sehemu ya mikakati ya UN kupitia WFP iliyoamua kufungua ofisi zake Zanzibar.

Alisema kufunguliwa kwa ofisi hiyo kwa kiasi kikubwa kutasaidia kuyafikia malengo hayo kwa kufuatilia kwa karibu ikiwamo kuwafikia walengwa - wakulima kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kujitosheleza kwa chakula.

"Umoja wa Mataifa kupitia WFP umekuja kufungua ofisi yake Zanzibar kwa ajili ya kufuatilia zaidi malengo na mikakati ya kujitosheleza na chakula pamoja na kufuatilia majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema.

Ofisi 11 za UN zimefunguwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya mikakati ya umoja huo kutekeleza malengo endelevu ya dunia ya kuleta ustawi bora wa wananchi na kukuza uchumi.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa (kulia), akikata utepe kuzindua mpango wa ufadhili wa masomo ya kuendeleza ujuzi kwa vijana kutoka kaya maskini na wanaoishi katika mazingira magumu uliofanyika katika Chuo cha Karume Zanzibar, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Vijana wa mazingira magumu kunufaika na mafunzo ya ujuzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa amezindua mpango wa ufadhili wa mafunzo ya kuendeleza ujuzi kwa vijana kutoka makundi maalum na wanaoishi kwenye mazingira magumu (Bursary Scheme for Vulnerable Groups).

Alizindua mpango huo jana wakati wa hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST).

Mpango huu wa ufadhili unasimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) chini ya programu ya kukuza ujuzi na stadi za kazi kwa ajili ya ajira zenye tija unaoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

SDF inafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia (WB), vijana 600 kutoka Zanzibar wakitarajiwa kunufaika nao.

Waziri Lela alisema lengo la ufadhili wa mafunzo ya ujuzi unaotolewa ni kuwezesha vijana wa kitanzania wanaotoka katika makundi maalum na kaya maskini kupata ujuzi na stadi za kazi zitakazowawezesha kuajiriwa na kujiajiri, hivyo kuchangia jitihada za serikali za kuwawezesha wananchi wake wa makundi yote kiuchumi na kijamii.

Alisema anaona fahari kushiriki katika hafla ya uzinduzi wa mpango huo wa mafunzo ya ujuzi kwa ajili ya vijana 600 ambao watapata fursa ya kupatiwa mafunzo ya ujuzi katika fani za ushonaji, umeme wa majumbani, udereva, useremala, ufundi bomba, ujenzi, ufundi magari, uchomeleaji, ususi na urembo, upishi, kompyuta, utengenezaji majokofu na kilimo cha bustani.

Waziri huyo alisema mafunzo hayo yanakwenda pamoja na programu ndogo ya Mafunzo ya Amali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama ilivyoanishwa kwenye bajeti ya wizara hiyo ya mwaka 2022/23 ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umaskini.

TEA imepewa jukumu la kusimamia na kutekeleza mpango huo na Wizara mama ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuwafikia vijana kutoka makundi maalum na wanaoishi kwenye mazingira magumu pamoja na walio kwenye kaya zilizosajiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuhakikisha wanafaidika na mpango huo kwa kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Prof. Maurice Mbago alisema taasisi hiyo ilipewa jukumu la kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa SDF mwaka 2017 na awamu ya kwanza ya utekelezaji ilifanyika mwaka wa fedha wa 2017/18 huku awamu ya pili ambayo inaendelea, ilizinduliwa rasmi mwaka 2020.

Prof. Mbago amlisema TEA kwa kushirikiana na WB imekamilisha taarifa ya ufuatiliaji wa wanufaika kwa lengo la kupima matokeo ya mafunzo ya kuendeleza ujuzi kwa wanufaika waliopata nafasi kushiriki mafunzo hayo. Ufuatiliaji huo uliohusisha wanufaika 3,871 kati ya wanufaika zaidi ya 35,000, umeonyesha asilimia 81 ya wanufaika hao wameajiriwa au wamejiajiri ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu walipopata mafunzo hayo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania, Bahati Geuzye alisema mpango huo unatoa ufadhili wa mafunzo ya ujuzi kwenye sekta sita za kipaumbele ambazo ni kilimo, biashara, utalii na huduma za ukarimu, uchukuzi, ujenzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Nishati.

# CCM, ACT watambiana uchaguzi wa ubunge leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VYAMA vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mdogo wa ubunge wa Amani, vimekamilisha kampeni na leo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itaendesha uchaguzi huo kufuatia kufariki dunia kwa aliyekuwa mbunge wake.

Akifunga kampeni za Chama Cha Mapinduzi (CCM) juzi, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Taifa, Hemed Suleiman Abdulla aliwaomba wananchi wa jimbo hilo kumchagua mgombea wao, Abdul Yussuf Maalim ili aendeleze utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Alisema Kamati Kuu imemkabidhi Ilani ya CCM, Abdul Yussuf Maalim ambayo ni mkataba wa chama na wananchi, hivyo chama kimemteua kusimamia ilani hiyo katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Hemed ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, aliwahakikishia wananchi wa jimbo hilo kuwa atasimamia ilani kwa kuwaletea maendeleo wananchi wote bila ya kujali itikadi zao.

Aliwataka wananchi kumuunga mkono kwa kumpigia kura mgombea huyo ili kuipa CCM ushindi wa kishindo kama katiba ya CCM inavyoeleza.

Alisema chama kimetengeneza miundominu mikubwa ikiwamo hospitali, shule na barabara ambayo inatarajiwa kufunguliwa kwenye shamrashamra za Sherehe za Mapinduzi.


Akiomba kura, Maalim aliwaomba wananchi wampe ridhaa ya kuwatumikia akiwa kwenye nafasi hiyo.

Akifunga kampeni hizo kwa upande wa Chama cha ACT Wazalendo, Mwenyekiti wake, Juma Haji Duni alisema wamejipanga kuhakikisha Uchaguzi Mkuu ujao wanaibuka na majimbo mengi zaidi wakianza na Jimbo la Amani.

Aliitaka NEC kusimamia vizuri majukumu yake ikiwamo kuwapo uchaguzi huru na haki kwa kuwahusisha wapigakura wa Jimbo la Amani na siyo mamluki.

"Matarajio makubwa yetu kwa NEC ni kuona uchaguzi wa Jimbo la Amani unakuwa huru na haki na kuepusha mivutano ya kuwaingiza watu ambao sio wapigakura halali wa jimbo hili," alisema.

Akiomba kura kwa wapigakura, mgombea wa ACT Wazalendo, Mohamed Khamis Mohamed aliwaomba wapiga kura kumpa ridhaa ya kuongoza jimbo hilo na kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili, ukiwamo uhaba wa maji safi na salama.



**SARAPHINA**

UKURASA 16



Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# LADY JAY DEE

UKURASA WA 16

YUKO WAPI ?

# FREDDIE NDALA KASHEBA-5

# Mchawi wa gita ‘kombora’, akalivunja na kuzikwa nalo

**Na Adam Fungamwango**

TUNAENDELEA na simulizi yetu kuhusu safari ya mwanamuziki nguli nchini Tanzania Freddie Ndala Kasheba aliyezaliwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mwaka 1946 na kufariki nchini Tanzania Oktoba 22, 2004.

Kiongozi huyo, mtunzi na mpangaji wa muziki, anakumbukwa sana na mashabiki wa muziki nchini kwa staili yake aliyokuja nayo ya kupiga gitaa la nyuzi 12 ambalo lilibatizwa majina mengi kama dazani au kombora. Aina yake ya upigaji pia ilivutia watu wengi.



**Avunja gitaa lake, akapata ushindi**

Katikati ya miaka ya 1980 kulitayarishwa shindano kati ya bendi aliyokuwa akiiogoza ya Orchestra Safari Sound ‘Dukudulu’ na mahasimu wao wakubwa Maquis Original chini ya Nguza Mbangu Viking.

Pambano hilo lilifanyika kwenye ukumbi wa DDC Magomeni Kondoa, ambapo umati mkubwa ulikuwa umefurika. Wakati huo bendi zote zilikuwa kamili, zenye mashabiki wengi na zilikuwa na nyimbo nyingi nzuri. Pambano lilielekea kama kuwa sare. Ukweli ni kwamba halikuwa na mahakimu, ila mashabiki wenyewe ndiyo walikuwa kama waamuzi.

Lilikuwa pambano la kibiashara zaidi kufuatia uhasimu wa bendi hizo mbili wakati huo.

Kasheba alifanya tukio ambalo limekuwa gumzo miaka na miaka na kutosahaulika kwa mashabiki wa muziki hadi leo hii. Wakati akipiga moja ya nyimbo zake zilizokuwa zikipendwa na mashabiki.

Alilipiga kwa ustadi mkubwa mpaka mashabiki wakalipuka kwa mayowe. Ni nafasi ambayo alikuwa akiihitaji. Aliliinua gitaa hilo juu na kulipigiza kwenye moja ya nguzo iliyokuwa kwenye ukumbi huo, likavunjika. Lilivunjika eneo la tumbo la gitaa yaani kule nyuma na kwenye mpini. Tumbo lilibaki peke yake na mpini ukawa kwake.

Tukio lile mbali na kushangaza watu, lilishangiliwa mno ikionekana kama Kasheba alipandwa na muktari wa gitaa kufanya kitendo hicho.

Wakati huo wapiga magitaa mengine kama second solo, rhythm na bass waliendelea kupiga kama kawaida wakati mashabiki walipiga mayowe na kushangazwa na kitendo kile. Dakika mbili baadaye lilitokea gitaa lingine dazani jipya kabisa kwenye sanduku, likaunganishwa na umeme akaendelea kupiga kama kawaida, na kuzidi kuamsha furaha na sauti za shangwe kutoka kwa mashabiki.

Pambano liliisha, lakini hakuna shabiki yeyote aliyetoka humo aliyezungumzia tena muziki, au nani kashinda, zaidi ya tukio alilofanya mwanamuziki huyo.

Lilitangazwa kwenye vyombo vya habari, redio na magazeti, picha zikasambaa, pamoja na kuwa ni stori kubwa kwenye vijiwe mbalimbali vya muziki.

Lile tukio ndilo linadaiwa kusababisha dukuduku ionekane kuwa ameshindwa pambano hilo. Na ndiyo tukio bora zaidi la kukumbukwa kwenye muziki wa dansi Tanzania.

Baadaye iligundulika kuwa mpango ule ulitengenezwa kwa makusudi. Kasheba alikuwa amepata gitaa lingine jipya la nyuzi 12, na lile alilopiga tayari lilikuwa kuukuu, hivyo alitengeneza mazingira yale kuwa atalivunja siku ya pambano kati yao na Maquis Original ili kutengeneza kiki kama wanavyosema mashabiki wa muziki wa kizazi hiki.

**Kifo chake**

Kabla hajafariki alitunga wimbo uitwao ‘Yellow Card’ uliokuwa unawasuta wale wote ambao walimvumishia amefariki. Hii ni kwa mara ya pili ukiachilia mbali alipolazwa Aga Khan mwaka 1984.

Ilikuwa ni katikati ya miaka ya 1990, ambapo ilivumishwa yupo hoi, mara amefariki, lakini akaibuka kama kawaida yake akiwajibu walimwengu kwa nyimbo.

Hii akawaambia kuwa walikukata kwenye stoo za vikontena ajenda ni maisha ya watu. Wakikutana kwenye miarobaini kwenye supu ya utumbo mazungumzo yao yote utumbo.

Kwenye wimbo huo, Kasheba akawaambia wale wote wanaomvumishia kifo kuwa wasiwe na wasiwasi kwani hata kama akifa hatomaliza ardhi wala vifo, atakwenda kwenye kaburi lake mwenyewe na wao wasihofu lipo kaburi lao kila mmoja linamsubiri.

Lenye mwanzo lina mwisho. Hatimaye Ndala Kasheba alifariki dunia Oktoba 22, 2004 jijini Dar es Salaam baada ya kuugua kwa miezi kadhaa.

Mamia ya mashabiki walikusanyika nyumbani kwake maeneo ya Kinondoni Dar es Salaam. Pamoja na shughuli zingine za kumuombea zikiendelea, lakini pia bendi yake ya Capital ilipiga muziki laivu nyumbani kwake kama ilivyo kwa taratibu na utamaduni wa Wakongomani.

Na wakati wa kuaga mwili wa marehemu, bendi hiyo maarufu kama Wazee Sugu walipiga wimbo uitwayo ‘Takadiri.’

Nakumbuka wakati mashabiki wa muziki wa dansi, wanamuziki, ndugu jamaa na marafiki wakiaga mwili wa Kasheba, wanamuziki wake wakiongozwa na King Kiki walikuwa wakipiga wimbo huo laivu, kiasi cha kuendelea kuzua simanzi kubwa.

Ndani ya sanduku la marehemu mlikuwa na gitaa. Mwamba alizikwa na gitaa lake. Na kwa mujibu wa wanamuziki wenzake walisema gitaa lile ni ule mpini wa gitaa la nyuzi dazeni alilolivunja kwenye mchuano kati ya bendi yake dhidi ya Maquis du Zaire miaka mingi iliyopita ukumbi wa Magomeni Kondoa.

**Itaendelea Jumamosi**

## UDAKU TU

# NI SALLAM SK...



INAWEZEKANA Sallam Sk, akatajwa kuwa meneja mpya wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize katika tangazo linalotarajiwa kutolewa muda wowote kuanzia sasa.

Kutajwa kwa Sallam Sk, kusimamia kazi za staa huyo, inakuja wiki kadhaa baada ya uvumi kwamba meneja huyo wa mwanamuziki mali, Diamond Platnumz, amejiondoa kusimamia lebo ya Wasafi.

Harmonize tayari ametangaza yuko mbioni kutangaza jina la meneja mpya, baada ya kuachana na meneja wake na mpenzi wake Kajala Masanja.

Minong'ono imesambaa mitandaoni kuwa Diamond na Sallam Sk, hawako vizuri na pengine wametupiana virago.

Minong'ono hiyo inaeleza kwamba Sallam kama vile amesusa kufanya kazi na Diamond, kiasi ambacho anakwepa kuambatana na msanii huyo katika ziara zake za muziki nje ya nchi.

Hata hivyo, kumekuwa na ukaribu wa Sallam Sk na wanamuziki wake wa zamani, Harmonize kiasi ambacho baadhi ya wadau wanaeleza ni dalili tosha kwamba meneja huyo amejiengua lebo ya Wasafi.

Hakuna aliyejitokeza kati ya Diamond na Sallam Sk kuelezea jambo hilo, japo kwa mtazamo wa wengi inaonyesha wawili hao wako katika ukaribu wa kufanya kazi kama ilivyokuwa nyuma.

Ukaribu wa Sallam na Harmonize unajadiliwa sana na wengi wanaona si jambo la kawaida na kwamba huenda ni wa kikazi.

Walitolea mfano kwamba wakati Diamond yuko Zanzibar katika shoo yake ya kumpongeza Rais Hussein Mwinyi, meneja wake huyo hakuwepo, lakini katika shoo ya Harmonize iliyofanyika katika kisiwa hicho alionekana akikumbatiana na msanii huyo.

"Sio suala la kuuliza hapa, ni wazi Sallam hayuko na Diamond na tunavyoona kupitia video ile ni kwamba Harmonize na huyu jamaa wana jambo wanalifanya pamoja," amesema mdau mmoja.

Kama akiondoka Sallam lebo ya wasafi, basi itakuwa ni mwendelezo wa watu wenye umuhimu kutoka na kutishia ustawi wa kundi hilo lenye muhimili mkubwa katika tasnia ya muziki.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**





**@shamsaford**
Kuna muda mwingine Mungu anakuepusha na mabalaa kwa kukukosesha vitu unavyopigania kuwa navyo karibu.

**@richmitindo**
Usije kuacha duka wazi ukakimbiza mwizi, Ni sawa ulichokiona kwa mchepuko kuna mtu kakiona kwa mkeo, kama uelewa wako mdogo usirudie kusoma.





**@Elizabethmichaelofficial**
Bwana Elon mwisho utuuwe kwa slesi, haya tuanzage kufanya mazoezi..! na bei za fotoshuti zitapanda. TUMEPATIKANA

**@roma_zimbabwe**
Vandame aliwapiga watu wengi saaana, wengine miamba haswaaa, na hakuwahi kupigwa kwa muda mrefu.
Siku moja alikutana na bwana mdogo tu, tulizoea kumuita #BrandonLee
DAME ALIPIGWA KAMA NGOMA!!



BASI SAWA

## Mc Pilipili kuichekesha Morogoro 'Boxing Day'




STAA wa vichekesho Bongo, Emmanuel Mathias maarufu kama Mc Pilipili, amewataka mashabiki kukausha mbavu zao kupitia onyesho lake la Christmas Comedy Festival litakalofanyika Desemba 26.

Akizungumza na BT, Pilipili amesema onyesho hilo litafanyika mkoani Morogoro katika ukumbi wa Mt. Uluguru Hotel na kusindikizwa na mastaa mbalimbali wa vichekesho kama Masanja Mkandamizaji, Leonardo, Oscar Nyerere, Mc Willy, Kipotosh, Mc Munga, DJ Wamoto na  Rahabu.

"Hii ni shoo ya familia kwahiyo unaweza kuja na marafiki zako na mpenzi wako, jambo la muhimu ni kwamba mapato yatakwenda kusaidia watoto wenye uhitaji mkoani humo na Dodoma," Mc Pilipili.

## Saraphina hawekagi 'vigodoro'



MSANII wa Bongo Fleva, Saraphina amesema anachukizwa na watu wanaomaliza bando lao kushinda mtandaoni kujadili umbo lake.

Amesema mwili wake umekuwa mjadala mkubwa kama anatumia 'kigodoro' kuongeza makalio yake, jambo ambalo si kweli bali Mungu ndivyo alivyomuumba awe hivyo.

"Mimi ndivyo nilivyoumbwa situmii kigodoro kuongeza mvuto, siwezi kuwaridhisha kila mtu kwani hata nikivaa dera watahoji. Muhimu uwe kama ulivyo kwa ajili ya kukupa  furaha." Amesema Saraphina.



# LADY JAY DEE, RAMA DEE WANAOGOPA MATOZO

NI kama wamerudi tena, ndivyo inaonekana kwa wakongwe wa muziki wa Bongo Fleva, Lady Jay Dee na Rama Dee, baada ya kuipua ngoma yao mpya inayoitwa Matozo.

Wakitumia mtindo wa 'Afrobeat' wawili hao wameonekana kufanya vyema katika wimbo huo na kuonyesha ukimya wao haukuwa wa bure, bali walikuwa wakijinoa kurudi jukwaani.

Hata kwenye video waimbaji hao wameitendea vyema kutokana na mandhari na mpangilio wa matukio kuwa wa kisasa na wenye ubora.



# Lukamba, Ceccy sasa hawashikiki

HALI ya mabishano makali inaendelea kati ya aliyekuwa mpiga picha wa Diamond, Lukamba na mke wake aliyemuacha Ceccy, kila mmoja akimtuhumu mwenzake kwa kusema uongo.

Hata hivyo, Ceccy amesema majibishano hayo kwake hayamhangaishi na kwamba hajaona faida ya Lukamba tangu alivyokuwa staa.

Amesema maneno anayotoa ni sawa na mkosaji na kwamba kinachotokea sasa ni kama hasira na kutaka huruma kwa jamii.

FILAMU

# Fitina:Heri mchawi kuliko fitina

**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI hawakukosea kusema 'heri ya mchawi kuliko fitina.

Hii inaonyesha kuwa mtu yoyote anayemfanyia fitina mwenzake anamsababishia mwenzake matatizo mengi mazito kuliko hata anayemroga.

Fitina zipo sehemu nyingi. Kwenye kazi, biashara, mahusiano, ndoa kote huko kuna fitina. Kuna baadhi ya watu wanataka kuona wenzao wakitaabika tu. Hawataki kuona wanafanikiwa. Kwenye mahusiano au ndoa wapo ambao hawapendi kuona watu wanapendana. Watafanya kila njia ili mkorofishane. Na kama wapenzi wenyewe wanapenda maneno ya kusikia, basi inakuwa ni rahisi sana kulivunja.

Filamu ya 'Fitina' inaeleza kila kitu. Imechezwa na wasanii Johnson Dastan, Amina Said, Mustapha Msigala, Theresia Joseph, Seif Ally, Samuel Ahmed, Rashid Khamis na wengineo.

John na mkewe Amina wanaishi kwenye ndoa ya amani na upendo kwenye kijiji fulani hapa nchini.

Wanapendana kama njiwa, bibi mbele, bwana nyuma. Mume pia amekuwa akimsaidia mkewe kazi mbalimbali kama kupika, kufua, kuchota maji, lakini pia wakikaa wenyewe wanaimbia hata nyimbo.

Aina hiyo ya mapenzi inawakera wengine ambao hawayapati kutoka kwa wake na waume zao. Zikaanza kutafutwa fitina. Ikawa inaenezwa propaganda kuwa huenda mwanamke amemuwekea mumewe dawa ya mapenzi, maarufu kama 'limbwata.'

Huyo mume mwenyewe John kila anapopita anaambiwa 'Bushoke'. Kuna dada mmoja jirani hapo anaitwa Jesca. Huyu alikuwa anataka anachofanyiwa Amina na mumewe awe yeye. Na akawa anampenda sana John kutokana na tabia yake hiyo kwa mkewe.

Akamchukia pia Amina.

John ana rafiki yake aitwaye Bravo. Walifanana hata tabia, ingawa Bravo alikuwa bado hajaoa. Naye alikuwa akimletea vijizawadi shemeji yake kama anavyofanya rafiki yake.

Ghafla tu, tabia ya John ikabadilika. Akaanza kumfokea mkewe na yale yote aliyokuwa anayafanya akasitisha baada ya 'kushikwa masikio' na wafitini.

Mke akawa mnyonge. Faraja yake kubwa ikawa ni shemeji yake Bravo ambaye yeye aliendeleza tabia ya kumletea zawadi na kumsaidia kazi ndogo ndogo. Wafitini wakavumisha kuwa Bravo anatembea na mke wa rafiki yake.

Siku moja, Jesca alimuona 'laivu' Bravo akitoka nyumbani kwa rafiki yake John wakati hayupo, akiwa tumbo wazi. Akaona tayari ameshapata ushahidi, akamwambia John. Akampiga mkewe na kumsaka Bravo kwa panga ili amuue.



Mke akakimbilia kwa shangazi yake John. Mume akaitwa na Bravo akaitwa pia. Kilichogundulika ni kwamba siku ile Bravo alipotoka ndani, ni kwamba aligonga hodi lakini akasikia kishindo kisicho cha kawaida, akaingia akamkuta shemeji yake ameanguka na  baada ya muda akazirai. Bravo akavua shati na kumpepea na kumpa huduma ya kwanza hadi akazinduka. Na wala haikuwa kama walivyovumisha. John akamuomba msamaha mkewe na rafiki yake Bravo.



# KALI 5 ZA TSHALA MUANA ZILIZOBAMBA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

DESEMBA 10 mwaka huu, mashabiki wa muziki wa rhumba duniani kote walipatwa na simanzi, baada ya kupata taarifa za kufariki dunia 'Malkia wa Mutuashi', Tshala Muana.

Alifariki dunia jijini Kinshasa akiwa na miaka 64 kutokana na maradhi ya kupooza ambayo yalimpata 2020, ambapo alisingiziwa kifo, lakini haikuwa hivyo, bali alikuwa amepatwa na ugonjwa huo.

Anakumbukwa mno nchini Tanzania kwani pamoja na kwamba kwenye miaka ya mwanzoni mwaka 1990 hadi mwishoni alikuwa akifanya ziara zake mara kwa mara, lakini pia nyimbo zake baadhi aliziimba kwa lugha ya kiswahili.

Alitunga na kuimba nyimbo nyingi kwa lugha nyingine kama kilingala, kifaransa, na nyingi zaidi aliimba kwa lugha ya kiluba katika mtindo wa mutuashi.

Kiluba ni lugha ya Waluba inayozungumwa maeneo ya Katanga na Kasai yaliyopo Kusini Mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Jina lake kamili ni Elisabeth Muidikay, alizaliwa Mei 13, 1958 Lubumbashi, na alianza muziki mwaka 1977 kama mchezaji shoo kwenye bendi ya Tsheke Tsheke iliyokuwa ikiongozwa na mwanamama mrembo wakati huo, Mpongo Love aliyeimba kibao maarufu cha 'Ndaya'.

Baadaye alianza kuimba na kujitegemea mwenyewe, ndipo alipoondokea kuwa maarufu mno. Wabongo watamkumbuka kwa vibao hivi.

**Sitambili**

Wimbo huu ulitoka mwaka 1986 na kwa kiasi kikubwa ndiyo ulimtambulisha Tshala Muana nchini Tanzania kiasi cha kuanza kuwa na wafuasi wengi walioanza kupenda kwa kufuatilia nyimbo zake, kwani aliimba kwa lugha ya kiswahili.

"Mpenzi wangu nitulize, unitilize miye wangu mi nalia moyo we. Mpenzi we natumaini natumaini, kesho utanikumbuka ee moyo we. Sasa mi najitolea najitolea, mwili mzima uchukue ee moyo ee." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo ambao ndiyo 'uliomtoa' mwanamuziki huyo hapa Bongo na kupata wafuasi wengi.

**Karibu Yangu**

Mwaka mmoja tu baadaye alipoona wimbo wenye lugha ya kiswahili umefanya vizuri Bongo alikuja na albamu nyingine aliyoiita 'Karibu Yangu.' Ni wimbo uliozidi kumpatia umaarufu mkubwa na kuanza sasa kufanya ziara hapa nchini. Baadhi ya mashairi yake ni haya.

"Unihurumie hurumie, nakukukua unite, unipeleke kwa baba akatupatie mali, tufunge oo ndoa ya lote, karibu oo karibu yangu."

**Dezo Dezo**

Alipofanya ziara nchini mwanzoni mwa miaka ya 1990, aliikuta bendi ya Zaita Musica chini ya Freddie Ndala Kasheba ambayo ilichukuliwa kutumbuiza kabla ya yeye kufanya maonyesho. Alivutia na nyimbo mbili, akaziomba kwa makubaliano maalum na Kasheba, akazichukua kwenda kuzirekodi nchini Ufaransa kwenye studio za kisasa na kuzifanya kuwa bora na kutangazika zaidi. Moja wapo ni huu 'Dezo Dezo'. "Unapenda Dezo Dezo, kodi ya nyumba hulipi, maji yameshakatwa, operesheni kata umeme inakuja."

**Kokola**

Upele ulikuwa umempata mkunaji. Moja ya nyimbo za Kasheba ulikuwa ni 'Kokola' aliouimba kwa lugha ya kiluba ambayo asilimia 70 ya nyimbo za Tshala Muana ameimba kwa lugha hiyo. Nao akauchukua na kwenda kuurekodi, ukapata umaarufu mkubwa.

**Mama Wenu**

Huu ni mmoja wa wimbo maarufu sana wa Tshala Muana ambao ulipendwa mno na mashabiki wa muziki wa Tanzania ukiacha zile  alizoimba kwa lugha ya kiswahili.

Hakuna aliyekuwa amebaki kwenye kiti kama ukipigwa kwenye sherehe mbalimbali za kijamii miaka ya 1990.

**BONGO FLEVA**

# Ticha star anyakua tuzo mbili muziki wa dansi Tanzania



USIKU wa siku ya Uhuru, kuliandaliwa tamasha maalum la utoaji tuzo kwa wasanii wa muziki wa dansi waliofanya vizuri mwaka 2022.

Miongoni mwa wasanii walionyakua tuzo hizo ni Ticha Star, ambaye alifanikiwa kung'ara katika vipengele viwili.

Ticha Star kutoka jijini Dodoma ameweza kutikisa tasnia ya muziki wa dansi kwa kushinda tuzo katika vipengele Msanii bora chipukizi na Wimbo bora wa kushirikiana.

Kilele utoaji tuzo hizo kilichofanyika kwenye ukumbi wa Break Point, Makumbusho mkoani Dar es Salaam.

Kibao kilichompatia tuzo hizo ni 'Ukinipenda' ambacho alikiachia mwezi Mei, akimshirikisha mwanadada Catty soul.

Tuzo hizo ambazo zina hadhi ya kitaifa zinatolewa kila mwaka na kampuni ya  Cheza Kidansi Entertainment.

Baada ya kupokea tuzo hizo, Ticha Star aliahidi kuongeza juhudi na kufanya makubwa zaidi katika muziki huo.

Alisema tayari amekamilisha nyimbo zingine mbili ambazo ni moto wa kuotea mbali anazotarajia kuziachia Januari mwakani.

Ticha star ametoa shukrani za dhati kwa mashabiki na wadau wote walioshiriki kumpigia kura nyingi, na kusababisha ushindi wake.

Aliwashukuru waandaaji wa tuzo hizo kwa kuwatia moyo wanamuziki wa dansi nchini kwa kuwapa tuzo wasanii wanaofanya vizuri.

Aidha, ameipongeza serikali kwa kuwainua wasanii mbalimbali katika njia tofauti kwa lengo la kutambulika ndani na nje ya nchi.

Ticha star amesema kwa sasa malengo yake ni kufika mbali kimuziki, na kushinda tuzo nyingi zaidi za nje ya mipaka ya Tanzania, kama walivyofanya wasanii wengine kama Diamond na Rayvanny.



# BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**FM Academia**

Leo Jumamosi wakiwa chini ya rais wao Patcho Mwamba, watatoa burudani katika ukumbi wa Kibamba Green Park, kesho watafanya vitu vyao ndani ya ukumbi wa Boardroom Sinza Mapambano.

**Twanga Pepeta**

Leo Jumamosi watazindua albamu yao ya 15 inayoitwa 'Chombo ya Fundi', katika ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe, kesho Jumapili wapo ndani ya ukumbi wa Hits Lounge Mtoni Kijichi.

**Malaika Band**

Bendi hii inayoongozwa na Christian Bella au 'Mfalme wa Msauti', leo Jumamosi itatoa burudani katika shughuli maalum, kisha itaendelea na maandalizi ya maonyesho ya Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya.

**Orchestra Sikinde Original**

Bendi hii mpya leo Jumamosi itakinukisha katika ukumbi wa Mawasiliano Park uliopo Kando ya Barabara ya Sam Nujoma Ubungo Dar es Salaam, kesho Jumapili wapo katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**The Boggos Musica**

Wakiwa chini ya rais wao Nyoshi El-Saadat, leo Jumamosi watatoa burudani  kwenye harusi, katika ukumbi wa JKT Mgulani, kesho watapumzika wakijiandaa na maonyesho ya Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya.

**Kimokimo Band**

Kama kawaida yao wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo  Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mjengoni Classic Band**

Ikiwa nyumbani kwake jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi ndani ya ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Town Classic Band**

Leo Jumamosi watawasindikiza Twanga Pepeta katika uzinduzi wa albamu ya 15, kesho Jumapili watafanya vitu vyao ndani ya ukumbi wa Twist Lounge Tabata, ambao zamani ulijulikana kama Kwetu Pazuri.

**Waluguru Original**


Bendi hii yenye maskani yake mjini  Morogoro, leo Jumamosi itatoa burudani ndani ya ukumbi wa Terminal Pub Msamvu, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

**Tukuyu Sound Band**

Kama kawaida yao, kila Jumapili vijana wa bendi hii watamalizia wikiendi yao katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma.

**Maina Band**

Bendi hii inayoongozwa na mwimbaji mkongwe, Liston Maina, leo Jumamosi itafanya makamuzi ya nguvu katika ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.



# FUNKE AAGA NOLLYWOOD

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Funke Akindele, amefichua mipango yake ya kustaafu kazi hiyo na kuweka akili yake katika siasa.

Amewaambia mashabiki zake kwamba filamu ya 'Battle on Bukka Street' ambayo imetoka hivi karibuni itakuwa filamu yake ya mwisho.

Hata hivyo, mrembo huyo ameeleza kwamba kwa sasa nguvu kubwa ameweka katika kuwania kiti cha naibu gavana kupitia chama cha PDP Julai mwakani.

Akindele amesema kuwa yuko tayari kulipa gharama ya kukabiliana na siasa, ikiwamo kusimamisha kazi yake katika tasnia ya filamu ya Nigeria.

Katika mahojiano na Deji Lambo wa Punch, mtayarishaji filamu huyo amesema kuwa filamu yake 'Battle on Buka Street', ni mradi wake wa mwisho na kwamba anajiingiza kikamilifu katika siasa.

Mwigizaji huyo yupo katika matayarisho makali ya kuwania unaibu gavana wa Jimbo la Lagos.

Aidha, amedai kuwa kuendelea kwake katika kazi hiyo ingemfanya kuwa nyuma kisanii, badala yake anawaachia wasanii wapya kuendelea na kazi hiyo.

Akindele alifichua haya alipoulizwa kuhusu kuhusika kwake katika mradi huo mpya.

"Mabadiliko makubwa yametokea kwa kuona, kutoka kuwa mwigizaji, sasa ninaandika, kuzalisha, kuongoza na kuibua sura mpya. Kwa hiyo, nimewaachia kijiti cha uzalishaji kwa vijana kwa sababu nimehamia kwenye siasa,"

Akaongeza "'Vita kwenye mtaa wa Buka' ni kama kuaga kwa sababu nitakuwa naibu gavana ajaye wa Jimbo la Lagos. Kwa hivyo, nimewaachia kijiti vijana wapya kwa sababu tunahitaji kuwapa fursa,"

Amesema bado atakuwa nyuma yao kuwashauri na kuwasimamia, wengi wamechoshwa kuona sura za zamani.




# Drake kuchumbia hakunaga sifa

RAPA maarufu wa Canada Drake, hatimaye amepata mkufu wenye vipande 42 vya madini ya Almas kwa jili ya kwenda kuchumbia.

Mkufu huo uliotengenezwa kwa dhahabu nyeupe ya gramu 18 vina karati 351.38 za almasi, iliundwa na mtengeneza vito mashuhuri kutoka New York, Alex Moss.

Moss alifichua kwamba vipande hivyo vya almasi 42 ni kwa ajili ya kumchumbia mpenzi wake ambaye hadi sasa hajawekwa wazi.



## Poul Okoye kaopoa tena

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, Paul Okoye, anayejulikana kama 'Rudeboy', amemtambulisha mpenzi wake mpya, Ivy Ifeoma.

Mwimbaji huyo alienda kwenye ukurasa wake wa Instagram kuweka video ikimuonyesha mpenzi wake huyo huku akisema anafurahishwa naye.

Mwimbaji huyo aligonga vichwa vya habari Jumapili iliyopita alipomuonyesha kwa mara ya kwanza walipokuwa wakisherehekea mwaka wao mmoja wa kuzaliwa.

## Kanye kalikoroga, sasa analinywa

RAPA maarufu wa Marekani Kanye West, ametajwa kuwa kinara wa watu waliofanya matukio makubwa ya kibaguzi dhidi ya Wayahudi.

Katika kura zilizopigwa na watu kupitia mtandao, kundi la StopAntisemitism limemtaja mwanamuziki huyo kama mshindi wa watu wenye chuki zaidi 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa StopAntisemitism Liora Rez, alisema "Kanye anatumia jukwaa lake la watu mashuhuri kueneza hatari za chuki dhidi ya Wayahudi,"





## Adele hukujua mapenzi sumu?

MWIMBAJI wa Uingereza, Adele amefichua kuwa alikuwa na vipindi vitano vya matibabu kwa siku wakati sakata la talaka na mume wa zamani Simon Konecki.

Akiwafichua mashabiki wake kwenye shoo yake mpya ya 'Weekends With Adele' huko Las Vegas, msanii huyo maarufu alisema kuwa alikuwa na vipindi hivyo ili kujizuia kupata talaka.

Adele amesema "Nilianza kupata tiba kwa sababu nilipita miaka michache bila hiyo. Nilihitaji kuanza ni wazi, nilipokuwa nikipitia talaka yangu. Kimsingi nilikuwa na vikao vitano vya matibabu kwa siku."

## Sina unakataa hukumpiga Korth

BINAMU wa mwanamuziki Davido, Adesina Adeleke, maarufu kama Sina Rambo, amekanusha madai ya unyanyasaji dhidi ya mkewe waliyeachana naye, Korth.

Korth, katika mfululizo wa malalamiko yake kupitia Instagram, alimshutumu Sina kwa vurugu huku akitangaza kuwa ndoa yao ilikuwa imeshakwisha kwa sababu alikataa kuvumilia aina yoyote ya unyanyasaji.

Kwa kujibu, mwimbaji huyo amesema madai ya Korth ni uongo na yenye nia ya kumpatia sifa mbaya kwa jamii.



**MAKALA**

# Huduma bora kwa wateja na nguzo muhimu katika utalii wa matibabu

**Na Mwandishi Wetu**

UMUHIMU wa kila muuguzi na mtumishi wa afya kuelewa maana ya huduma kwa wateja ni jambo la kuzingatiwa ili kuongeza ufanisi katika utendaji wao na kuchangia katika kujitangaza.

Weledi wa kuwahudumia wateja unakwenda sambasamba na uboreshaji wa huduma unaofanywa na kampuni au taasisi husika.

Hayo yamesemwa juzi na Mkufunzi John Nicholas kutoka Afrika ya Kusini wakati wa mafunzo ya huduma bora kwa wateja kwenye sekta ya Afya.

Mafunzo hayo ya kipekee yalitolewa wiki iliyopita na Kampuni ya AAM Consultancy kwa kushirikiana na BMK Trainings ya Afrika ya Kusini katika ukumbi wa Golden Tulip Posta mkoani Dar es Salaam.

Wafanyakazi waliohudhuria walitoka Hospitali ya Rufaa ya Bombo, Mount Meru na kliniki ya Esnan Dental ya Uturuki.

Mmoja ya wanufaika wa mafunzo hayo Dk. Mariam Ali Mtanda, kutoka kliniki ya Esnan Dental, anasema mafunzo hayo yameonyesha uhitaji na umuhimu wa kupewa kila mfanyakazi wa sekta hiyo.

Anasema waandaaji wa mafunzo hayo wanatakiwa kuandaa mafunzo mengine kama hayo ili kuweza kuwafikia watumishi wengi kwani manufaa yake ni makubwa.

Lengo likiwa ni kuendelea kuwajengea uwezo watumishi hao kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wanaohudumiwa.

Dk.Mtanda anaeleza mafunzo hayo yanasaidia kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi na kuboresha mfumo huo ambao ni muhimu wakati sasa kuna maandalizi ya kufanikisha mpango wa kutoa huduma ya afya kimataifa.

"Mafunzo haya yamenisaidia kuelewa umuhimu wa kile ninachokifanya, na kupata mbinu ya kuhakikisha huduma bora inadumu katika hospitali yetu, nadhani kozi hii inasubiriwa kwa muda mrefu, kuweza kuwafikia wauguzi wengi zaidi," anasema Dk. Mtanda.

Anaongeza "rai yangu kuwa mafunzo haya yawe yanatolewa mara kwa mara ili kukuza utoaji wa huduma bora kwa wateja nchini, hasa katika muda huu ambapo tunajiandaa kupokea wagonjwa kupitia mpango wa serikali wa kufungua mipaka na kuhamasisha utalii wa matibabu"

Akiwasilisha mafunzo hayo kwa wauguzi wa vituo mbalimbali vilivyoshiriki, mwezeshaji John Nicholas kutoka Afrika ya Kusini, anaeleza kuwa, utoaji wa huduma bora kwa mteja ni njia mojawapo ya kujitangaza hivyo ni muhimu kwa kila mmoja kufanya jitihada za kubadilika na kuwa na mtazamo chanya ili kuweza kuwahudumia wateja kwa namna bora zaidi.




**"Mafunzo haya yamenisaidia kuelewa umuhimu wa kile ninachokifanya, na kupata mbinu ya kuhakikisha huduma bora inadumu katika hospitali yetu, nadhani kozi hii inasubiriwa kwa muda mrefu, kuweza kuwafikia wauguzi wengi zaidi," anasema Dk. Mtanda.**



John anasema huduma bora kwa wateja si zoezi la msimu, kama ambavyo inasherehekewa, wala sio siku moja, bali ni zoezi endelevu linalohitaji mbinu na mikakati maalumu ikiwa ni pamoja na mfumo utakaohakikisha utekelezaji wa malengo ya kampuni iliyoyaweka na kuadhimia kuyatekeleza.

Anasisitiza kuwaelekeza watoa huduma kutabasamu pekee haikidhi mahitaji ya huduma bora kwa mteja.

Akitoa mfano kuwa wakati mwingine kutabasamu mbele ya mgonjwa anaehitaji msaada nikuonyesha dharau. Sekta ya Afya ni muhimu na yenye uhitaji mkubwa wa namna ya kutoa huduma bora kwa wateja.

Anazitaja njia mbalimbali za kuhudumia wateja na kuwa njia hizi zipo za ana kwa ana, lakini ni muhimu kujua aina gani inafaa Kwa kutambua mahitaji ya mteja.

Anasema ili kuleta mabadiliko katika kutoa huduma bora kwenye sekta ya Afya ni kuanza kumuangalia mgonjwa kama mteja.

"Faida nyingi zinaweza kupatikana mhudumu unapojiandaa katika kutoa huduma bora kwani si mteja pekee atafaidika, bali hadi mtoa huduma vilevile" anasema.


Kwa upande wake, Dk.Mtanda anasema kuwa, ili kituo kiwe kizuri ni muhimu kila mtumishi kukubali kujifunza na anapokosea inapaswa aambiwe ukweli ili kutorudia kosa na hatimaye kupata matokeo chanya.

Watumishi waliopata mafunzo hayo kwa pamoja waliahidi kubadilika katika utoaji wa huduma ili vituo wanavyoviwakilisha viwe mfano wakuigwa katika utoaji huduma nzuri kwa wateja wanaowahudumia.

Baadhi ya mafuzo yaliyotolewa katika wiki ya mafunzo ya huduma kwa wateja ni pamoja na kutambua huduma bora kwa wateja ni ipi, namna ya kupokea na kutatua changamoto za wagonjwa wakorofi, mfumo wa kupima na kuchukua taarifa za huduma kwa wateja.

# UGUMBA TISHIO LA DUNIA

- Uzalishaji mbegu za kiume wapungua
- Chanzo unene, ngono, kompyuta mpakato



KATIKA hali ya kutatanisha imebainika kiwango cha mbegu za uzazi za kiume kinachotolewa wakati wa tendo la kujamiiana kimeshuka kwa asilimia 51 katika kipindi cha miaka 50 iliyopita.

Hayo yamebainika katika matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Chuo Kikuu cha Hebrew cha Jerusalem, nchini Israel, kwa kushirikiana na chuo cha tiba cha Mount Sinai, nchini Marekani.

Watafiti walifanya mahesabu na kubaini kuwa katika miaka ya 1970, wanaume walikuwa na wastani wa uzalishaji wa seli za uzazi milioni 101 kwa mili lita ya majimaji ya mbegu za uzazi .

Wastani huo umepungua hadi kufikia milioni 49 katika miaka ya hivi karibuni.

Ushahidi pia unafichua kuwa kupungua kwa ubora wa seli za uzazi za kiume, pia hazina uwezo wa kupenya na kuingia ndani ya yai la uzazi la kike.

"Idadi kubwa za mbegu uwezo wa kutungisha mimba unapungua," anasema mtaalamu wa afya ya uzazi ya wanaume Moacir Rafael Radelli, ambaye pia ni makamu rais wa Shirika la Brazil la madaktari wa uzazi wa kusaidiwa.

Hali hii inayoendelea kuwa mbaya inatoa dalili za hatari miongoni mwa wasomi wa sekta ya afya.

Kuanzia miaka ya 2000, kiwango hicho kilipanda hadi 2.64%: zaidi ya mara dufu.

**TATIZO DUNIANI**

Wanasayansi waligundua kupungua kwa idadi ya majimaji yanayohifadhi mbegu za uzazi za kiume katika nchi za Ulaya, Afrika, Amerika ya Kati na Amerika Kusini.

Je ni nini kinachosababisha hali hii?

Wataalamu wanaeleza walau kuna sababu tano na habari njema ni kwamba kuna njia za kuzui tatizo hilo

**UNENE KUPINDUKIA**

Uzito wa mwili wa kupindukia huongeza athari kwa mbegu za kiume za uzazi.

Kuongezeka kwa ukubwa wa seli za mafuta, zinazomfanya mtu anenepe na kusababisha majeraha mwilini kwa kitaalam inafahamika kama inflammatory, ambayo huathiri uzalishaji wa homoni za uzazi za kiume au testosterone, ambazo ni muhimu katika kutengeneza maji maji yanayotunza mbegu za kiume.

Daktari wa uzazi wa wanaume nchini Brazil, Eduardo anasema uzito wa mwili wa kupindukia pia hutengeneza kile kinachoitwa oxidative stress , mchakato ambao huharibu seli mbali mbali za mwili.

"Kwa njia sawa na hivyo, mtu mwenye unene wa mwili wa kupindukia, huwa na mafuta zaidi katika maeneo ya viungo vyake vya uzazi, kitu ambacho huathiri vibaya utengenezwaji wa mbegu za uzazi za kiume ," anasema mtaalamu huyo.

Kende ambayo seli za uzazi hutengenezwa na kutunzwa, yanapaswa kuwa na kiwango cha joto cha nyuzi joto 1 hadi 2 wakati wote ili kufanya kazi vyema.

Hii ndio maana mfuko huo wa mbegu za uzazi uko nje ya mwili.

Hii inaongeza mzigo wa mafuta kwenye viungo vya uzazi, ambavyo huacha kufanya kazi yake kama vinavyotarajiwa.

Shirika la Afya duniani linakadiria kuwa asilimia 39 ya wanaume wana uzito wa mwili wa kupindukia duniani, takwimu ambazo zinadhihirisha sababu ya kupungua kwa mbegu za uzazi za wanaume katika miongo mitano iliyopita.

**MATUMIZI VILEVI**

Pombe, sigara za kawaida, sigara za kielekroniki, bangi, Cocaine na dawa zenye anabolic zinachangia uwepo wa tatizo hilo.

Je unafahamu kuwa dawa hizi zote hutumiwa mara kwa mara na idadi kubwa ya wanaume?

"Baadhi ya vilevi na madawa haya huharibu moja kwa moja seli za uzazi za kiume, ," anaeleza Dk. Miranda.

Kuna zingine hazina madhara ya moja kwa moja, huathiri homoni za uzazi zinazochochea utendaji kazi wa manii.

Mfano unaotolewa zaidi miongoni mwa wataalamu ni kubadilishwa kwa testosterone kwa njia ya tembe, jeli, na sindano, ambazo hutumiwa na wanaume ili kuongeza ukubwa wa misuli.

**MAAMBUKIZI MAGONJWA YA ZINAA**

Magonjwa kama vile Klamidia na kisonono, ambayo husababishwa na bakteria, yanaweza kusababisha majeraha katika njia ya mbegu za kiume iliyopo nyuma ya kende.

Njia hiyo huunganisha sehemu ya juu ya kende na ni sehemu inayotunza mbegu za kiume za uzazi.

Madhara yoyote kwa sehemu hiyo, husababisha hatari kwa mbegu za kiume za uzazi.

Shirika la WHO linakadiria kuwa, katika mwaka 2020 pekee, kulikuwa na visa vipya milioni 129 vya maradhi ya chlamydia na visa milioni 82 vya kisonono miongoni mwa wanaume na wanawake.

Kiwango hiki kimeendelea kuimarika na kuongezeka katika miongo ya hivi karibuni.

Radaelli anaongeza kuwa ugonjwa wa tatu kwenye orodha ya maradhi yanayosababisha kupungua kwa mbegu za kiume za uzazi ni virusi vya human papillomavirus, unaofahamika zaidi kama HPV.

"Pia unafahamika kwamba unaweza kuathiri uzalishaji wa mbegu au hata vinasaba DNA ya mbegu ya uzazi ," anasema.

**KOMPYUTA MAPAJANI**

Unakumbuka kuwa kende inapaswa kuwa katika hali ya hewa yenye kiwango cha katika ya 1 hadi 2, baridi kuliko sehemu nyingine yoyote ya mwili.

Tafiti zilizochapishwa katika miongo iliyopita zimefichua kuwa kubeba kipakatarishi chako au kompyuta mpakato kwenye paja kunasababisha hatari ya ziada katika uzalishwaji wa mbegu za kiume za uzazi.

Hii ni kwa sababu betri ya kifaa hicho hupata joto na inaweza kupasha joto mbegu za kiume.

Dk. Miranda anasema kwamba tabia nyingine zinazohusiana na viwango vya juu vya joto pia husababisha hatari kwa viungo vya uzazi.

Kwa mfano, kuoga kwa muda mrefu maji moto au kuingia katika sauna kwa saa nyingi ni hatari.

**KEMIKALI ZA SUMU**

Wataalamu wanatahatharisha pia kuhusu msururu wa kemikali za sumu zinazofahamika kwa ujumla kama endocrine disruptors.

Kemikali hizo ni pamoja na zile zinazochafua hali ya hewa, pamoja plasiki na kemikali za kuua wadudu.

Kwa ujumla, sumu hizo zina muundo sawa na ule wa homoni katika miili yetu.

**NINI LA KUFANYA?**

Kwa wale ambao wanataka kupata watoto, hatua ya kwanza ya kuongeza nafasi za kupata mtoto ni kufanya mabadiliko katika mtindo wa maisha unayoishi na hivyo kupunguza mchakato unaodhuru manii.

Hiyo ni pamoja , na kwa mfano kuimarisha au kupunguza uzito wa mwili kwa kula mlo kamili na kufanya mazoezi ya mara kwa mara ya mwili.

Kuepuka pombe, sigara na madawa mengine pia ni mambo ya msingi yanayoshauriwa uyafanye.

Watu wanaopata chanjo dhidi ya HPV katika miaka yao ya kwanza ya kubalehe pia hujikinga zaidi dhidi ya virusi hivyo na madhara ndani ya mwili

"Iwapo una umri wa chini ya miaka 35, wenzi wanapaswa kuwa na mtoto kwa hadi mwaka mmoja, kwa kufanya tendo la ndoa mara kwa mara, walau mara tatu kwa wiki , huku wakifuatilia kipindi cha utungwaji wa mimba," anasema Dk. Miranda.

Iwapo wenzi wana umri wa zaidi ya miaka 35, wanashindwa kupata ujauzito kwa zaidi ya miezi sita ni tahadhari kwao, na wanapaswa kupata ushauri wa kimatibabu.

Kama tatizo ni la upande wa mwanaume, wataalamu kwa kawaida humshauri kupata dawa mbadala zenye uwezo mkubwa wa kuondoa sumu mwilini, ambazo pia husaidia kuyalinda manii.

**Chanzo: BBC**

BALAA RUSHWA YA NGONO

# Laibua wanaharakati kupinga TAKUKURU kubadili sheria

## • Wamsihi Rais Samia awanusuru wanawake

Na Sabato Kasika

MAREKEBISHO ya kipengele cha Sheria ya Rushwa ya Ngono yanayofanyika ili kumhukumu aliyetendewa kosa hilo,yanahofiwa kuendeleza ukandamizaji kwa wanawake na kuongeza ukimya zaidi dhidi ya kuripoti na kuzungumzia vitendo hivyo.

Aidha, kuwahukumu wanaolalamikia rushwa ya ngono huenda kukasababisha wanawake kuendelea kuathirika kuanzia kudhalilishwa hata kuambukizwa maradhi bila watuhumiwa kuchukuliwa hatua.

Ni kwa mujibu wa tamko linalotolewa wiki hii na Mwenyekiti wa Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania Profesa, Ruth Meena .

Akizungumza katika Mkutano wa Kitaifa wa Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono unaofanyika Dar es Salaam, anasema wanamuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati kipengele cha 25 cha Sheria ya Rushwa ya Ngono kisipitishwe, kwa maelezo kwamba kinamhukumu aliyetendewa udhalilishaji huo.

"Kulingana na mapendekezo ya muundo ya sheria hiyo, kipengele cha 25 (ii) kinaelekeza kumhukumu anayedaiwa rushwa ya ngono. Kitendo hicho kitaendelea kuwalinda watu wanaofanya vitendo hivyo na kuwaathiri zaidi wanawake, ambao ndio waathirika wakubwa," Prof Ruth anasema.

Kwa mujibu wa maelezo yake kipengele hicho kinaweza kuongeza ukimya dhidi ya vitendo vya rushwa ya ngono na kusababisha wanawake kuendelea kuathirika bila hatua kuchukuliwa kwa wahusika.

"Tunamuomba Rais Samia na vyombo vinavyohusika na mabadiliko ya sheria hii ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bunge letu wasikubali pendekezo la kubadilisha kifungu hiki," anasisitiza.

Wadau hao ni mashirika zaidi ya 150, yanayounda mtandao huo, ambao sasa huenda wakawa na mvutano kati yao na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), katika vita hiyo.




Mwenyekiti wa Wanamtandao hao, Profesa Ruth Meena (katikati), aliposoma tamko lao. Wengine ni wajumbe wa wanamtandao hao Shamshad Rehematullah (kulia), Dk. Hellen Kijo-Bisimba, Rose Marandu na Clemence Mwombeki.



Madereva wa bodaboda ambao ni wanachama wa WAJIKI wakitoa elimu ya rushwa ya ngono mitaani eneo la Kigogo Dar es Salaam.

### RUSHWA KUONGEZEKA

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la Door of Hope Tanzania, Mwombeki Clemence, anasema sheria hiyo itawabana hata watendewa, na kwamba ukimya utazidi, taarifa hazitatolewa, hatua hazitachukuliwa na rushwa ya ngono itaongezeka.

"Katika mazingira hayo, tutakuwa na taifa linalofumbia macho vitendo vya ukatili ndani ya jamii na matumizi mabaya ya madaraka katika huduma za jamii ikiwamo afya, yanaweza kuzidi kuongezeka," anasema Mwombeki.

Anasema siku moja vyombo vya habari vilitoa taarifa kuhusu mama aliyelazimishwa kutoa rushwa ya ngono, ili mtoto wake mahututi apatiwe huduma, na kwamba jamii imechoka matukio kama hayo.

Mwombeki anaongeza kuwa hivi karibuni kiongozi mmoja wa dini alitoa ushuhuda kuhusu Profesa aliyekiri kwake kusababisha wanafunzi wengi aidha kufeli na wengine kujiua kwa kukataa kutoa rushwa ya ngono.

"Mchakato wa kubadilisha sheria ya kupambana na kuzuia rushwa ikiwa ni pamoja na kifungu cha 25 kinachobainisha rushwa ya ngono na rushwa nyingine kwa kuongezea kipengele 25 (ii) kitakachofananisha rushwa ya ngono na rushwa nyingine (supply na demand), unaendelea, lakini hatua hiyo inaweza kukwamisha vita dhidi ya rushwa hiyo nchini," anasema.

### NJOONI TUONGEE

Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma kutoka TAKUKURU, Joseph Mwaiswelo, anasema taasisi hiyo imefungua milango kwa wadau kutoa maoni ya kuboresha mabadiliko ya sheria hiyo.

"Bado tunaendelea na mchakato wa kutunga sheria, siyo kwamba imekamilika, maoni yenu yanaendelea kupokelewa, na ninaomba tuelewane kuwa tuko behewa moja tusigombane," anasema Mwaiswelo.

Anasema taasisi hiyo haina ugomvi na wanamtandao hao, na kwamba bado inatoa nafasi ya kutoa maoni ili hatimaye kufikia makubaliano yatakayosaidia kumaliza rushwa ya ngono nchini.

"Kwanza adhabu ya rushwa ya ngono imeongezwa kulingana na maoni yenu wadau na kwamba taasisi hii haiwezi kugombania chochote nanyi kuhusu suala hili, hivyo ninawaomba tuendelee kushirikiana," anasema.

Aidha, Mwaiswelo anakumbushia kuwa wadau hao walishatoa maoni kuhusu rushwa ya ngono kwenye kura ya maoni za vyama na kutaka iingizwe pia katika uchaguzi kama mwendelezo wa kudhibiti vitendo hivyo.

"Kwa niaba ya Mkurugenzi wa TAKUKURU, naomba niweke kumbukumbu sawa, kwa sababu tumeambiwa hapa kuwa tuliwaita Women Fund Tanzania (WFT) kusikiliza tu. Hiyo habari siyo kweli," anasema.

Anafafanua kuwa katika sekreterieti alikuwepo mjumbe kutoka WFT na wawakilishi wengine kutoka taasisi zinzofadhiliwa na WFT, ambao waliwasilisha maoni yao, na kwamba inashangaza kuona yanaibuka mapya.

### ELIMU MITAANI

Huku kukiwa na mvutano huo, shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), linaloendesha kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', limeamua kwenda mtaa hadi mtaa kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya rushwa ya ngono.

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawinza ,anasema wanachama wa shirika wakiwamo madereva wa bodaboda, wanatumia magari ya matangazo kwa kuzunguka mitaa mbalimbali ya jijini la Dar es Salaam.

"Septemba 22 mwaka huu, mimi ni miongoni mwa walioalikwa na TAKUKURU jijini Dodoma kutoa maoni kuhusu sheria hiyo, lakini hawakutupa uhuru, walitaka tukubali kuwa mtoa rushwa ya ngono naye abanwe bila kujali kwamba mazingira halisi ya utoaji," anasema Mawinza.

Mawinza anasema mbalimbali kutoa elimu, wanataka jamii iwaunge mkono, ili rushwa ya ngono isiunganishwe na nyingine, kwa kuwa utoaji wa rushwa hiyo unahusisha vitisho, kulazimishwa na kwa njia nyingine za hatari.

"Kwa kuwa rushwa hiyo inazidi kuota mizizi, sisi WAJIKI kama wadau, tumeamua kuingia mitaani kuelimisha umma, ili utambue madhara ya rushwa hiyo na mbinu nyingine zinazotumika kuifanikisha.

Anafafanua kuwa wataendelea kutoa elimu hiyo hadi mwaka kesho katika maeneo mbalimbali ya wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke, na kuongeza kuwa wanafanya chini ya uwezeshwaji wa WFT.

"Tumekuwa tukishuhudia kampuni, taasisi na watu mbalimbali wakitangaza shughuli zao kwa kutumia magari ya matangazo, sisi tunatumia magari kueneza elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono," anasema.

Mkurugenzi huyo anakumbusha kuwa rushwa ya ngono inadhalilisha na inaua, na kwamba bahati mbaya baadhi ya watu hawajui hayo wamekuwa wakiichukulia kama jambo la kawaida kama sehemu yao ya maisha.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kinamama walivyokuwa wakialikana kutwanga mahindi, mtama na mpunga

Na Adam Fungamwango



MIAKA mingi nyuma, hata mijini tu hakukuwa na mashine nyingi za kusaga na kukoboa. Kwenye jiji kubwa hata la Dar es Salaam miaka ya mwanzoni mwa 1990 kurudi nyuma pia hakukuwa mashine nyingi za aina hiyo.

Huko vijijini ndiyo kabisa, tena kwa sababu hakukuwa na umeme, kulikuwa na mashine chache sana ambazo zilikuwa zinatumia mafuta ya dizeli.

Inaweza ikawa moja tu mkoani, baadhi ya wananchi wa vijiji vya jirani wanakwenda kusaga na kukoboa hapo.

Na kuna wakati mtu anadamka alfajiri kwenda kusaga anarudi jioni au usiku na baiskeli yake kutokana na foleni kubwa anayoikuta.

Mijini nako ni hivyo hivyo tu. Nakumbuka Dar es Salaam kulikuwa na maeneo yanayohesabika ya mashine za kukoboa na kusaga.

Ila za Dar zilitumia umeme. Nazo pia zilikuwa na foleni kubwa.

Ingawa kwa sasa mijini mashine za kusaga na kukoboa, zinaonekana kama hazina umuhimu sana kama ilivyokuwa zamani.

Wakati enzi hizo utakuta makundi makubwa ya akinamama na watoto mashineni, lakini kwa sasa huwezi kukuta hali kama hiyo, hasa mijini.

Maendeleo ya teknolojia yamesababisha hali hiyo. Kwa sasa kuna unga wa sembe au dona ambao tayari umefungwa kwenye mifuko, umeshakobolewa na kusagwa.

Hata mpunga kwa sasa kwa asilimia kubwa unakobolewa huko huko mashambani. Kuna matrekta ambayo yanavuna na kukoboa kwa wakati mmoja, pumba kwake na mchele kwake.

Si rahisi kuona mtu anasafiri na mpunga kutoka kijijini kwenda mjini, au kutoka mikoani kwenda Dar. Anakwenda na mchele tu.

Kwa siku za karibuni ukimuona mama mashineni basi anakwenda kusaga mchanganyiko wa vyakula vya mtoto, ambavyo ni mchanganyiko wa vyakula lishe, karanga na dagaa. Pia navyo tayari wafanyabiashara wameshaanza kusindika. Kuna unga spesheli ambao unachanganywa na vitu vyote hivyo na kuuzwa madukani kwenye mifuko maalum.

Hebu turudi sasa miaka ya nyuma tuangalie akimama wengi walivyokuwa wakikwepa adha ya kwenda kukoboa mahindi, mtama na mpunga na kuamua kutwanga wenyewe. Walikwepa usumbufu wa foleni au gharama.

> **Baba huyo alikuwa akilalamika kuwa wanawake wa siku hizi wamekuwa wavivu kiasi kwamba wanashindwa kuwapikia vyakula vya kitamaduni, hata kutwanga tu shida kwa sababu ya kuogopa kuharibu kucha zao.**

Wakati mwingine ni kupunguza kazi ya leo kwenda kukoboa na kesho kwenda kusaga. Wakati mwingine hata hayo mahindi huyakoboa na baadaye kuyatwanga kabisa kupata unga ambao unachekechwa na chenga zake zinarudiwa tena kutwangwa.

Kuna waliokuwa wakitwanga mahindi kwa ajili ya kukoboa tu kwa ajili ya kande. Mtama nao ulitwangwa ili upatikane unga.

Mpunga ulitwangwa kwa staili ya kukobolewa tu, na baada ya hapo unawekwa kwenye ungo na kupepetwa, ili kutenganisha chuya na mchele wenyewe.

Kwanza akinamama walikuwa wanafanya kazi ya kualikana. Mwenye mpunga wake, mahindi au mtama ataomba msaada kwa mashoga zake. Na kazi hiyo mara nyingi huanza jioni kuanzia saa tisa hadi saa 12:00 jioni.

Jioni watakusanyika eneo husika. Kunaweza kuwa na kinu kimoja au viwili. Wawili wawili watatwanga kwenye kila kinu kimoja.

Wakati mwingine kinu kimoja wanaweza kutwanga watatu kama wamealikana wengi. Hapo pembeni hatari kuna ungo mmoja au miwili au mitatu ambayo baadaye itatumika kupeta mahindi yaliyokobolewa, au mpunga baada ya kutwangwa.

Watoto watakusanyika pembeni kuwaona mama zao jinsi wanavyofanya kazi hiyo. Kila mmoja anakuwa ameshika mchi, anainua juu na kuurudisha ndani ya mchi kwa nguvu. Wakati huyo anarudisha chini mwingine anakuwa ameinua juu. Hata kama watatu kwa kinu kimoja kutakuwa na mpishano mmoja wa kuvutia na kushangaza.

Wakati mwingine kinu kinazungushiwa khanga ili mahindi yasimwagike.

Sasa hapo unaweza kukutana na akinamama wenye mbwembwe, anaweza akainua juu mchi halafu akauachia, akapiga mikono yake, halafu haraka akaudaka na kuendelea kutwanga.

Hii ilikuwa ni burudani sana ukiwaangalia. Unaweza kukuta wengine wanatwanga huku wakiimba nyimbo. Wakimaliza wataanza kupeta, wakiwa wamejifunga kitambaa kichwani ili kujikinga vumbi la chuya au pumba. Wakilamaliza kila mmoja atatimka nyumbani kwake. Kinachofuata hapo ni kwamba aliyewaalika atawapelekea ama unga, mchele au mahindi yaliyokobolewa kama yatakuwa ya kande.

Kwa sasa mambo hayo hayapo tena, si mjini tu, yameanza kuadimika hata kijijini. Ukimkuta mama anatwanga labda kisamvu. Mjini huku sasa hata kisamvu chenyewe kinatwangwa na mashine.

Siku moja nilisikia malumbano ya baba na mama mmoja mtaani, kila mmoja akivuta kwake.

Baba huyo alikuwa akilalamika kuwa wanawake wa siku hizi wamekuwa wavivu kiasi kwamba wanashindwa kuwapikia vyakula vya kitamaduni, hata kutwanga tu shida kwa sababu ya kuogopa kuharibu kucha zao.

Mwanamama akamjibu kuwa nyakati zimebadilika na haziwezi kurudi nyuma. Akasema siku hizi kila kitu kinauzwa kwenye vifungashio. Unga wa sembe, dona, mchele, na mashine pia zipo, ya nini kuhangaika kutwanga.

Akamwambia kama hata mashine za kufulia nguo zipo kwa nini mtu ajisumbue kufua? Na kama trekta zipo kwa nini mtu utumie jembe ya mkono?

Akamwambia mabadiliko ya sayansi na teknolojia yamebadilisha mfumo wa maisha, kiasi cha kurahisisha, hivyo asitake wanawake waendelee kuwa vile vile kama zamani. Nao wanabadilika kutoka kizamani na kuishi kwa kutumia vifaa vya kisasa.

**Tuma meseji 0716 350534**

## HABARI KIMATAIFA

### Biden kufanya ziara Afrika mwakani

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema ataitembelea Afrika mwaka unaokuja katika wakati nchi yake inalenga kuyaweka karibu zaidi mataifa ya bara hilo ili kukabiliana na ushawishi unaoongezeka wa China.

Rais Biden ametoa tangazo hilo katika siku ya mwisho wa mkutano wa kilele kati ya Marekani na Afrika uliotilia mkazo nia ya utawala wake kutanua ushirikiano na nchi za Afrika ikiwa ni pamoja na kulipa umuhimu bara hilo kwenye jukwaa la kimataifa.

Ziara hiyo ambayo bado haijapangwa wala kuorodhesha mataifa atakayoyatembelea, itakuwa ya kwanza kufanywa na kiongozi wa Marekani kwenye mataifa ya Afrika kusini mwa jangwa la sahara katika kipindi cha muongo mmoja uliopita.

Katika mkutano uliomalizika juzi Marekani iliahidi kutoa kitita cha zaidi ya dola bilioni 2 kulisaidia bara la Afrika kwenye masuala ya usalama wa chakula na demokrasia. **DW**

### ANC yaanza mkutano wake mkuu

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI.

CHAMA tawala nchini Afrika Kusini ANC,kimeanza mkutano wake mkuu jana ambao unatarijiwa kumchagua kwa mara nyingine Rais Cyril Ramaphosa kuwa mwenyekiti.

Rais Ramaphosa anachaguliwa licha ya kashfa iliyomchafulia jina wiki kadhaa zilizopita.

Kiongozi huyo anawania muhula mwengine wa uongozi wa chama hicho katika wakati ANC inakabiliwa na mivutano ya ndani na kupoteza uungaji mkono wa wapigakura kwenye historia yake ya miaka 28 ya kuwa madarakani. Mwanasiasa huyo anayejinasibu kuwa mpinga rushwa alichukua hatamu za uongozi wa chama mwaka 2017 baada ya mtangulizi wake Jacob Zuma kuandamwa na kashfa nyingi za rushwa na ukiukaji wa maadili.

Hata hivyo taswira ya Ramaphosa nayo imeingia doa wiki chache zilizopita baada ya kutuhumiwa kuwa alificha taarifa za wizi wa kiwango kikubwa cha fedha uliotokea kwenye shamba lake huko Phala Phala **DW**

# Russia yazidi kuiponda Ukraine, raia wateseka kukosa maji, umeme

**KYIV,** UKRAINE

MASHAMBULIZIU makubwa kutoka Russia yamepiga katika maeneo mbali mbali nchini Ukraine, huku miundo mbinu muhimu ikionekana kulengwa.

Katika mji mkuu wa Kyiv, maofisa walisema kuwa shambulio kubwa la makombora limepiga ukingo wa kushoto wa Mto Dnipro pamoja na wilaya ya kusini- magharibi, na kuyaacha maeneo ya mji huo bila umeme na maji.

Mji wa pili kwa kubwa wa Kharkiv hauna umeme baada ya makombora 10 kupiga katika eneo hilo.

Miji mingine mikuu ambayo ni pamoja na Odesa na Zaporizhzhia pia imeshambuliwa.

Katika mji wa Kryvyi Rih, majengo ya makazi yalipigwa, watu wawili wamefariki na wengine watano wamejeruhiwa, wakiwemo watoto wawili, walisema maofisa.

Ukraine imeishutumu Russia kwa kutumia majira ya baridi kama silaha kwa kushambulia huduma muhimu wakati nchi ikikumbwa na majira ya baridi.

Russia imepiga zaidi ya makombora ya masafa marefu 1,000 na droni zilizotengenezwa na Iran, maafisa walisema.

Tangu oktoba kumekuwa na mashambulizi ya mfululizo kati yake yamekuwa yakizimwa na mifumo ya ulinzi ya anga ya Ukraine.

Aidha, wakazi wa Kharkiv nchini Ukraine wamekuwa wakizungumza na BBC kuhusu mashambulizi hayo walisema kuwa alishuhudia mashambulio ya silaha nzito na ghafla umeme ukakatika .

Akizungumza na kipindi cha BBC World Service cha Newshour kabla ya matangazo, alikumbuka hali ya mateso yasiyoisha.

Alisema kinachoifanya hali kuwa mbaya zaidi ni ukweli kwamba yeye ni mama wa mtoto mchanga wa miezi mitatu.

Katika hatua nyingine, Ukraine imeishutumu Russia kwa kupanga mashambulizi ya ardhini katika kipindi cha mwaka mpya.

Rais Volodymyr Zelensky na maofisa wakuu walionya kwamba nchi hiyo na washirika wake lazima wajilinde dhidi ya kuridhika.

Mashambulizi hayo yanaweza kutokea katika eneo la mashariki la Donbas, kusini, au hata kuelekea Kyiv, majenerali wakuu walisema.

Wachambuzi wa nchi za Magharibi walisema uwezo wa Russia kufanya operesheni za kushambulia kwa mafanikio unapungua kwa kasi.

Ofisa mkuu wa kijeshi wa Uingereza Admiral Sir Tony Radakin alisema wiki hii kwamba vita vitazidi kuwa vibaya zaidi kwa Russia ambayo inakabiliwa na uhaba mkubwa wa silaha za mizinga.

Katika mfululizo wa taarifa kwa vyombo vya habari, Waziri wa Ulinzi wa Ukraine Oleksii Reznikov, alisema ushahidi unaongezeka kwamba Russia ambayo imepata hasara nyingi katika uwanja wa vita, inapanga mashambulizi mapya.

Alikisia kuwa inaweza kutokea Februari wakati nusu ya wanajeshi 300,000 walioandikishwa Oktoba kusaidia vita vya Ukraine wangemaliza mafunzo.

"Sehemu ya pili ya usajili wa wanajeshi wa ziada takriban 150,000 wanachukua angalau miezi mitatu kujiandaa. Ina maana wanajaribu kuanza wimbi jingine la mashambulizi pengine mwezi Februari, kama mwaka jana. Huo ni mpango wao," alisema Reznikov.

Mashambulizi mapya yanaweza kutokea mara Januari, lakini uwezekano mkubwa zaidi katika majira ya kuchipua, ilisema tathmini hiyo ilitoka kwa Rais Zelenskiy, Jenerali Valery Zaluzhny na Jenerali Oleksandr Syrskyi katika mahojiano ya hivi karibuni. **BBC**




Mwanamke akipita katika jengo la ofisi mbalimbali ambalo limeharibiwa kwa mashambulizi ya Russia katika mji wa Donetsk, nchini Ukraine. **PICHA: REUTERS**

### Tisa taabani kwa kula Spinachi

**CANBERRA,** AUTRALIA

RAIA wa nchi ya Australia wamekuwa na hofu baada ya kutolewa tahadhari kufuatia watu tisa waliokula mboga aina ya Spinach yenye sumu kuguua na kuchanganyikiwa.

Watu hao walihitaji huduma ya matibabu baada ya kula mboga hiyo ya Spinach inayolimwa na kampuni ya Riviera Farms iliyopo katika eneo la Costco.

Maofisa wa afya walisema dalili za ugonjwa huo zilikuwa ni pamoja na kuchanganyikiwa , kuongezeka kwa viwango vya juu vya joto la mwili na kushindwa kuona vizuri.

Kampuni ya Riviera Farms ilisema kuwa spinach hizo zilikuwa zimechafulia na magugu, lakini hakuna bidhaa nyingine zilizoathiriwa.

Idara ya afya ya New South Wales ilionya kuwa paketi zenye nembo ya spinachi hiyo zenye tarehe ya usindikaji ya 16 Disemba sio salama kuliwa na zinapaswa kutupwa.

Ilimtaka yeyote aliye na dalili zisizo za kawaida za ugonjwa baada ya kula mboga hizo kupata huduma ya matibabu ya hospitali haraka. **DW**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI
S L P
MWANZA

**OMBI LA URAIA**



**MAIMUNA ABDILLAHI ALI**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh waziri wa mambo ya ndani ya nchi, utaifa wake wa sasa ni KENYA inchi atokayo ni KENYA shughuli zake ni mama wa nyumbani na anwani yake ni SLP MWANZA yupo nchini tangu mwaka 1990.
Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania atume taarifa ya maandishi kwa kamishna Jenerali wa uhamiaji SLP 512, Dar es salaam. Kumb na DN

Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999
KUSUDIO LA KUTOHUSISHA MILIKI YA ARDHI

MMILIKI ALIOANDIKISHWA: OMARI RASHID WA S.L.P MOROGORO
ARDHI: KIWANJA NA. 16 KITALU "O" MTAA WA KONGA
MANISPAA YA MOROGORO
MUOMBAJI: SEGOLINA DIONIS CHUWA S.L.P 6206. MOROGORO.

Taarifa inatolewa kwamba **HATI YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imekwisha muda wake na ninakusudia kutohusisha miliki yake kwa aliyekua mmiliki wa kwanza ndugu **OMARI RASHID.**
Zaidi sana ofisi inakusudia kumilikisha ndugu **SEGOLINA DIONIS CHUWA** ambaye ndiye anayendeleza kiwanja hiki iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti

**MAELEZO** yoyote yaelekezwe kwa M**KURUGENZI WA MANISPAA YA MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

# Wawasilisha pingamizi mali zilizopigwa mnada

**Na Grace Gurisha**

MAWAKILI George Masudi na Godfrey Ambet wamewasilisha mahakamani pingamizi la awali la kupinga maelezo ya mashahidi watatu katika shauri la madai namba 40/2028 lililofunguliwa na wasimamizi wa mirathi ya marehemu Joseph Katambi.

Awali mawakili hao baada ya Joseph kufariki dunia Novemba 23, 2020 waliomba kufanya marekebisho na kuwaweka wasimamizi wa mirathi Aloyce Katambi, Michael Katambi na Hoteli ya Hilux Ltd kama walalamikaji katika shauri hilo.

Kesi hiyo ilifunguliwa na Joseph dhidi ya Benki ya CRDB PLC, kampuni ya minada ya Comrade Auction Mart, Court Brocker na kampuni ya Great Vision Adventures kwa kuiomba Mahakama Kuu itamke kuwa mali za marehemu hazikuuzwa kihalali kutokana na mkopo aliyoukopa.

Pingamizi hilo liliwasilishwa jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa mahakama hiyo wakati shauri hilo lilipoletwa kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji wa mashahidi wa upande wa walalamikiwa.

Ambet alidai kuwa maelezo hayo ya mashahidi watatu wa upande wa walalamikiwa yatupiliwe mbali kwa kuwa yana upungufu wa kisheria.

Alidai kuwa maelezo hayo hayajatiwa saini na mashahidi hao na pia hayana tarehe kuwa yaliandaliwa lini, hivyo nyaraka hizo ziliwasilishwa mahakamani kinyume cha matakwa ya kisheria.

Wakili Masudi alidai kuwa maelezo hayo hayaendani na maelekezo yaliyowekwa kwenye Tangazo la Serikali namba 355 lililochapwa Mei 20, 2022.

Alidai tangazo limetoa marekebisho ya fomu mbalimbali za madai 'fomu C/13', ambapo maelezo ya mashahidi yanapaswa kufuata marekebisho hayo, hivyo kwa kutokuyafuata, fomu zao zimekwenda kinyume.

Kesi itaendelea kusikilizwa Februari mwakani mbele ya Jaji Kakolaki ambapo katika hati ya madai wadai wanaiomba mahakama itamke mali zilikuwapo kwenye Ploti 301 Block DD eneo la Msufini, mjini Morogoro, Ploti 303 Block DD Morogoro bado zipo kwenye umiliki halali wa mlalamikaji.

Pia wanaiomba itamke mnada uliofanyika wa kuuza mali ulikuwa ni batili kwa sababu hakupata utaratibu wa kisheria na pia iwaamuru walipe fidia kutokana na kuzuiwa kuendelea kufanya biashara ya hoteli hiyo baada ya kuuzwa kwa hoteli hiyo.

Kitambi analalamika kuwa mali zake zimeuzwa kinyume cha sheria kwa sababu tayari alishaanza kufanya mazungumzo na benki hiyo jinsi ya kuwalipa mkopo wake, lakini wakati wanaendelea na mazungumzo hayo wao wakauza mali zake wakati yeye alalimini kuwa anaweza kulipa mkopo huo.




Askari wakiwa wamesimamisha daladala baada ya kuingilia msafara wa wadau wa kupinga rushwa ya ngono kutoka Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), waliokuwa wakipita maeneo ya Mabibo, Dar es Salaam, kutoa elimu ya kupinga rushwa hiyo, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA.**

## Mahakamani tuhuma za kughushi ridhaa ya mke kupata mkopo benki

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Kitunda Mwanagati, jijini Dar es Salaam, Seleman Maziku, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na tuhuma za kughushi ridhaa ya mke wake na kujipatia Sh. milioni 140.

Akisoma hati ya mashitaka jana, Wakili wa Serikali Yusuph Aboud alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio, kuwa Desemba 10, mwaka huu, mahali pasipojulikana, mshitakiwa alighushi ridhaa ya mkewe, Scola Bundala.

Aboud alidai katika shtaka la pili, siku hiyo hiyo, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Maziku alijipatia mkopo wa Sh. milioni 140 kutoka benki ya Stanbic baada ya kuwasilisha ridhaa hiyo ya kughushi ya mkewe.

Hata hivyo mshitakiwa alikana kutenda makosa hayo na kwa mujibu wa upande wa mashitaka, upelelezi katika kesi hiyo umekamilika.

Hakimu Mary alisema ili mshitakiwa awe nje kwa dhamana anatakiwa awe na wadhamini wawili wenye barua watakaotoa fedha taslimu Sh. milioni 70 kila mmoja au kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo.

Mshitakiwa alishindwa kutimiza masharti ya dhamana na amerudishwa rumande hadi Desemba 28, mwaka huu kesi hiyo itakapokuja kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

**Hata hivyo mshitakiwa alikana kutenda makosa hayo na kwa mujibu wa upande wa mashitaka, upelelezi katika kesi hiyo umekamilika.**

## Waandishi kunolewa kuandika habari za uchunguzi kuchochea maendeleo

**Na Jenifer Gilla**

UMOJA wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na Asasi ya Jamii Forums wamesaini makubaliano ya ushirikiano wa kimkakati wa kuwajengea uwezo waandishi wa habari ya namna ya kuandika habari za kiuchunguzi na zenye maslahi kwa umma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa UTPC, Keneth Simbaya, alisema lengo la mkakati huo ni kuchochea uwajibikaji na utawala bora katika jamii kupitia taarifa za kina zitakazoandikwa na waandishi hao.

Alisema mkakati huo umekuja baada ya kugundua kuwa uandishi wa habari za kiuchunguzi umeshuka kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo uoga wa waandishi kuandika habari za namna hiyo pamoja na kutokuwa na elimu ya namna ya kuziandika.

"Waandishi pia watajengewa uwezo kuhusu usalama wa kidigitali, matumizi sahihi na bora wa vifaa na mifumo ya kidigitali na namna bora ya kutumia uwanja wa kidigitali kuendeleza kazi zao, ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia," alisema Keneth.

Alisema pia watatoa mafunzo kwa waandishi wa habari ya namna ya kuandika habari zenye kugusa maslahi mapana ya umma, ili kuchochea mabadiliko na kuwa sehemu ya wenye kuleta mabadiliko chanja kwa jamii inayowazunguka.

Mkurugenzi wa Jamii Forum, Maxence Melo alisema ushirikiano huo utarahishisha kazi ya uhakiki wa taarifa kutoka sehemu mbalimbali nchini kupitia jukwaa la Jamii Check walilolizindua, ili kuhakiki taarifa mbalimbali zinazosambaa mtandaoni na nje ya mtandao.

Aidha, alisema kupitia ushirikiano huo pia wanatarajia kuendesha shindano la uandishi wa habari zenye kuleta mabadiliko litakaloshirikisha waandishi habari wote nchini ambapo washindi watapewa tuzo mbalimbali kuanzia mwakani.

"Tunatarajia ushirikiano huu utakuwa chachu ya kukuza tasnia ya habari na kuzalisha wanahabari wenye uwezo wa mkubwa wa kufanya kazi zinazoendana na mabadiliko ya dunia na kuongeza maudhui yenye tija na uhakika mtandaoni," alisema Maxence.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-10

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Mimi niko tayari kwa sharti lolote utakalonipa, lakini hili liishie humu."

"Nataka unikubalie, niwe mpenzi wako."

Mary aliangalia juu kama kuna kitu anafikiri, akajibu.

"Mimi sina neno na hilo. Niko radhi, ila tu itabidi univumilie kidogo."

"Kuna nini tena?" Akang'aka.

"Nilikuwa na matatizo ya tumbo, nikaenda hospitali, nikapimwa na kupewa dawa za kutumia ambazo naendelea kuzitumia. Sasa waliniambia nisifanye kitu chochote kwa miezi mitatu. Ikiisha tu basi tutaanza rasmi uhusiano," akaongea kwa sauti ndogo na ya aibu.

"Mimi nitajuaje kama dozi hiyo imeisha baada ya kufika miezi mitatu?"

"Nitakwambia, lakini na wewe hesabu kuanzia mwezi huu, ikiisha sina hata haja ya kukwambia. Ila naomba sasa usiwe uko sana karibu yangu, si unajua nina mchumba."

"Najua Mary. Imeisha hiyo. Mimi kesho tu nitakwenda kwa mzee Chale. Hana tatizo yule anapenda pesa tu, nikimpa milioni zake mbili tu, atanyamaza. Halafu shoo nasimamia mimi mwenyewe. Nitamwambia habari hii haitakiwi kuvuka kijijini hapa."

"Nitashukuru sana."

"Kama kweli umenikubali, hebu naomba nikubusu."

Kwa aibu za kike, Mary aligeuza kichwa chake. Usonzo akapeleka mdogo wake shavuni, akambusu.


"Samahani kuna kitu kingine muhimu ambacho nilitaka kusahau." Mary alikaa tena kwenye kiti cha wageni kwenye ofisi ya Usonzo.

"Mhh, wewe nawe umeshaanza hivyo, hujaacha tu mambo yako?" Tayari Usonzo alishaanza utani wa mtu na mpenzi wake.

"Eee, nalo hili lililotaka kusahau ni muhimu sana."

"Lipi Baby?" Usonzo alikuwa ameshaanza kujimilikisha.

"Ni kwamba, baada ya tukio la kumwagia tindikali, nilimchukua na kumpeleka hospitali, gharama zote zimetolewa na wazazi wangu, ndugu zangu na kiakiba changu nilichoweka. Nilichofanya ili yasiwe makubwa na yasifike mbali baada ya akili kunirudia baada ya hasira ni kumuomba radhi kijana wa watu.




**"Sasa je. Mpango huo hata mchumba wangu Enock anaujua na kuuelewa, ingawa sijamwambia hilo jambo la kumkubalia kuwa mpenzi.**

Nimetumia ujuzi wangu wote wa kike, hadi amekubali. Nimemdanganya kuwa nimemkubalia awe mpenzi wangu..."

"Hapo ndipo ulipokosea, unamwagiaje tindikali, halafu baadaye umwambie unamkubalia, usingemwagia basi..."

"Sikiliza bwana Usonzo, wewe ni mwanaume, uwe mvumilivu, mtulivu na mwelewa." Kauli hiyo ilionekana kumvunja nguvu baada ya kuonekana anaanza kulaumu.

"Nimekwambia nimetumia njia hiyo ili akubali kunyamaza na kutokwenda kushtaki. Kumbuka yule kwao ni Dar es Salaam ambako kuna kila kitu, anaweza kwenda huko akashtaki wakaja maaskari kutoka Kituo cha Kati Dar. Nimemwambia asishtaki na nimemwambia pia nitamgharamia gharama za matibabu Dar es Salaam ili wakafanye uchunguzi huenda anaweza kuona tena. Baada ya kumwambia hivyo amekubali. Nikatoka hapo, nikaenda hadi kwa ndugu zake, maana mtu anaweza kukubali, lakini ndugu zake wakapinga. Nao nimewatuliza kwa kuwaambia kuwa ndugu yao anaweza kupona kwa kumpeleka Dar kwa matibabu zaidi, lakini ukweli ni kwamba hawezi kupona au kuona maisha yake yote daktari amethibitisha."

"Sasa anaondoka lini huku kwenda kwenye matibabu feki atuondolee jinamizi sisi huku?"

"Usonzo, jambo hili ni kubwa, usilione ni rahisi rahisi, limekaa kimitego sana. Ndiyo maana nimekwambia bado kuna kitu hapa.

Wewe naona kimekuuma kukwambia nimemkubalia uwe mpenzi wangu. Yule kwa sasa nakaa naye nyumbani ili asishawishiwe na mtu kubadili mawazo akaenda kushtaki. Yeye anaamini kuwa atakwenda Dar kutibiwa atapona, na baada ya hapo ndiyo tutaanza kuwa wapenzi..."

"Ahaa, yaani umemdanganya akishatibiwa ndiyo mtaanza rasmi uhusiano?"

"Sasa je. Mpango huo hata mchumba wangu Enock anaujua na kuuelewa, ingawa sijamwambia hilo jambo la kumkubalia kuwa mpenzi.

"Du, msichana una akili wewe, yote haya kakufundisha nani? Yaani wewe Mafia."

"Ngoja, sikiliza sasa, ndiyo nakuja huko."

Enhe, lete habari mpenzi."

"Kwa maana hiyo pia ninaomba kiasi cha pesa kidogo ili nikawapelekee ndugu zake hapa kijijini kama rushwa wasiongeeongee sana. Halafu nataka nimlete kwako, ili umwambie kuwa wewe utagharamia matibabu yake yote mjini. Unajua tayari ameshanza kuniuliza wewe pesa zote utatoa wapi? Nimemwambia nina wadau wangu watanisaidia."

"Yaani kwa plani yote uliyoifanya nakupa mia kwa mia, hata kesho mlete nimwambie mimi nitamgharamia kila kitu, safari pamoja na matibabu."

"Sawa ila subiri muda wa kumuondoa hapa utakuwa ule ambao nilikwambia tutaanza rasmi uhusiano. Miezi mitatu ijayo."

"Halafu tunampeleka Dar, Muhimbili tunamtelekeza huko huko."

"Sawa kabisa."

"Ila nina swali hapo kidogo Mary?"

"Lipi tena Usonzo na wewe?"

"Kama akitoka hospitalini huko na kuwataja waliomtelekeza si anaweza kuja na polisi huku?"

"Sasa hapo tutakuwa wapenzi kamili kazi kwako baba."

"Basi nitakuhamisha hapa, nitakupeleka Arusha ukale kuku. Wakija hapa hola." Akaongea Usonzo kwa furaha.

Walicheka pamoja na kugongesheana mikono.

"Na Enock je utakuwaje?" Lilikuwa ni swali la ghafla kutoka kwa Usonzo.

"Hilo niachie mimi. Kwani kanioa, ni mchumba tu? Na yeye ataachwa vile vile."

Kuna wakati Usonzo aliona kama anaota ndoto. msichana mrembo Mary aliyekuwa anamtoa udenda. Akamtongoza kwa njia zote, za kumlambisha asali na kutumia nguvu lakini zilidunda. Leo amemfuata mwenyewe ofisini na kila kitu kimeenda kama kilivyopangwa.

Alitaka kila kitu kitokee kwa muda mfupi ili awe ubavuni na mrembo huyo. Miezi mitatu aliiona ni mbali. Hata hivyo ilibidi kila kitu kiende kama kilivyopangwa na muda uliopangwa pia. Ilibidi tu awe mvumilivu.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO

# PARIMATCH YATOA BODABODA, YAHIMIZA WATEJA KUWANIA GARI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubahatisha ya Parimatch Tanzania imewasisitiza wateja wake kuendelea kushiriki katika kampeni yao ya 'Chomoka na Ndinga' ambayo imesalia wiki chache droo yake kuchezeshwa, ambapo mshindi wa gari mpya atapatikana na kutangazwa.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed wakati alipokuwa akizungumza kwenye hafla fupi ya kukabidhi zawadi ya pikipiki kutoka katika droo ya tatu ya shindano la Chomoka na Ndinga.

Ismael alisema hadi sasa wameshatoa zawadi ya simu 36 kwa washindi kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania pamoja na bodaboda 8 mpya aina ya Hero Hunter zenye ukubwa wa 125cc.

Washindi wa wiki ya pili ni Neema Tairo kutokea Sinza na Passian Kika kutokea Mabibo na washindi kwa wiki ya tatu ni Ahmad Omary kutokea Dar es Salaam pamoja na Kelvin Mansoor kutokea Mara.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Erick Gerald ameonesha kufarihishwa kwa ushindi wa Neema ambaye amekuwa mshindi wa kwanza kujishindia bodaboda tangu kuanza kwa mashindano hayo.

"Ushindi wa Neema unaonesha kuwa sasa michezo ya kubashiri inazidi kushika kasi na inazidi kukubalika katika jamii, hii ni motisha kwa wanawake na mabinti wote ambao walidhani michezo hii ni kwa ajili ya wanaume tu," alisema.

"Parimatch Tanzania wametoa fursa hii kwa watanzania wote, haijalishi jinsia, kama una umri wa miaka 18 na kuendelea jukwaa hili ni lako kujaribu bahati yako leo. Tembelea www.parimatch.co.tz na uweke mkeka wako, zimebaki wiki chache lakini zawadi ni nyingi sana na hapo bado kuna zawadi kubwa ya gari kutoka Toyota," aliongeza Erick.

Kwa wiki tatu sasa Parimatch kupitia droo yake ya Chomoka na Ndinga, imekua ikitoa zawadi za simu janja mbili kila siku na pikipiki mbili kila wiki.

Droo hiyo itafikia tamati wiki ya sita ambapo atatangazwa mshindi wa zawadi kubwa ya gari mpya kutoka Toyota! Tofauti na kampuni nyingine za kubashiri, Parimatch inakupa zawadi kwa kuweka ubashiri tu, bila kujali kuwa ubashiri wako umefanikiwa ama la. Nafasi yako ya ushindi inaongezeka unapobashiri zaidi.

Kwa upande mwingine, Kampuni ya Parimatch ndio kinara wa michezo ya kubashiri mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya 100% mpaka Sh 1,000,000 kwa wateja wapya wanaojiunga nasi! Parimatch imekuwepo nchini Tanzania tangu mwaka 2019, ikitoa huduma nzuri ikijumuisha malipo ya haraka, odds kubwa na promosheni za kusisimua kwenye soka, Kasino na Michezo ya virtual. Mbali na soka, kampuni ya Parimatch pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye tenisi, UFC, mpira wa vikapu, Kriketi, baseball na michezo mingine mingi ya Live na pre-match.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Parimatch Tanzania, Erick Gerald (wa pili kutoka kushoto), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kukabidhi zawadi kwa mshindi, Ahmad Pongalani na Neema Tairo. Wa pili kutoka kulia ni Norah Mapunda kutoka kampuni ya Hero. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# *Gwambina yapokwa pointi 15 Championship*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Gwambina imenyang'anywa pointi 15 kwenye Ligi ya Championship kwa kosa la kushindwa kufika kwenye kikao cha maandalizi ya mechi dhidi ya African Sports na baadaye kushindwa kufika kwenye Uwanja wa Nyamagana kwenye mechi dhidi ya timu hiyo.

Uamuzi huo umetolea na Kamati ya Uendeshaji na Usimamazi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) katika kikao chake cha Desemba 13 mwaka huu, ilipopitia mwenendo na matikio mbalimbali ya ligi hiyo.

Mbali kupokwa pointi hizo, Gwambina ambayo ilicheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, imetozwa faini ya shilingi milioni mbili kwa kosa hilo na kutoonekana au kuingia uwanja siku hiyo, huku African Sports ikizawadiwa pointi tatu na mabao matatu.

Hata hivyo, Gwambina mpaka sasa haijafikisha pointi hizo kwenye ligi hiyo, kwani ina pointi saba tu ikicheza mechi 11, ikishinda mechi mbili, sare moja na kupoteza michezo minane.

Kwa maana hiyo ni kwamba iwapo timu hiyo itaendelea kucheza mechi zake na kufikisha idadi ya pointi zinazotakiwa kutatwa, zitachukuliwa na kuanza upya huku ikiendelea kuhesabishwa michezo ambayo imeshacheza.

Wageni wa mechi hiyo iliyotakiwa kuchezwa Desemba 4, African Sports ya Tanga walifika mapema na kufuata taratibu zote, wakianza mazoezi ya kupata moto misuli kusubiri muda wa mchezo lakini wenyeji Gwambina hawakuonekana.

Timu hiyo inatumia uwanja huo, baada ya uwanja wake wa Gwambina Complex kufungiwa na Bodi ya Ligi kwa kutokidhi kanuni.

Mwamuzi wa kati aliyekuwa achezeshe mechi hiyo, Shomari Lawi, alikikagua kikosi cha African Sports na kufuata taratibu zote, ikiwa ni pamoja na kuwasubiri kwa dakika 30, kisha akapuliza kipenga cha kuashiria kusitisha mechi hiyo.

## Kocha Coastal ataka beki haraka, akikalia kuti kavu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Coastal Union, Yusuph Chipo ameilalamikia safu yake ya ulinzi kuwa ina matatizo akiwataka viongozi wa klabu hiyo kuingia sokoni haraka kumsajilia beki mmoja mkakamavu.

Wakati kocha huyo akipendekeza hivyo, zipo taarifa kuwa hata yeye mwenyewe amekalia kuti kavu baada ya juzi kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya KMC, mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, ikichezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

"Tuna tatizo sehemu ya ulinzi, yule jamaa alituliza mpira peke yake na ndiye aliyesababisha bao. Tunakwenda kwenye dirisha dogo inabidi tupate mtu pale nyuma, naamini tukipata beki makakamavu tutakuwa tumetibu tatizo,mpira una sehemu mbili, kuna kushambulia na kuzuia kwa hiyo pale nyuma inabidi tufanye jambo la haraka sana," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa uongozi wa Coastal Union una mpango wa kuachana na kocha huyo na makocha wawili Bakari Shime na Malale Hamsini huenda wakachukua nafasi yake.

Kocha huyo alichukua kijiti kutoka kwa Juma Mgunda ambaye kwa sasa ni Kaimu Kocha Mkuu wa Simba.

Coastal iko kwenye nafasi ya 12 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imeshacheza mechi 16 na pointi zake 15.

## KMKM kutumia Mapinduzi Cup kuimarisha kikosi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM imesema kuwa itatumia mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao katika mbio za kuetetea taji la ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

KMKM ni miongoni mwa timu sita kutoka Zanzibar ambazo zinashiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi linalotarajiwa kuanza Januari Mosi 2023.

Akizungumzia na gazeti hili Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ame Msimu alisema mbali na kutamani kufanya vizuri katika michuano hiyo, lakini pia mpango wao mwingine ni kuhakikisha timu hiyo inapata mbinu mpya.

Alisema mashindano hayo kwa upande wa Zanzibar yanamsaada mkubwa pale wanapokutana na timu za kutoka nje ya Zanzibar, kwani hutumika kwa ajili ya ujiimarisha.

"Sio mara ya kwanza kushiriki Kombe la Mapunduzi, lakini kila mashindano yanakuja na ukali wake, sisi kwa timu za Zanzibar kwetu ni faida kubwa kwakuwa ni mara chache sana kupata mechi na timu za nje," alisema.

Timu ya KMKM ipo nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar ikiwa na alama 29, ambapo katika michezo yake ya mzunguko wa kwanza imeshinda mara nane, imetoka sare mara tano na kufungwa mara mbili.

## ZISIKUPITE

**AMRABAT ATAKIWA LIVERPOOL**
WAWAKILISHI wa kiungo wa Fiorentina, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 26, wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco kujiunga na Liverpool. (***Football***)

**FOFANA AKARIBIA CHELSEA**
CHELSEA wanakaribia kumsajili mshambuliaji wa Ivory Coast, David Datro Fofana mwenye umri wa miaka 19 kutoka klabu ya Molde ya Norway kwa zaidi ya euro milioni 10. (***Fabrizio Romano, Twitter***)

**MUDRYK AZIDI KUWINDWA**
ARSENAL ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazofanya mazungumzo kuhusu mpango wa kumnunua winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk, lakini Shakhtar Donetsk wamesisitiza kuwa rais wao ndiye atakayeamua mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 - mara watakapopokea ofa yoyote rasmi. (***Mail***)

**BELLINGHAM EURO MIL 150**
KLABU ya Liverpool italazimika kulipa euro milioni 150 kwa kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 na karibu euro milioni 100 kwa kiungo wa kati wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21. (***Mundo Deportivo***)

**SAKA AWANIWA CITY**
MIPANGO ya baadaye ya Manchester City ya uhamisho inahusisha kujaribu kumsajili nyota wa Arsenal na England, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 21. (***90min***)

**FELIX ANAITAKA PSG**
MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 23 ambaye amepewa ofa ya kujiunga na klabu za Ligi Kuu ya England zikiwemo Arsenal na Manchester United, anataka kuchezea Paris St-Germain. (***Gianluca di Marzio Via Soccernews***)

**MOUKOKO MKATABA MPYA**
MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Youssoufa Moukoko mwenye umri wa miaka 18, anakaribia kusaini mkataba mpya na Borussia Dortmund licha ya Chelsea, Manchester United na Liverpool kumtaka. (***Ruhr Nachrichten Via Metro***)

**GAKPO AWINDWA**
KLABU za Manchester United na Newcastle United zinachuana na Real Madrid kuwania kumsajili winga wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23. (***Mirror***)

**CUNHA ANYATIWA**
KLABU ya Wolves italazimika kupambana na wapinzani wengi wa Ligi Kuu England kuwania saini ya mshambuliaji wa Brazil, Matheus Cunha mwenye umri wa miaka 23. (***90min***)

**LEAO AWANIWA MILAN**
KLABU ya Chelsea italazimika "kusukuma tena" kujaribu kumsajili fowadi wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23. (Givemesport)

**KUDUS KUTUA EVERTON**
EVERTON wanabakia katika nafasi nzuri ya kumsajili fowadi wa Ajax, Mohammed Kudus baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kucheza vyema katika michuano ya Kombe la Dunia akiwa na Ghana. (***Sky Sports Via Liverpool Echo***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEVILLE: SOUTHGATE ABAKI ENGLAND HADI EURO 2024

**●●● Adai ni kocha mwenye mafanikio na tayari amekibadilisha kikosi kwa kiasi kikubwa na...**

**LONDON,** England

GARETH Southgate anafaa kubakia kuwa kocha wa England kwenye Euro 2024 licha ya kutolewa katika robo fainali ya Kombe la Dunia, kwa mujibu wa Gary Neville.

Akiwa ameiongoza England maarufu kama Simba Watatu tangu mwaka 2016, Southgate tayari amejiimarisha kama kocha bora kuchukua mikoba tangu mshindi wa Kombe la Dunia 1966, Alf Ramsey, na alitinga nusu fainali Urusi 2018 na fainali ya Euro 2020.

Kichapo kwenye hatua ya robo fainali Qatar 2022 kimemfanya Southgate kutafakari mustakabali wake, ingawa amekiambia chama cha soka kuwa angependa kupata muda zaidi wa kufikiria.

Neville anaamini anafaa kubakia katika kampeni ya michuano mikubwa ijayo ya England na alipendekeza kuwa anaweza kutumia muda wa mwaka mmoja na nusu kusaidia kupata mrithi wa kufuata nyayo zake.

**"Kutakuwa na wale wanaosikiliza, ambao watasema, 'Lazima uwe na mtu ambaye anatuweka juu ya mstari, lazima uwe na mtu ambaye ana mawazo ya kushinda, lazima ubadilishe kocha'" alisema Neville akiiambia Sky Sports.**

"Nakumbuka tuliachana na Bobby Robson mwaka wa 1990. Nakumbuka tulimuondoa Terry Venables mwaka wa 1996.

"Haikuwa sawa baada ya mashindano hayo na nadhani Gareth amefanya kazi nzuri sana na anafaa kuwa kwenye michuano mingine mikubwa.


"Natumainoi, timu hii inaweza kushikamana na kubadilika. Nadhani ilibadilika katika mashindano haya. Tulikuwa na maendeleo zaidi, chanya zaidi katika mechi.

"Ameona yote, na nadhani anapaswa kuwekwa ndani ya mfumo kutengeneza siku zijazo. Ningependa abaki na FA zaidi ya jukumu lake la ukocha."

Southgate kwa sasa mkataba unamalizika baada ya michuano ya euro 2024.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,058,2
MECHI KALI
CROATIA
VERSUS
MOROCCO
1 | 2.29
X | 3.34
2 | 2.99
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

## URENO YAACHANA NA KOCHA SANTOS



**LISBON, Ureno**

FERNANDO Santos ameacha nafasi yake kama kocha mkuu wa Ureno, na kuhitimisha utawala ambao ulimfanya kuwa kocha mwenye mafanikio zaidi katika historia ya timu hiyo.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 68 anaondoka baada ya Ureno kuondolewa katika robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Morocco.

Awali Santos aliiongoza Ureno kutwaa ubingwa wa euro 2016 na ubingwa wa Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Kuondoka kwake kulithibitishwa na taarifa ya Shirikisho la Soka la Ureno, iliyosema: “FPF na Fernando Santos wamekubaliana kumaliza safari yenye mafanikio makubwa iliyoanza Septemba mwaka 2014.

“Baada ya moja ya ushiriki bora kuwahi kufanywa na timu ya taifa katika hatua ya mwisho ya Kombe la Dunia, huko Qatar, FPF na Fernando Santos wanaelewa kuwa huu ni wakati muafaka wa kuanza mzunguko mpya.

“Ilikuwa heshima kuwa na kocha na mtu kama Fernando Santos mkuu wa timu ya taifa.

“FPF inamshukuru Fernando Santos na timu yake ya ufundi kwa huduma zinazotolewa kwa muda wa miaka nane ya kipekee na inaamini kwamba shukrani hizi pia zitatolewa kwa niaba ya watu wa Ureno.”

Santos anaondoka wakati ambapo mashaka yamebakia iwapo Cristiano Ronaldo atarefusha maisha yake ya soka ya kimataifa.

Santos ilimpunguzia Ronaldo nafasi ya kucheza kwa Ureno katika mechi mbili za mtoano kwenye Kombe la Dunia, ushindi wa 6-1 dhidi ya Uswisi na kupoteza 1-0 kutoka kwa Morocco.

Santos baadaye alisema “sijutii” kutompa nafasi mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d’Or.

Mataji ambayo Santos alishinda akiwa na Ureno ndiyo pekee ya heshima kubwa nchini humo, baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Ufaransa kwenye fainali ya Euro

## Mpoland kuamua Argentina vs Ufaransa

**DOHA, Qatar**

SHIRIKISHO la soka la Kimataifa, Fifa, limethibitisha kwamba, Szymon Marciniak atakuwa mwamuzi wa fainali ya Kombe la Dunia Jumapili kati ya Argentina na Ufaransa.

Marciniak tayari amesimamia michezo ya miamba hiyo miwili iliyofika fainali nchini Qatar.

Alichezesha kwenye ushindi wa 2-1 wa Ufaransa katika hatua ya makundi dhidi ya Denmark na ushindi wa 16 bora wa Argentina dhidi ya Australia.

Mwamuzi huyo ambaye pia alichezesha mechi za Kombe la Dunia 2018 nchini Urusi, ameonesha kadi tano pekee za njano katika mechi zake mbili za michuano ya mwaka huu na bado hajatoa kadi nyekundu.




Baadhi ya waamuzi wamekosolewa kwa uchezaji wao katika hatua ya mtoano ya Kombe la Dunia, akiwemo Antonio Mateu Lahoz, aliyetoa kadi 15 za njano katika ushindi wa robo fainali ya Argentina dhidi ya Uholanzi.

Shirikisho la Soka la Morocco limewasilisha malalamiko kwa Fifa kuhusu uchezaji wa Cesar Ramos kama mwamuzi wakati wakifungwa kwenye nusu fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa, Jumatano.

FIFA pia ilitangaza kuwa mwamuzi wa Qatar, Abdulrahman Al Jassim atachezesha mchezo wa kuwania nafasi ya tatu Jumamosi kati ya Croatia na Morocco.

HABARI MICHEZO

211,696/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/12/22 | 19:30 | Aquila Montevarchi vs Rimini FC 1912 | 2.70 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 17/12/22 | 19:30 | Olbia Calcio vs Lucchese Libertas 1905 | 3.00 | 3.10 | 2.42 |
| 03. 17/12/22 | 20:00 | SC Pisa vs Brescia Calcio | 2.34 | 3.15 | 3.10 |
| 04. 17/12/22 | 20:00 | Akritas Chlorakas vs Nea Salamina Famagusta | 2.95 | 3.25 | 2.36 |
| 05. 17/12/22 | 21:30 | Beitar Jerusalem FC vs Maccabi Netanya FC | 2.90 | 3.25 | 2.42 |
| 06. 17/12/22 | 22:00 | Estrela Amadora vs FC Penafiel | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 07. 17/12/22 | 22:30 | Reggina 1914 vs SSC Bari | 2.36 | 3.05 | 3.15 |
| 08. 17/12/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.50 | 2.80 | 3.15 |
| 09. 18/12/22 | 07:00 | Western United FC vs Western Sydney Wanderers | 2.70 | 3.40 | 2.46 |
| 10. 18/12/22 | 13:30 | Bandirmaspor vs Pendikspor | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 11. 18/12/22 | 14:00 | CD Atletico Baleares vs Real Murcia CF | 2.32 | 3.10 | 3.15 |
| 12. 18/12/22 | 14:30 | Turris Calcio vs Calcio Foggia | 2.75 | 3.05 | 2.65 |
| 13. 18/12/22 | 15:45 | AO Egaleo 1931 PAE vs Chania Kissamikos | 2.33 | 2.95 | 3.30 |
| 14. 18/12/22 | 16:00 | Cosenza Calcio vs Ascoli Calcio 1898 | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 15. 18/12/22 | 16:00 | Modena FC vs Benevento Calcio | 2.41 | 3.10 | 3.00 |
| 16. 18/12/22 | 20:45 | Palermo FC vs Cagliari Calcio | 2.70 | 3.15 | 2.65 |
| 17. 18/12/22 | 21:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.36 | 2.90 | 3.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 17/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 5204 | Aberdeen vs Celtic | 6.57 | 4.98 | 1.38 |
| 16:00 | 1694 | Hapoel Tel Aviv vs Hapoel Haifa | 1.94 | 3.25 | 3.60 |
| 16:00 | 2349 | Hapoel Hadera vs Hapoel Katamon | 2.82 | 3.02 | 2.41 |
| 16:00 | 3629 | Sakaryaspor vs Genclerbirligi | 1.68 | 3.70 | 4.29 |
| 18:00 | 1012 | Yeovil vs Dorking Wanderers | 1.87 | 3.60 | 3.50 |
| 18:00 | 1050 | Hearts vs Kilmarnock | 1.77 | 3.54 | 4.38 |
| 18:00 | 1527 | Queen of South vs Kelty Hearts FC | 1.80 | 3.66 | 3.91 |
| 18:00 | 1600 | Bristol City vs Stoke City | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 18:00 | 1626 | Hull City vs Sunderland | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 18:00 | 1632 | Raith Rovers vs Arbroath | 1.96 | 3.34 | 3.64 |
| 18:00 | 1802 | Huddersfield vs Watford | 3.47 | 3.27 | 2.05 |
| 18:00 | 1857 | Peterborough vs Shrewsbury | 1.97 | 3.42 | 3.57 |
| 18:00 | 1896 | Ross County vs St Johnstone | 2.64 | 3.09 | 2.69 |
| 18:00 | 2137 | Croatia vs Morocco | 2.29 | 3.34 | 2.99 |
| 18:00 | 2129 | Derby vs Forest Green | 1.42 | 4.45 | 6.53 |
| 18:00 | 2471 | West Bromwich vs Rotherham | 1.42 | 4.36 | 6.93 |
| 18:00 | 2937 | Cardiff vs Blackpool | 1.83 | 3.42 | 4.17 |
| 18:00 | 3224 | Bolton vs Exeter | 2.11 | 3.37 | 3.22 |
| 18:00 | 3426 | Burnley vs Middlesbrough | 2.11 | 3.28 | 3.33 |
| 18:00 | 3562 | Charlton vs Bristol Rovers | 2.20 | 3.38 | 3.03 |
| 18:00 | 3640 | Motherwell vs St Mirren | 2.24 | 3.18 | 3.18 |
| 18:00 | 3840 | Wycombe vs Ipswich | 3.86 | 3.46 | 1.88 |
| 18:00 | 4166 | Cheltenham vs Lincoln | 2.49 | 3.13 | 2.79 |
| 18:00 | 4242 | Peterhead vs Clyde | 2.57 | 3.26 | 2.57 |
| 18:00 | 4454 | Edinburgh City vs Montrose | 2.86 | 3.45 | 2.25 |
| 18:00 | 4524 | Barnsley vs Burton | 1.95 | 3.47 | 3.57 |
| 18:00 | 4610 | Livingston vs Dundee Utd | 2.01 | 3.28 | 3.68 |
| 18:00 | 4658 | Dundee FC vs Cove Rangers | 1.47 | 4.34 | 5.72 |
| 18:00 | 4679 | Hamilton vs Inverness | 2.38 | 3.36 | 2.72 |
| 18:00 | 4929 | Alloa Athletic vs Falkirk FC | 2.66 | 3.35 | 2.44 |
| 18:00 | 5006 | Sheffield Wed vs Oxford Utd | 1.69 | 3.77 | 4.46 |
| 18:00 | 5187 | Morton vs Queens Park | 2.07 | 3.50 | 3.16 |
| 18:00 | 5363 | Partick Thisle vs Ayr United | 2.22 | 3.45 | 2.91 |
| 18:00 | 5505 | Plymouth vs Morecambe | 1.50 | 4.27 | 5.57 |
| 18:00 | 5545 | Coventry vs Swansea | 2.38 | 3.22 | 2.87 |
| 18:00 | 5674 | Portsmouth vs MK Dons | 1.97 | 3.43 | 3.58 |
| 18:00 | 5701 | Preston vs QPR | 2.27 | 3.18 | 3.08 |
| 18:00 | 5997 | Fleetwood Town vs Cambridge Utd | 2.32 | 3.26 | 2.92 |
| 18:15 | 5463 | Mirandes vs Ponferradina | 2.07 | 3.27 | 3.42 |
| 18:15 | 5628 | Lugo vs Granada | 3.62 | 3.13 | 2.06 |
| 19:00 | 1850 | Eyupspor vs Boluspor | 1.70 | 3.60 | 4.28 |
| 19:00 | 3138 | Young Africans vs Polisi Tanzania | 1.16 | 5.82 | 14.55 |
| 20:00 | 4868 | Pisa vs Brescia | 2.31 | 3.11 | 3.06 |
| 20:30 | 1583 | Norwich City vs Blackburn | 1.78 | 3.53 | 4.27 |
| 20:30 | 2077 | Villarreal B vs Las Palmas UD | 3.31 | 3.12 | 2.19 |
| 20:30 | 3871 | FC Cartagena vs Racing Santander | 1.96 | 3.11 | 4.05 |
| 21:30 | 3009 | FC Ashdod vs Hapoel Beer Sheva | 3.89 | 3.45 | 1.81 |
| 21:30 | 3398 | Beitar Jerusalem vs Maccabi Netanya | 2.81 | 3.15 | 2.34 |
| 22:30 | 2784 | Reggina vs Bari | 2.12 | 3.12 | 3.47 |
| 23:00 | 3447 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.68 | 2.78 | 2.88 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS ZATUMIANA SALAMU LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI zikitarajiwa kupamba Desemba 22 kwenye mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu ya soka ya Wanawake Tanzania Bara, timu za Simba Queens na Yanga Princess zimetumiana salamu kuelekea 'dabi' hiyo kila timu ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye mechi zao.

Kwenye Uwanja wa Black Rhino, Karatu Arusha, Simba Queens ilichakaza The Tigers Queen mabao 4-0 kwenye mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu, baada ya kuchapwa bao 2-1 dhidi ya JKT Queens kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam.

Baada ya kichapo hicho, Simba Queens haikuwa na mzaha tena, ikaichakaza timu hiyo juzi kwa mabao ya Opa Clement akifunga mawili na Pambani Kuzoya pia akifunga mawili.

Yanga Princess ambayo ilichapwa bao 1-0 kwenye mechi ya ufunguzi dhidi ya Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Uhuru na kusababisha kutimuliwa kwa benchi la ufundi likiongozwa na Edna Lema, ilisawazisha makosa yake juzi kwenye uwanja huo huo, ikitoa kipigo cha mabao 4-0 dhidi ya Mkwawa Queens.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Fred Mbuna amesema kwenye mechi ya kwanza walifanya makosa, lakini kwa sasa wamejirekebisha na kupata matokeo hayo.

Kocha Mkuu wa Mkwawa Queens, Miraji Fundi alisema kuwa kipigo hicho kimetokana na ugeni wa timu yake kwenye ligi kwani imepanda msimu huu.

"Timu yangu ugeni wa mashindano, tumepanda msimu huu hatukusajili, tumetumia wachezaji wale wale, tena na wengine wamechukuliwa na timu zingine, malengo yetu msimu huu tusishuke daraja," alisema kocha huyo za zamani wa Sayari Queens.

Baada ya kila mmoja kushinda mabao 4-0, Alhamisi ijayo timu hizo mbili zinakutana kwenye uwanja ambao bado haujapangwa, ikiwa ni raundi ya tatu ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Mechi zingine zilizochezwa juzi ni Alliance Girls ambayo ilikuwa kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza ikitoka suluhu dhidi ya JKT Queens, Baobab ikiishindilia Ceasiaa Queens mabao 2-1, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, na Amani Queens ikiwa nyumbani ilikubali kupigo cha mabao 4-0 dhidi ya Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Nyangao Sekondari, Lindi.

# TRY AGAIN: MASHABIKI

INATOKA UK. 32

wa Simba ukimuuliza atakwambia maeneo ambayo timu yake inatakiwa kuyapa nguvu. Ni ushambuliaji, kiungo mkabaji na baadhi ya maeneo ambayo baadhi ya wachezaji wanahitaji msaada wa kuongezewa nguvu," alisema Ahmed.

Wakati huo huo wachezaji John Bocco na Aishi Manula wamewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kujiandaa kuwapa tafu kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ajili ya kuhakikisha wanachukua pointi zote tisa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kama ilivyo kawaida yao.

Nahodha wa timu hiyo, Bocco alisema timu zote zilizo kwenye kundi hilo ambazo ni Horoya ya Guinea, Raja Casablanca ya Morocco na Vipers ya Uganda ni nzuri, lakini haiwafanyi kujiandaa na mkakati wa kutimiza malengo yao waliojiwekea.

"Kikubwa mimi nayaangalia mashindano kwa ujumla, tumejiwekea malengo kama klabu kuwa tunatakiwa tufikie hatua fulani, kikubwa tuzingatie aina ya mpinzani tunayekwenda kucheza naye, kwa kipindi hiki cha miaka mitatu minne ambayo tumecheza michuano hii, kuna uzoefu ambao tumeupata unaoweza kutusaidia kuweza kufikia malengo yetu ya msimu huu," alisema straika huyo.

Manula aliwataka wanachama na mashabiki kungana pamoja na wachezaji kuhakikisha michezo ya nyumbani wanapata ushindi kama ambavyo huwa wanafanya miaka yote wanayoshiriki.

"Tumepata kundi gumu, inabidi tufanye kazi ya ziada ili tufikie malengo tuliyojiwekea, siyo kundi ambalo baadhi ya watu wanaong'ona kuwa linaweza kuwa jepesi, mimi natumaini ni kundi gumu ni lazima tufanye kazi, tukubali kujitolea tukishiriakiana na mashabiki kuhakikisha michezo ya nyumbani tunapata kile kitu ambacho siku zote tunafanya kwenye uwanja wa nyumbani," alisema kipa huyo.

# YANGA KAZI

INATOKA UK. 32

tukiwa katika hali nzuri kwa sababu wachezaji wetu wote wako fiti hata wale majeruhi wamepona, nina imani utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa," alisema Kaze.

Alisema kuwepo nafasi ya chini kwa Polisi sio jambo la msingi kwao zaidi ya kuona mabadiliko makubwa kwa wapinzani wao hao kwa sababu ya jinsi walivyowaona katika mechi iliyopita.

Nahodha wa Yanga, Zawadi Mauya alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya wapinzani wao wako katika nafasi ya chini katika msimamo na wanahitaji kujiondoa walipo.

"Mechi itakuwa ya ushindani hatutaingia kwa kuwadharau kwa sababu ya kuwepo katika nafasi ya chini, kwani wamejipanga kutafuta matokeo mazuri kujiondoa katika nafasi waliyopo," alisema Mauya.

Kwa upande wa kocha msaidizi wa Polisi, John Tamba alisema kiufundi timu yao iko vizuri kuhakikisha wanakwenda kutafuta pointi muhimu dhidi ya Yanga.

Alisema mzunguko wa kwanza hawakufanya vizuri na sasa duru la pili wamekuja kivingine kuhakikisha wanakuwa makini katika mchezo huo kwa kupata matokeo chanya ili kujitoa mkiani.

"Tunafahamu ubora wa wapinzani wetu, tumefanyia kazi mapungufu yetu kwa kuimarisha kila idara ili kuanza vizuri mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya Yanga, tunawaheshimu na wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupaga matokeo," alisema Tamba.

Mwakilisi wa wachezaji wa Polisi, Jeremiah Kisubi alisema wamejiandaa vizuri na amewataka mashabiki wao wajitokeze uwanjani kwa sababu wanaimani ya kupata matokeo mazuri.

"Tumejipanga vizuri na kesho (leo) tunaenda kuanza ligi, tumejiandaa vizuri kuhakikisha hatufanyi makosa yoyote, hatuko katika nafasi nzuri katika msimamo na leo tunahitaji kupata matokeo chanya, ili kujiondoa tulipo," alisema Kisubi.

# Michezo

Jumamosi Desemba 17, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Neville: Southgate abaki England hadi euro 2024

# YANGA KAZI NI ILE ILE

## ●●●Inashuka dimbani leo kuanza mzunguko wa pili ikiivaa Polisi huku...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga leo kitashuka dimbani kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania dhidi ya Polisi Tanzania.

Yanga itashuka dimbani huku ikiwa chini ya Kocha wake Mkuu, Nasreddine Nabi aliyekosekana kwenye benchi katika michezo mitatu iliyopita.

Nabi alikuwa anatumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu na kulipa faini Sh. 500,000 baada ya kukutwa na hatia ya kuwashambulia waamuzi wa mchezo wao dhidi ya Ihefu FC, ulifanyika Mbarali Mbeya.

Kocha huyo alikosekana katika mchezo dhidi ya Prisons, Namungo FC na kwenye mchezo wa kombe la FA dhidi ya Kurugenzi FC.

Katika mchezo wa leo Nabi ataongoza kikosi cha timu hiyo kinachoshuka dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Polisi ambayo kwa sasa inanolewa na Mwinyi Zahera aliyewahi kuwa kocha wa Yanga.

Yanga inashuka dimbani ikiwa na nia moja tu ya kuendeleza wimbi la ushindi kama ilivyokuwa kwenye mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ambapo hadi sasa ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 38 baada ya mechi 15.


Wakati Polisi inalazimika kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo kujiondoa kwenye nafasi ya chini katika msimamo.

Kuelekea mchezo huo, msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze amesema mechi itakuwa tofauti na wanatarajia mchezo utakuwa mgumu na wa ushindani.

Alisema wamewaona Polisi walivyocheza na Azam kwamba wamekuwa na mabadiliko makubwa kiuchezaji na ufundi kwa sababu wameonyesha ushindani mkubwa.

"Kwa upande wetu tunaanza duru la pili

INAENDELEA UK. 31



Wachezaji wa Yanga, Khalid Aucho na Stephane Aziz Ki wakiwa kwenye mazoezi: **PICHA: YANGA**

## Try Again: Mashabiki wa Simba puuzeni usajili wa Miquissone

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Bodi wa Klabu ya Simba, Salim Abdallah maarufu 'Try Again' amethibitisha rasmi kuwa klabu hiyo itafanya usajili kwenye dirisha dogo ambalo limefunguliwa, huku akiwataka wanachama na mashabiki kupuuzia tetesi za kurejea kwa Luis Miquissone.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, mwenyekiti huyo alisema kuwa klabu hiyo itafanya usajili kwenye maeneo machache ya kuziba au kuongezea pale panapoonekana kuna mapungufu.

"Ni kweli taarifa rasmi ni kwamba Simba itafanya usajili na hii ni kwa kulingana na ripoti ya wataalam wetu kuboresha pale panapoonekana pana mapungufu kwa hiyo wananchama na mashabiki wetu wasiwe na wasiwasi, watafurahi," alisema Try Again.

Kuhusu wachezaji ambao wanatajwa sana kusajiliwa na klabu hiyo alisema yeye hawezi kusema chochote bali muda utaamua kwa sababu usajili ni jambo la kitaalam.

"Kazi hii ni ya kitaalam kwa hiyo tuwaachie wataalam, kama ni Cesar Manzoki, Victorien Adebayor, Saido na wengine wanaotajwa kama ni kweli au si kweli, basi tutaona nani ameingia kwenye kikosi chetu," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kupuuza taarifa za kurejea kwa Miquissone akidai bado ni mchezaji halali wa Al Ahly ya Misri na popote anapokwenda kucheza anakwenda kwa mkopo.

"Bado wanachama na mashabiki wetu wanafanya kosa lile lile,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042